NDAKI YA ELIMU
SKULI YA ELIMU

# MCHANGO WA TEHAMA KATIKA UFUNDISHAJI WA FASIHI ANDISHI YA KISWAHILI KATIKA SHULE ZA SEKONDARI TEULE WILAYANI NYAGATARE NCHINI RWANDA

**NA**

**TULINUMUKIZA FRODOUARD**

**222011736**

**TASNIFU ILIYOWASILISHWA KWA AJILI YA KUKAMILISHA MAHITAJI YA SHAHADA YA UMAHIRI WA ELIMU KATIKA KISWAHILI NA ELIMU YA CHUO KIKUU CHA RWANDA, NDAKI YA ELIMU**

**OKTOBA, 2024**

## IKIRARI NA HAKIMILIKI

Mimi, **Tulinumukiza Frodouard,** ninathibitisha kuwa tasnifu hii ni kazi yangu ya asilia na haijawahi kuwasilishwa katika chuo kikuu chochote kwa ajili ya kutunukiwa shahada.

Tulinumukiza Frodouard

(Mtafiti)

Tarehe: 10/10/2024

## ITHIBATI YA MSIMAMIZI

Aliyetia saini hapa chini anathibitisha kuwa tasnifu yenye anwani **“Mchango wa TEHAMA katika Ufundishaji wa Fasihi Andishi katika Shule za Sekondari Wilayani Nyagatare Nchini Rwanda”,** ameisoma na anapendekeza ikubaliwe kwa ajili ya kutunukiwa Shahada ya Umahiri wa Elimu katika Kiswahili na Elimu ya Chuo Kikuu cha Rwanda, Ndaki ya Elimu.

Dkt. Wallace Kapele Mlaga (PhD)

(Msimamizi)

Tarehe: /10/2024

## SHUKRANI

Ninatoa shukrani za dhati kwa Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha kuwa hai na kukamilisha masomo yangu. Namshukuru msimamizi wangu, Dkt. Wallace Kapele Mlaga, kwa mwongozo na ushauri wake mzuri wa kitaalama ambao uliniwezesha kukabiliana na changamoto mbalimbali na kukamilisha tasnifu hii. Ujuzi wake wa thamani na bidii yake vimeniongoza kwa mafanikio. Pia, ninamshukuru shemeji yangu, Ndikubwimana Jean de Dieu na kaka yangu, Nyiramahirwe Peace, ambao walinipa motisha na pongezi nyingi pamoja na upendo usio na kikomo katika safari yangu ya masomo. Nawashukuru kutoka moyoni mwangu kwa msaada wao mkubwa na kuwaombea baraka nyingi.

Ninawashukuru wazazi wangu, Rwasamanzi Dominique na Mukakomine Pluscule, kwa kunilea na kunipa kila kitu kilichohitajika ili maisha yangu yawe mazuri. Mungu awabariki na kuwapa furaha maishani mwao. Mwisho, ninatoa shukrani zangu za dhati kwa marafiki na ndugu zangu wote ambao walinisaidia kwa hali na mali katika safari yangu ya masomo. Mungu awabariki sana ndugu zangu wapendwa.

# TABARUKU

Ninawashukuru sana wazazi wangu, Rwasamanzi Dominique na Mukakomine Pluscule, kwa upendo wao na msaada wao wa daima. Hawa ni faraja na nguzo imara katika maisha yangu.

# IKISIRI

Utafiti uliofanyika ulilenga kuchunguza mchango wa TEHAMA katika ufundishaji wa fasihi andishi katika shule za sekondari wilayani Nyagatare nchini Rwanda. Uchunguzi huu ulifanyika kwa kutimiza malengo mahususi mawili. Kwanza, kubainisha mchango wa TEHAMA katika ufundishaji wa fasihi andishi katika shule za sekondari teule wilayani Nyagatare nchini Rwanda. Pili, kuunda miongozo ya utumiaji wa TEHAMA ili kuleta ufanisi wa ufundishaji wa fasihi katika shule za sekondari wilayani Nyagatare nchini Rwanda. Ili kutimiza malengo haya, utafiti uliongozwa na Nadharia ya Uunganisho. Mbinu ya usaili, ushuhudiaji na uchanganuzi matini zilitumiwa ili kukusanya data. Wango la utafiti lilikuwa, viongozi wa shule, wakuu wa masomo, walimu wa Kiswahili na wanafunzi wa mchepuo wa LFK. Sampuli ya utafiti ilihusisha wanafunzi 103, walimu wa Kiswahili kumi, wakuu wa masomo watano na wakurugenzi watano ambao waliteuliwa kwa kutumia mbinu ya usampulishaji lengwa. Data za utafiti zilichanganuliwa, kufasiliwa na kuwasilishwa kwa kutumia njia ya madondoo na maelezo. Matokeo ya utafiti yameonesha kwamba TEHAMA ina mchango mkubwa katika ufundishaji wa fasihi andishi katika shule za sekondari teule wilayani Nyagatare kwa sababu zifuatazo: Kwanza, TEHAMA inaleta urahisi katika upatikanaji wa nyenzo za ufundishaji na ujifunzaji kama vitabu vya kielektroniki na video za ufafanuzi. Pili, TEHAMA inawezesha wanafunzi kujifunza fasihi andishi ya Kiswahili kwa kuwaunganisha na wanafunzi wengine duniani kote kupitia mitandao ya kijamii na tovuti tofauti. Tatu, TEHAMA inawezesha wanafunzi kujifunza stadi mpya zinazohitajika katika fasihi andishi kama vile stadi ya ubunifu na kutafakari kitunduizi. Nne, TEHAMA inawapa wanafunzi motisha ya kujifunza fasihi andishi ya Kiswahili. Mwisho, matokeo ya utafiti yameonesha kwamba matumizi ya TEHAMA yanarahisisha ufundishaji wa fasihi andishi ya Kiswahili kwa sababu wanafunzi huvutiwa zaidi kwa kutumia vifaa vya kidijiti kama vile simu na kompyuta. Zaidi ya hayo, matokeo ya utafiti yamebainisha changamoto za ufundishaji wa fasihi andishi ya Kiswahili kupitia TEHAMA katika shule za sekondari teule wilayani Nyagatare. Changamoto hizo ni ukosefu wa zana za kufundishia na mbinu za ufundishaji zinazotumiwa na walimu. Isitoshe, matokeo ya utafiti yametoa miongozo ya utatuaji wa zana za kufundishia fasihi andishi ya Kiswahili kupitia TEHAMA katika shule za sekondari wilayani Nyagatare nchini Rwanda. Miongozo hii unahusisha utumiaji wa projekta na slaidi, usimulizi wa kidijiti na mitandao ya kijamii. Mwisho, ili kukabiliana na changamoto za ufundishaji wa fasihi andishi ya Kiswahili kupitia TEHAMA, matokeo ya utafiti yamependekeza mbinu tofauti za ufundishaji wa fasihi andishi ya Kiswahili na kutilia mkazo kwenye maandalizi ya warsha za matumizi ya TEHAMA na kuimarisha miundombinu ya TEHAMA shuleni.

**Maneno ya Msingi**: *TEHAMA, Fasihi Andishi, Ufundishaji, Shule za Sekondari*

# YALIYOMO

IKIRARI NA HAKIMILIKI ........ ii
ITHIBATI YA MSIMAMIZI ........ iii
SHUKRANI ........ iv
TABARUKU ........ v
IKISIRI ........ vi
ORODHA YA MAJEDWALI ........ x
ORODHA YA VIFUPISHO ........ xi
SURA YA KWANZA: UTANGULIZI ........ 1
1.1 Utangulizi ........ 1
1.2 Usuli wa Tatizo la Utafiti ........ 1
1.3 Tamko la Tatizo la Utafiti ........ 5
1.4 Malengo ya Utafiti ........ 5
1.4.1 Lengo la Jumla ........ 6
1.4.2 Malengo Mahususi ........ 6
1.5 Maswali ya Utafiti ........ 6
1.6 Umuhimu wa Utafiti ........ 6
1.7 Mawanda ya Utafiti ........ 7
1.7.1 Mawanda ya Kimaudhui ........ 7
1.7.2 Mawanda ya Kijiografia ........ 7
1.7.2 Mawanda ya Kimuda ........ 8
1.8 Vikwazo vya Utafiti na Utatuzi Wake ........ 8
1.9 Mpangilio wa Ripoti ya Utafiti ........ 9
1.10 Muhtasari wa Sura ya Kwanza ........ 9
SURA YA PILI: MAPITIO YA MAANDIKO ........ 10
2.1 Utangulizi ........ 10
2.2 Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji wa Fasihi ........ 10
2.2.1 Namna Ufundishaji na Ujifunzaji wa Fasihi Unavyofanyika ........ 10
2.2.2 Changamoto za Ufundishaji na Ujifunzaji wa Fasihi ........ 15
2.3Mchango wa TEHAMA katika Ufundishaji na Ujifunzaji wa Stadi za Lugha ........ 20

2.4 Mchango wa TEHAMA katika Ufundishaji na Ujifunzaji wa Fasihi Andishi .................. 23
2.5 Miongozo ya Utumiaji wa TEHAMA katika Ufundishaji wa Fasihi Andishi .................. 25
2.5.1 Utumiaji wa Projekta na Slaidi .................. 25
2.6.2 Utumiaji wa Usimulizi wa Kidijiti .................. 27
2.6.3 Utumiaji wa Mitandao ya Kijamii .................. 28
2.7. Mapengo ya Tafiti Tangulizi .................. 29
2.8. Nadharia ya Utafiti .................. 30
2.9. Muhtasari wa Sura ya Pili .................. 31
SURA YA TATU: METHODOLOJIA YA UTAFITI .................. 32
3.1 Utangulizi .................. 32
3.2 Paradima ya Utafiti .................. 32
3.3 Usanifu wa Utafiti .................. 33
3.4 Eneo la Utafiti .................. 33
3.4 Wango na Sampuli ya Utafiti .................. 34
3.4.1 Wango la Utafiti .................. 34
3.4.2 Sampuli ya Utafiti .................. 34
3.5 Mbinu za Ukusanyaji wa Data .................. 35
3.5.1 Usaili .................. 36
3.5.2 Ushuhudiaji .................. 36
3.5.3 Uchanganuzi wa Matini .................. 36
3.6 Aina ya Data Zilizokusanywa .................. 37
3.6.1 Data za Msingi .................. 37
3.6.2 Data za Upili .................. 37
3.7 Vifaa vya Utafiti .................. 37
3.8 Uchanganuzi wa Data .................. 38
3.9 Itikeli za Utafiti .................. 38
3.10 Uhalali na Uthabiti wa Utafiti .................. 39
3.11 Mpango Kazi .................. 40
3.12 Muhtasari wa Sura ya Tatu .................. 41
SURA YA NNE : MJADALA NA UWASILISHAJI WA MATOKEO YA UTAFITI .................. 42

4.1 Utangulizi ........ 42
4.1 Mchango wa TEHAMA katika Ufundishaji wa Fasihi Andishi ya Kiswahili katika Shule za Sekondari ........ 42
4.1.1 TEHAMA Inawasaidia Wanafunzi Kufikia Kazi za Fasihi Andishi ya Kiswahili na Vyanzo vya Kitaaluma kwa Urahisi ........ 42
4.1.2 TEHAMA Inawaunganisha Wanafunzi wa Fasihi na Wanafunzi Wengine ........ 45
4.1.3 TEHAMA Inawasaidia Wanafunzi Kukuza Stadi Muhimu Zinazohitajika katika Masomo ya Fasihi Andishi ........ 48
4.1.4 TEHAMA Inawapa Wanafunzi Motisha ya Kujifunza Fasihi Andishi ........ 50
4.2 Miongozo ya Utumiaji wa TEHAMA katika Ufundishaji wa Fasihi Andishi ya Kiswahili52
4.3.1 Mwongozo wa Utumiaji wa Projekta na Slaidi ........ 52
4.3.2 Mwongozo wa Utumiaji wa Usimulizi wa Kidijiti ........ 54
4.3.3 Mwongozo wa Utumiaji wa Mitandao ya Kijamii ........ 56
4.4 Muhtasari wa Sura ya Nne ........ 58
SURA YA TANO: MUHTASARI WA MATOKEO YA UTAFITI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO ........ 59
5.1 Utangulizi ........ 59
5.2 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti ........ 59
5.2.1 Lengo Mahususi la Kwanza ........ 59
5.2.2 Lengo Mahususi la Pili ........ 60
5.3 Ufaafu wa Nadharia ya Utafiti Iliyotumika ........ 61
5.4 Hitimisho ........ 62
5.5 Mapendekezo ........ 63
5.5.1 Mapendekezo kwa Wanafunzi ........ 63
5.5.2 Mapendekezo Walimu wa Kiswahili ........ 63
5.5.2 Mapendekezo kwa Wizara ya Elimu ya Rwanda ........ 64
5.5.3 Mapendekezo kwa Tafiti Zijazo ........ 64
5.4 Muhtasari wa Sura ya Tano ........ 64
MAREJELEO ........ 65
VIAMBATISHO ........ 72

# ORODHA YA MAJEDWALI

Jedwali 1: Mpango Kazi ........................................................................................................ 40

# ORODHA YA VIFUPISHO

**Dkt**: Daktari wa Falsafa (PhD)

**ES**: Ecole Secondaire

**GS**: Groupe Scholaire

**khj**: Keshatajwa hapo juu

**LFK**: Literature in English, French, Kinyarwanda and Kiswahili

**TEHAMA**: Teknolojia ya Habari na Mawasiliano

**TY**: Tafsiri Yetu

**whj**: Wameshatajwa hapo juu

# SURA YA KWANZA: UTANGULIZI

## 1.1 Utangulizi

Sura ya kwanza inalenga kutoa taarifa za msingi kuhusu utafiti uliofanyika. Kwa hiyo, sehemu zinazojenga sura hii ni utangulizi, usuli wa tatizo la utafiti, tamko la tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti. Aidha, surah ii inashughulika na umuhimu, mawanda, vikwazo vya utafiti, mpangilio wa ripoti ya utafiti na muhtasari wa sura ya kwanza.

## 1.2 Usuli wa Tatizo la Utafiti

TEHAMA ni teknolojia ya habari na mawasiliano inayojumuisha utafiti, miradi, mafanikio, msaada na utawala wa mifumo ya habari ya kompyuta, hasa programu na vifaa vya kompyuta (Mishra & Koehler, 2006). TEHAMA ni mchakato wa kusasisha, kulinda, kukuza, na kusambaza habari kwa msaada wa kompyuta za elektroniki na programu za kompyuta. TEHAMA pahali pote duniani na katika karne hii ya 21, inazidi kuendelea haraka ukilinganisha na enzi zilizotangulia karne hii (Meskills & Ranglova, 2000).

Aidha, Wamitila (2003) anasema kwamba, fasihi ni aina ya sanaa inayojumuisha matumizi ya lugha na maneno kwa lengo la kueleza hisia, mawazo na malengo ya wanajamii. Maelezo haya yanamaanisha kwamba fasihi ni njia ya ubunifu inayowezesha watu kutoa maoni yao, kuwasilisha hadithi au kueleza uzoefu wa maisha ya wanajamii kwa kutumia lugha yenye umbo na muundo wa pekee. Fasihi ina tanzu mbili ambazo ni fasihi simulizi na fasihi andishi. Kwa mujibu wa Njogu & Chimerah (1999) fasihi andishi ni aina ya fasihi inayopatikana kwa maandishi, ambayo huandikwa na kuchapishwa kwa kutumia mfumo wa maandiko. Hii inajumuisha mashairi, riwaya, hadithi fupi, tamthilia na aina nyinginezo za maandishi maandiko.

Kupitia fasihi andishi, watu wanaweza kugusa hisia za wasomaji kuhamasisha mawazo na kutoa picha halisi au taswira za jamii na tamaduni zao. Fasihi ni kioo cha maisha. Kwa maana kwamba, mtu anaweza akajitazama, akaona taswira yake na akajirekebisha (Nkwera, 1970). Fasihi andishi ina jukumu kubwa katika kudumisha, kueneza na kuchunguza utamaduni na maisha ya kijamii. Kwa hiyo, ufundishaji wa fasihi ni jambo ambalo ni lazima litiliwe manani.

Hivyo basi, tumeona kwamba kuna haja ya kuchunguza hali ya ujumuishaji wa TEHAMA katika ufundishaji wa fasihi. Hii ni kwa sababu TEHAMA inaweza kuongeza ufanisi wa ufundishaji kwa kutoa njia za kuvutia za kusoma na kuelewa maudhui ya fasihi (Karantalis & Koukopoulos, 2022). Ndiyo maana tuliamua kufanya utafiti ili tuchunguze mchango wa TEHAMA katika ufundishaji wa fasihi andishi katika shule za sekondari teule wilayani Nyagatare. Tuliamua kufanya utafiti kuhusu fasihi andishi na kuacha fasihi simulizi kwa sababu zama za sasa na katika ulimwengu wa kiutandawazi, walimu na wanafunzi hupenda kutumia mitandao ya kijamii na tovuti tofauti katika ufundishaji na ujifunzaji wa fasihi andishi ya Kiswahili kupitia zana za kidijiti.

Kwa mujibu wa Ratheeswari (2018), TEHAMA imepata umaarufu mkubwa katika sekta ya elimu kutokana na umuhimu wake wa kuboresha mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Wataalamu wa elimu wamekuwa wakisisitiza umuhimu wa kujumuisha kwa TEHAMA katika mifumo ya elimu ili kufanikisha malengo ya ufundishaji na ujifunzaji wa kisasa. TEHAMA inatoa msaada muhimu kwa walimu na wanafunzi, ikiboresha njia za kufundisha na kujifunza (Ratheeswari, khj).

Hii inaonesha jinsi TEHAMA inavyochukuliwa kama nyenzo muhimu ya kufanikisha elimu katika nchi mbalimbali. Kwa kutoa fursa za ubunifu, ufikiaji rahisi wa taarifa, na mawasiliano bora, TEHAMA inachangia kwa kiasi kikubwa katika kuandaa vizazi vya wanafunzi wenye uwezo wa kukabiliana na changamoto za dunia ya kidigiti. Hivyo basi, Ratheeswari (2018) anasema kwamba nchi tofauti zimepata uamuzi wa kujumuisha TEHAMA katika elimu ili kudumisha mafanikio ya shughuli za ufundishaji na ujifunzaji.

Nchini Urusi, TEHAMA ina jukumu muhimu katika kutoa elimu kwa wanasayansi na wataalamu wa nyanja mbalimbali. Kama inavyodhihirishwa na Schauman (2001), matumizi ya TEHAMA yanalenga kuongeza ustadi wa kidigiti kwa umma. Historia ndefu ya Urusi katika uwanja wa viwanda na teknolojia imesababisha serikali kuwekeza kwa nguvu katika kukuza idara imara za kiteknolojia (Koroleva, 2020).

Kufanya sayansi ya kompyuta kuwa somo la lazima katika ngazi zote za elimu ni hatua muhimu inayolenga kuhakikisha kuwa raia wanakuwa na ujuzi wa kisasa wa TEHAMA. Hii inaonesha jinsi nchi ya Urusi inavyotilia mkazo matumizi ya TEHAMA kwa lengo la kuimarisha sekta ya

elimu na kuandaa wataalamu wenye uwezo wa kushiriki kikamilifu katika maendeleo ya kiteknolojia nchini humo.

Kwa upande wa Uchina, Makaun (1990) anasema kwamba, juhudi kubwa zimefanywa nchini Uchina kuboresha sekta ya elimu kupitia TEHAMA. Serikali ya Uchina imeanzisha mipango muhimu kama vile: Mpango wa Tano wa Matumizi ya TEHAMA katika Elimu na Mpango wa Hatua za Kuinua Elimu katika Karne ya 21 (Zeng, 2022). Mipango hii imeanzishwa nchini humo kwa lengo la kuimarisha matumizi ya teknolojia katika mfumo wa elimu (Zeng, khj).

Hizi ni hatua zinazodhihirisha dhamira ya serikali ya Uchina katika kutilia mkazo TEHAMA kwa lengo la kuongeza ubora na ufanisi wa elimu nchini. Mipango hii inaonesha jinsi TEHAMA inavyochukuliwa kama zana muhimu ya kuboresha mazingira ya kujifunza na kukuza maendeleo ya elimu kwa kizazi cha sasa na kijacho.

Zaidi ya hayo, Kenya imeonesha msimamo wake muhimu katika kukuza matumizi ya TEHAMA katika mfumo wa elimu. Kwa mujibu wa Fellenz & Brady (2007), serikali ya Kenya iligundua umuhimu wa TEHAMA katika elimu na hivyo ikaanza kuwekeza katika miradi inayolenga kusambaza kompyuta na kutoa mafunzo kwa walimu katika shule za sekondari. Kama inavyoelezwa na Fellenz & Brady (whj), kuanzishwa kwa mradi wa kusisitizia ujumuishaji wa TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji kwa ngazi zote za elimu ni hatua kubwa inayodhihirisha utashi wa serikali ya Kenya katika kuendeleza elimu kwa kupitia matumizi ya TEHAMA. Kwa hiyo, matokeo chanya yaliyoonekana katika ufundishaji na ujifunzaji katika shule tofauti nchini Kenya yanathibitisha mchango wa TEHAMA katika kuboresha mfumo wa elimu nchini humo. Wazo hili linathibitisha mchango wa TEHAMA katika uboreshaji wa shughuli za ufundishaji na ujifunzaji.

Hatimaye, serikali ya Rwanda imeonesha dhamira ya kuendeleza nchi kwa kutilia mkazo ujumuishaji wa TEHAMA katika shughuli mbalimbali. Kulingana na Mukama & Andersson (2008. Mwelekeo huu unajikita katika maendeleo katika nyanja tofauti kama file afya, uchumi, elimu na nyinginezo. Mbodila, Jones na Muhandji (2013) wanaongezea kwamba nchini Rwanda, kumekuwa na msisitizo mkubwa wa ujumuishaji wa TEHAMA katika mfumo wa elimu, lengo likiwa ni kufanya Rwanda iwe nchi inayoelekea maendeleo yanayotegemea maarifa. Hii inathibitisha jinsi TEHAMA inavyochukuliwa kama njia muhimu ya kuboresha elimu na

kusaidia katika kufanikisha malengo ya maendeleo ya kitaifa nchini Rwanda. Hii ndio sababu tuliamua kufanya utafiti wetu ili tuchunguze namna TEHAMA ina nafasi chanya katika ufundishaji wa fasihi andishi ya Kiswahili kwa shule teule za sekondari wilayani Nyagatare nchini Rwanda.

Hata hivyo, licha ya kuona kwamba TEHAMA imejumuishwa katika elimu ili kufanikisha malengo ya ujifunzaji na ufundishajii kwa ajili ya maendeleo endelevu ya nchi tofauti, bado kuna tafiti ambazo zinaonesha kwamba ufundishaji wa fasihi ungali unakabiliwa na changamoto kadhaa (Tayib & Hassan, 2020). Mojawapo ya changamoto hizo ni ukosefu wa zana za kufundishia na kujifunzia, utumiaji wa mbinu za ufundishaji ambazo hazina ufanisi. Kwa mfano, kutumia mbinu za kizamani mfano wa mbinu hizo ni kama mbinu ya Kumbukumbu, mbinu ya Maelekezo mbinuya Vitbu vya mwanafunzi na mbinu ya Mwalimu kwa mwanafunzi, zinazotegemea mihadhara badala ya mbinu shirikishi na za dijitali zinazoweza kuhamasisha wanafunzi kushiriki kikamilifu. Changamoto nyingine ni mtazamo wa wanafunzi kuhusu somo la fasihi. Kama inavyoelezwa na Gomez (2022), wanafunzi wanaichukulia fasihi kama somo gumu, hali ambayo inaweza kuathiri ufanisi wao wa kujifunza na kufikia malengo ya somo hilo.

Kwa hiyo, ili kuepukana na changamoto zinazokabili ufundishaji wa fasihi, Courville (2011) & Osario (2017) wanaonesha kuwa matumizi ya TEHAMA yanaweza kusaidia kukabiliana na changamoto zinazojitokeza katika ufundishaji wa fasihi ya Kiingereza, kutoa njia mpya na inayovutia ya kufundisha na kujifunza lugha hiyo. Alnord (2021) anaongezea kwamba, matumizi ya programu za kompyuta mfano wa Microsoft neno, chrome na zana za kidigiti kama projekta na kompuyuta yanaweza kuboresha ufundishaji wa fasihi kwa kukuza uwezo wa lugha kwa wanafunzi na kuchangia katika kujenga mazingira bora ya kufundishia na kujifunzia.

Isitoshe, Stanley (2018) anaonesha mchango wa TEHAMA katika ufundishaji wa Kiswahili kwa ujumla kwa kusema kwamba, matumizi ya TEHAMA yameongeza ushirikiano wa wanafunzi na walimu, kurahisisha upatikanaji wa nyenzo za kujifunzia, na kuboresha stadi za lugha kwa kutumia programu mbalimbali za lugha. ambazo ni kujifunza lugha mpya, kuboresha ujuzi wa lugha au kutafsiri lugha, baadhi ya program maarufu za lugha ni duolingo, babble, rosetta stone na memrise. Hii inaweza kutoa njia inayovutia na inayofaa zaidi ya kufundisha lugha hiyo na kuhimiza wanafunzi kujenga ujuzi wa Kiswahili kwa ufanisi.

Licha ya maelezo yaliyotolea, tunaona kwamba kungali na mapengo ambayo yanafaa kuzibwa. Kwanza, tafiti za hapo juu zilieleza tu dhana ya TEHAMA na fasihi bila kuonesha uhusiano uliopo kati yake. Pili, tafiti zilizofanywa na watafiti tuliowarejelea hapo juu zinaonesha namna ambavyo nchi tofauti zilijumuisha TEHAMA katika elimu tu bila kueleza Tehama na fasihi andishi ya kiswahili Tatu, tafiti zilizofanywa zinazungumzia ufundishaji wa fasihi na changamoto zinazokabili ufundishaji wa fasihi bila kugusia mbinu za utatuzi wa changamoto hizo.

Nne, licha ya tafiti zilizofanywa kuonesha mchango wa TEHAMA katika ufundishaji wa fasihi, tafiti hizi zinajihusisha na lugha ya Kiingereza tu na kuacha pengo kuhusu mchango wa TEHAMA kwenye ufundishaji wa fasihi andishi ya Kiswahili. Mwisho, tafiti zilizofanyika zinaonesha mchango wa TEHAMA katika ufundishaji wa Kiswahili kwa ujumla. Tafiti husika hazioneshi mchango wa TEHAMA katika ufundishaji wa Kiswahili hasa somo la fasihi andishi katika lugha hiyo. Hivyo basi, tulipata shauku ya kufanya utafiti wenye mada "Mchango wa TEHAMA katika Ufundishaji wa Fasihi Andishi katika Shule za Sekondari Wilayani Nyagatare Nchini Rwanda" kwa kusudi la kuziba mapengo hayo.

**1.3 Tamko la Tatizo la Utafiti**

Kwa mujibu wa El-Helou (2012), fasihi huwajengea wanafunzi uwezo wa kutumia lugha kwa kuzingatia utamaduni, imani, mitazamo na itikadi mbalimbali. TEHAMA inaweza kutumiwa ili kukabiliana na changamoto zinazokabili ufundishaji wa fasihi (Courville, 2011; Osario, 2017 & Alnord, 2021). Hata hivyo, ufundishaji wa fasihi bado unakabiliwa na changamoto tofauti (Tayib & Hassan, 2020). Gomez (2022) anasema kuwa wanafunzi wanaichukulia fasihi andishi kama kozi ngumu na jambo hili huwazuia kupata uwezo wa kutumia lugha lengwa kutegemeana na muktadha.

Hivyo basi, hali hii ilituchochea kufanya utafiti wetu ili tuchunguze mchango wa TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji wa fasihi andishi katika shule za sekondari wilayani Nyagatare nchini Rwanda. Isitoshe, tuliamua kufanya utafiti wetu ili kutoa mwongozo bora wa kuwasaidia walimu wa Kiswahili kufanikisha ufundishaji wa fasihi andishi kwa kutumia TEHAMA.

**1.4 Malengo ya Utafiti**

Melengo ya utafiti uliofanyika yanagawanyika katika lengo la jumla na malengo mahususi.

### 1.4.1 Lengo la Jumla

Lengo la jumla ni kuchunguza mchango wa TEHAMA katika ufundishaji wa fasihi andishi katika shule za sekondari wilayani Nyagatare nchini Rwanda.

### 1.4.2 Malengo Mahususi

i) Kubainisha mchango wa TEHAMA katika ufundishaji wa fasihi andishi katika shule za sekondari wilayani Nyagatare nchini Rwanda.

ii) Kuunda miongozo ya utumiaji wa TEHAMA ili kuleta ufanisi wa ufundishaji wa fasihi andishi katika shule za sekondari wilayani Nyagatare nchini Rwanda.

## 1.5 Maswali ya Utafiti

i) Je, TEHAMA ina mchango gani katika ufundishaji wa fasihi andishi katika shule za sekondari Wilayani Nyagatare nchini Rwanda?

ii) Je, tunaweza kuunda vipi miongozo ya utumiaji wa TEHAMA ili kuleta ufanisi wa ufundishaji wa fasihi andishi katika shule za sekondari wilayani Nyagatare nchini Rwanda?

## 1.6 Umuhimu wa Utafiti

Matokeo ya utafiti wenye anuani "Mchango wa TEHAMA katika Ufundishaji wa Fasihi Andishi katika Shule za Sekondari Wilayani Nyagatare Nchini Rwanda" yatakuwa na umuhimu mkubwa kwa wadau mbalimbali katika uga wa lugha, elimu na TEHAMA nchini Rwanda na nje ya Rwanda.

Mosi, matokeo ya utafiti yatakuwa muhimu kwa walimu wanaofundisha katika michepuo ya lugha nchini Rwanda. Matokeo husika, yataongeza maarifa ya walimmu kuhusu jinsi TEHAMA inavyoweza kuboresha ufundishaji na ujifunzaji wa fasihi andishi katika shule za sekondari nchini Rwanda. Kuelewa athari za TEHAMA katika ufundishaji wa fasihi andishi kunaweza kuchochea uundaji mbinu bora za ufundishaji na za kuvutia, na hivyo kuboresha utendaji wa kitaaluma na ujuzi wa lugha miongoni mwa wanafunzi.

Pili, matokeo haya yatasaidia katika kuboresha uzoefu wao wa kujifunza fasihi andishi kwa kutumia mbinu za kisasa za teknolojia. Wanafunzi watafaidika na mbinu zinazowezesha kuelewa na kujifunza fasihi kwa njia inayovutia zaidi, kama vile kutumia zana za multimedia, mijadala ya

mtandaoni, na mifumo ya mawasiliano ya kidijitali. Hii itawafanya wawe na hamasa zaidi katika kujifunza, kuongeza kiwango cha ushiriki wao darasani, na kuchangia kwa kiasi kikubwa katika kuimarisha uelewa wa maandiko ya fasihi kwa kina.

Tatu, matokeo ya utafiti yatakuwa muhimu kwa wabunifu wa sera za elimu nchini Rwanda. Yatatoa mwongozo katika kuboresha sera na mtaala wa elimu, hasa kwenye ufundishaji wa Kiswahili. Hii itawawezesha kubuni mbinu bora za kuingiza TEHAMA katika ufundishaji wa lugha. Matokeo haya yatasaidia kuimarisha mfumo wa elimu na kuhakikisha kuwa mtaala unalingana na mahitaji ya sasa.

Mwisho, matokeo haya yatakuwa rejea kwa tafiti zijazo kwa kuwa nchini Rwanda hakuna utafiti wa kutosha kuhusu TEHAMA na ufundishaji wa fasihi andishi, na hivyo yatafundisha watafiti wa siku zijazo kuhusu mchango wa teknolojia katika kuboresha mbinu za ufundishaji na kuongeza uelewa wa fasihi andishi katika muktadha wa Rwanda.

### 1.7 Mawanda ya Utafiti

Utafiti ulikuwa na mawanda tofauti kama yanavyoelezwa hapa chini:

#### 1.7.1 Mawanda ya Kimaudhui

Kimaudhui, utafiti ulijikita katikamchango wa TEHAMA katika ufundishaji wa fasihi andishi katika shule za sekondari wilayani Nyagatare nchini Rwanda. TEHAMA inaweza kuwa muhimu katika ufundishaji wa masomo tofauti na utendekaji wa mambo kadhaa. Ingawaje TEHAMA inaweza kutumika mahali tofauti, katika utafiti uliofanyika, tulijikita katika mchango wa TEHAMA na namna inavyoweza kutumiwa katika ufundishaji wa fasihi andishi hasa katika shule za sekondari wilayani Nyagatare nchini Rwanda

#### 1.7.2 Mawanda ya Kijiografia

Kijiografia, utafiti ulifanyika katika shule za sekondari wilayani Nyagatare nchini Rwanda. Nyagatare ni wilaya ambayo inapatikana katika Mkoa wa Mashariki. Wilaya hii ina tarafa 14: Gatunda, Kiyombe, Karama, Karangazi, Katabagemu, Matimba, Mimuli, Mukama, Musheli, Nyagatare, Rukomo, Rwempasha, Rwimiyaga na Tabagwe. Ijapokuwa wilaya husika ina tarafa 14, utafiti wetu ulifanyika katika tarafa 4 tu ambazo ni Kiyombe, Mukama, Mimuli na Nyagatare. Tarafa hizi nne zilichaguliwa kwa kuwa ndizo zenye shule ambazo zina maabara za kompyuta, kupitia mradi wa serikali wa "Kompyuta Moja kwa Kila Mwanafunzi." Tulichagua

tarafa hizi tukitumaini kwamba zitaruhusu uchunguzi wa kina wa mchango wa TEHAMA katika ufundishaji wa fasihi andishi ya Kiswahili katika mazingira yaliyo na rasilimali za teknolojia zilizowekwa vizuri.

Kwa hiyo, utafiti wetu ulifanyika katika shule za sekondari zifuatazo: G.S. Cyabayaga (Tarafa ya Mimuli), G.S Nyagatare (Tarafa ya Nyagatare), G.S Gishororo (Tarafa ya Mukama), G.S Kabale II (Tarafa ya Kiyombe) na G.S Bufunda (Tarafa ya Mukama). Kwa kuwa shule husika zina mchepuo wa LFK, tulitarajia kwamba huenda tukapata taarifa zilizo hitajika.

### 1.7.2 Mawanda ya Kimuda

Utafiti uliofanyika ulikusudia kuchunguza mchango wa TEHAMA katika ufundishaji wa fasihi katika shule za sekondari wilayani Nyagatare nchini Rwanda. Kimuda, utafiti huo ulijishughulisha na kipindi cha wakati cha miaka kati ya 2023 na 2024.

Kipindi hiki kilichaguliwa kwa kuwa ndicho kipindi cha karibu ambacho kinatawaliwa na maendeleo makubwa katika sekta ya teknolojia. Aidha, tulichagua miaka hii tukifikiri kwamba itaruhusu kukusanya data za kutosha kuhusu mchango waTEHAMA na katika ufundishaji wa fasihi andishi kwenye shule za sekondari teule wilayani Nyagatare.

## 1.8 Vikwazo vya Utafiti na Utatuzi Wake

Utafiti ulikabiliwa na vikwazo tofauti. Aya zinazofuata zinafafanua vikwazo hivyo na namna vilivyotatuliwa. Kwanza, utafiti wetu ulifanyika katika shule ambazo hazikakaribiani. Hali hii ilikuwa kikwazo kwa kuwa kufikia kila shule kulihitaji uwezo wa kifedha. Ili kuepukana na kikwazo hiki, mtafiti alipanga mapema bajeti ya kwenda katika ukusanyaji data. Aidha, palipowezekana, ukusanyaji data katika shule zinazokaribiana ulifanyika siku moja.

Pili, kutokana na kwamba ujumuishaji wa TEHAMA ni jambo ambalo limepewa kipaumbele katika sekta ya elimu nchini Rwanda, kuna walimu na wakurugenzi ambao walitoa taarifa ambazo si za ukweli kwa lengo la kuonesha kuwa TEHAMA inatumiwa kwa ufasaha shuleni kwao. Jambo hili lilithibitishwa na kwamba waliyoyasema, yalitofautiana na yaliyosemwa na washiriki wa utafiti wengine kutoka kwenye shule moja. Ili kuepukana na kikwazo hiki, taarifa kutoka kwa wakurugenzi, wakuu wa masomo na walimu zilikusanywa na kulinganishwa kwa

ajili ya kupata uamuzi wa kijumla. Vilevile, mtafiti alifanya ushuhudiaji ili kuhakikisha ukweli wa taarifa zilizotolewa na washiriki wa utafiti.

Tatu, kuna washiriki wa utafiti ambao walikataa kushiriki katika utafiti kwa kudhani kwamba mtafiti anafanya upelelezi ambao unaweza kuwadhuru. Ili kuepukana na kikwazo hiki, mtafiti aliwaelezea washiriki wa utafiti malengo ya utafiti. Vilevile, mtafiti aliwaonesha kibali kutoka katika wilaya ambacho kinamruhusu kukusanya data. Isitoshe, mtafiti aliwahakikishia washiriki hao kwamba taarifa watakazozitoa zitatunzwa kisiri na hazitatumiwa kwa lengo jingine zaidi ya utafiti uliofanyika.

Mwisho, wakati wa usaili, kulizuka tatizo la lugha hasa wakati mtafiti alipokuwa anafanya mahojiano na wakuu wa masomo na wakurugenzi ambao hawajui Kiswahili. Ili kutatua kikwazo hiki, mtafiti alitafsiri maswali ya mahojiano katika lugha ya Kiingereza.

## 1.9 Mpangilio wa Ripoti ya Utafiti

Tasnifu hii inagawanyika katika sura tano. Sura ya kwanza inajihusisha na taarifa tangulizi kuhusu utafiti. Aidha, sura ya pili inajihusisha na mapitio ya maandiko na kiunzi cha nadharia. Zaidi ya hayo, sura ya tatu inajadili methodolojia ya utafiti. Isitoshe, sura ya nne inahusika na uchambuzi, mjadala na uwasilishaji wa matokeo ya utafiti. Sura ya mwisho ambayo ni ya tano ni muhtasari, hitimisho na mapendekezo ya utafiti.

## 1.10 Muhtasari wa Sura ya Kwanza

Sura ya kwanza imelenga kutoa taarifa za msingi kuhusu utafiti. Kwa hiyo, sehemu zinazojenga sura ya kwanza ni: utangulizi, usuli wa tatizo la utafiti, tamko la tatizo la utafiti, malengo ya utafiti, maswali ya utafiti, umuhimu wa utafiti, mawanda ya utafiti, vikwazo vya utafiti, mpangilio wa utafiti na muhtasari.

# SURA YA PILI: MAPITIO YA MAANDIKO

## 2.1 Utangulizi

Sura ya pili inahusu mapitio ya maandiko na kiunzi cha nadharia. Pamoja na hayo, sura hii inagawanyika katika sehemu tisa: utangulizi, ufundishaji na ujifunzaji wa fasihi, ujumuishaji wa TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji wa lugha, mchango wa TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji wa lugha, mchango wa TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji wa fasihi, miongozo ya utumiaji wa TEHAMA katika ufundishaji wa fasihi. Aidha, sehemu hii inahusika na mapengo ya tafiti tangulizi na nadharia iliyoongoza utafiti wetu. Sehemu ya mwisho ni muhtasari wa sura ya pili.

## 2.2 Mbinu za Ufundishaji na Ujifunzaji wa Fasihi

Utafiti wetu ulikusudia kuchunguza mchango wa TEHAMA katika ufundishaji wa fasihi andishi katika shule za sekondari wilayani Nyagatare nchini Rwanda. Kwa hiyo, ilikuwa bora kupitia maandiko kuhusu ufundishaji wa fasihi ili kufahamu namna ufundishaji na ujifunzaji wa fasihi unavyofanyika na changamoto zake. Hivyo basi, sehemu hii inagawanyika katika sehemu mbili. Sehemu hizo ni namna ufundishaji na ujifunzaji wa fasihi unavyofanyika na changamoto za ufundishaji na ujifunzaji wa fasihi.

### 2.2.1 Namna Ufundishaji na Ujifunzaji wa Fasihi Unavyofanyika

Ufundishaji wa fasihi ni mchakato wa kuelezea na kuchambua vitabu vya fasihi na hadithi za kifasihi (Daskalovska & Dimova, 2012). Ufundishaji wa fasihi unaweza kufanywa katika mazingira mbalimbali kama vile darasani, redioni au kwa kutumia mwongozo wa uhakiki ulioundwa na wataalamu wa fasihi. Katika mchakato wa kufundisha fasihi, walimu wanatarajia wanafunzi kuelewa na kukumbuka yaliyofundishwa, labda kwa ajili ya ufanisi katika mitihani (Daskalovska & Dimova, whj).

Hivyo, ufundishaji wa fasihi unajumuisha kuelewa dhana na lengo la fasihi, kutofautisha kati ya fasihi simulizi na fasihi andishi na kufikiria kuhusu muktadha wa kazi za fasihi. Hii ina maana kwamba, ufundishaji wa fasihi ni njia muhimu ya kuwawezesha wanafunzi kugundua na kufurahia utajiri wa fasihi kwa ujumla. Kwa hiyo, sehemu hii inaangazia kuonesha namana ambavyo ufundishaji wa fasihi hufanyika.

#### 2.2.1.1 Ufundishaji wa Fasihi kwa Mbinu ya Kusoma kwa Sauti na Masimulizi

Mbinu ya kusoma kwa sauti na masimulizi ni njia ya jadi iliyokuwa ikitumika kwa muda mrefu katika ufundishaji wa fasihi. Chacha (2016) akimrejelea Chamber (1980), anasema kuwa kusoma kwa sauti na kusimulia hadithi ni mbinu mbili ambazo zinaweza kuchochea hamu ya wanafunzi kujifunza fasihi na kukuza mapenzi yao ya kusoma. Kwa kusoma kwa sauti, mwalimu au mwanafunzi anaweza kutoa maelezo ya kina na kusisimua yanayowafanya wanafunzi kuelewa na kuona umuhimu wa kazi za fasihi.

Aidha, Karantalis & Koukopoulos (2022) wanabainisha kuwa masimulizi ni njia nyingine inayoweza kutumika katika ufundishaji wa fasihi. Kupitia njia hii, mwalimu anaweza kusimulia hadithi kwa wanafunzi au kuwapa nafasi wanafunzi kusimulia hadithi kwa wenzao. Hii inaweza kuchangia kujenga uhusiano wa karibu zaidi kati ya wanafunzi na maudhui ya fasihi wanayojifunza (Karantalis & Koukopoulos, whj). Hii inamaanisha kwamba masimulizi yanaweza kuchochea ubunifu wa wanafunzi na kuwapa uwezo wa kufikiri kwa kina.

Kwa mujibu wa Njogu na Chimera (1999), mbinu ya kusoma kwa sauti na masimulizi inaweza kutumiwa na walimu wa fasihi kwa kuwa ni njia nafuu ukilinganisha na mbinu nyingine za ufundishaji wa fasihi. Hii ni kwa sababu haichukui gharama kubwa kutekelezwa na inaweza kufanyika bila kutumia vifaa vya kisasa ambavyo ni ghali. Hii huifanya kuwa rahisi kwa walimu kuitumia ili kuwapa wanafunzi maudhui kadhaa ya fasihi bila ya kupata vikwazo vya kifedha. Ingawa mbinu hii imeoneshwa kama njia nafuu katika ufundishaji wa fasihi, haiendani na mtaala unaoegemea katika uwezo ambao unatekelezwa nchini Rwanda.

Urahisi wa utekelezaji wa mbinu hii ni faida nyingine ambayo inawasukuma baadhi ya walimu kutumia (Chacha, khj). Mbinu ya kusoma kwa sauti na masimulizi inaweza kutumiwa na walimu bila kuhitaji ujuzi wa hali ya juu. Hii huifanya mbinu hii kuwa ya kuvutia kwa walimu wapya au wale ambao wanaweza kukutana na changamoto katika kutumia teknolojia au mbinu za kisasa za ufundishaji.

Hivyo, kwa kuzingatia gharama na urahisi wa utekelezaji, mbinu ya kusoma kwa sauti na masimulizi inaweza kuwa chaguo bora katika kufundisha fasihi. Kwa hiyo, maelezo ya Chacha

(khj), Karantalis & Koukopoulos (whj) na Njogu Chimera (whj), mbinu ya kusoma kwa sauti na masimulizi ina fanikisha ufundishaji wa fasihi kwa kuwa ni nafuu na ni rahisi kutekeleza.

Licha ya kwamba mbinu ya kusoma kwa sauti na masimulizi inaweza kuonekana kuwa bora na nafuu katika ufundishaji wa fasihi, mbinu husika inaweza kukabiliwa na changamoto katika muktadha wa mtaala unaoegemea katika uwezo unaotekelezwa nchini Rwanda. Mtaala huu unazingatia zaidi mbinu zinazotumia teknolojia au mbinu za kisasa za ufundishaji (Rwabizambuga, 2018). Mbinu hizi ni tofauti na mbinu za jadi kama kusoma kwa sauti na masimulizi tu. Hii inaweza kuathiri jinsi mbinu hii inavyopokelewa na kutekelezwa katika mazingira ya elimu ya Rwanda, kwa kuwa haijumuishi vipengele muhimu vya mtaala au haiwezi kufikia malengo yaliyowekwa na mamlaka husika. Hivyo basi, hali hii ilitusababisha kufanya utafiti wetu ili kuunda muongozo wa kutumia TEHAMA katiaka ufundishaji wa fasihi andishi ya Kiswahili katika shule za sekondari wilayani Nyagatare nchini Rwanda.

#### 2.2.1.2 Ufundishaji wa Fasihi kwa Mbinu ya Majadiliano katika Makundi

Mbinu ya majadiliano katika makundi ni mbinu nyingine ambayo inatumiwa na walimu katika ufundishaji wa fasihi andishi. Hii ni mbinu inayowahusisha wanafunzi katika mchakato wa kujifunza kupitia mijadala inayohusu kazi za fasihi (Chacha, khj). Katika mbinu hii, mwalimu huchagua waschana na wavulana kwa usawa, kulingana na idadi ya wanafunzi wote, na wanafunzi hupangwa katika makundi na kushiriki katika majadiliano kuhusu maudhui, mbinu za uandishi na muktadha wa kazi za fasihi wanazosoma. Mijadala hii inawawezesha wanafunzi kutoa maoni yao, kubadilishana mawazo na kukuza ufahamu wao wa mambo mbalimbali ya fasihi.

Aidha, Chacha (khj) anaendelea kusema kwamba, mbinu ya majadiliano katika makundi ina mchango mkubwa katika kukuza uwezo wa wanafunzi katika tanzu mbalimbali za fasihi. Wanafunzi wanaposhiriki katika majadiliano, wanachangia maoni yao, wanajiuliza maswali na wanachambua kwa kina mada za fasihi. Hii inasaidia kuimarisha uwezo wao wa kuelewa na kufafanua dhana za fasihi pamoja na kuendeleza ujuzi wa kiutunzi na kiuhakiki.

Kwa kuongezea, Hambur (2018) anasema kwamba mbinu ya majadiliano katika makundi inajenga mazingira ya ushirikiano na ushiriki wa wanafunzi wote katika mchakato wa

ufundishaji na ujifunzaji. Kila mwanafunzi katika kikundi anaweza kuwa na majukumu fulani ili kukamilisha kazi. Baadhi ya majukumu hayo ni, kuwa kiongozi wa majadiliano, mwandishi wa muhtasari au mwakilishi ripoti. Hibyo basi, wanafunzi wanaajibika na kushirikiana kati yao ili kutimiza kazi ya fasihi wanayopewa.

Zaidi ya hayo, Chacha (khj) anasema kuwa, mbinu ya majadiliano katika makundi inaruhusu walimu kufundisha mada za kifasihi tofauti kwa muda mfupi, huku kila kikundi kikijadili mada inayohusiana na mada mahususi ya fasihi. Hii inatoa fursa ya kuleta tofauti za muktadha, mitindo ya uandishi na maudhui. Kupitia matumizi ya mbinu husika, mwalimu anaweza kuchochea majadiliano yanayozingatia tanzu mbalimbali za fasihi, kuwawezesha wanafunzi kuchambua tofauti za kimuktadha na kimaudhui katika kazi za fasihi (Chacha, khj). Hii ina maana kwamba, mbinu hii huleta utofauti katika mchakato wa kujifunza na kuimarisha ufahamu wa wanafunzi kuhusu kazi za fasihi.

Isitoshe, mbinu ya majadiliano katika makundi pia ni chombo kinachowezesha mwalimu kufundisha matini za kifasihi tofauti wakati mmoja (Chacha, khj). Kupitia matumizi ya mbinu husika, wanafunzi wanaweza kujadili kazi tofauti kama vile riwaya, tamthilia au shairi, kuwezesha kulinganisha na kuchanganua muktadha, mbinu za uandishi, na maudhui. Hivyo, mbinu hii inaleta ufanisi kwa kutoa ufahamu wa kina na upana kuhusu fasihi kwa wanafunzi.

Kwa hiyo, kutokana na maelezo ya hapo juu, mbinu ya majadiliano katika makundi inahusisha wanafunzi katika mijadala kuhusu kazi za fasihi, ikichochea ufahamu wao na uwezo wa kiutunzi na kiuhakiki. Aidha, mbinu hii inawaruhusu walimu kufundisha mada tofauti za kifasihi wakati mmoja. Licha ya maelezo hayo, bado watafiti hawajaonesha namana ambavyo ufundishaji wa fasihi kwa mbinu ya majadiliano katika makundi inaweza kutekelezwa hasa katika enzi hizi ambazo ni za kidijiti. Hivyo basi, tulipata shauku ya kufanya utafiti wetu ili tubainishe namna ufundishaji wa fasihi kwa mbinu ya majadiliano katika makundi inavyoweza kutekelezwa kupitia matumizi ya TEHAMA.

#### 2.2.1.3 Ufundishaji wa Fasihi kwa Mbinu ya Ziara za Masomo

Ufundishaji wa fasihi kwa mbinu ya ziara za masomo ni njia inayojumuisha wanafunzi katika uzoefu wa moja kwa moja na muktadha wa lugha inayozungumzwa mitaani (Rodrigues & Ravasco, 2020). Mbinu hii ni muhimu katika kujenga uhusiano wa karibu kati ya nadharia ya

fasihi na vitendo vya lugha. Ziara za masomo zinaweza kutoa fursa ya kuleta muktadha wa shule karibu na mazingira halisi ya lugha, kuchochea ugunduzi na uelewa wa wanafunzi kuhusu fasihi na jamii inayowazunguka. Unaweza kufundisha riwaya kupitia ufundishaji wa masomo kwa kutumia mbinu shirikishi zinazochanganya majadiliano, uchambuzi, na mazoezi ya vitendo. Mwalimu anaweza kugawa riwaya katika sura au sehemu, na wanafunzi wanajadiliana kuhusu wahusika, dhamira, na mtindo wa mwandishi. Pia, mwalimu anaweza kutumia vitabu vya kiada, video, na mahojiano na waandishi ili kuelezea dhana za fasihi. Mazoezi ya kufupisha au kuandika insha juu ya masuala yaliyopo kwenye riwaya husaidia wanafunzi kuelewa kwa undani zaidi.

Kwa mfano, wanafunzi wanaweza kufanya ziara ya masomo katika maeneo kama vile makumbusho ya fasihi, maktaba zenye hazina ya maandiko ya kihistoria, au maeneo yenye umuhimu wa kihistoria na kitamaduni vinavyohusiana na maandiko wanayoyasoma. Ziara hizi zinaweza kujumuisha mada kadhaa na kuchunguza sehemu tofauti za mtaala, hivyo kuchangia katika kuwawezesha wanafunzi kuona ukweli wa fasihi na kuhusisha nadharia na vitendo kwa njia inayofaa na inayovutia (Rodrigues & Ravasco, 2020). Hivyo, mbinu hii inatoa njia ya kipekee ya kukuza uelewa wa kina wa fasihi kwa wanafunzi kwa kuunganisha maarifa ya nadharia na uzoefu halisi wa maisha. Kupitia TEHAMA Mwalimu anaweza kufundisha Riwaya kwa kutumiaProjekta, kwa kutumia projekta wanafunzi wanaweza kusoma maandishi Pamoja wakaelewa zaidi na wakafurahia maandishi hayo.

Aidha, ziara za masomo zinaleta fursa kubwa za kielimu, kwani malengo yake yanazidi yale yanayoweza kufikiwa darasani (Rodrigues & Ravasco, whj). Kufundisha ndani ya darasa na kuunganisha na ziara za masomo kunawezesha aina ya kujifunza yenye msisimko na kina, ikiruhusu wanafunzi kuchanganya utamaduni mpana na uzoefu wa kujifunza kwa undaniKutokana na Rodrigues & Ravasco (whj), ziara za masomo hutoa fursa za kujifunza kujua na kufaidika na uzoefu wa kujifunza maisha yote.

Ziara hizi zinaweza kutokea mahali popote zikiwa na lengo kuchochea ugunduzi na kuongeza maarifa kwa njia inayojumuisha furaha na michezo. Hii ina maana kwamba ziara za masomo ni bora katika ufundishaji wa fasihi kwa kuwa huweza kuwamotisha wanafunzi kwa kutoa mazingira fasaha ya kujifunzia.

Isitoshe, Rodrigues & Ravasco (whj), wanasema kuwa, ziara za masomo zinasaidia kuimarisha mahusiano ya wanafunzi na wasemaji wa asili wa maeneo wanayotembelea. Kujua lugha ya pili, pamoja na desturi na sheria za maisha, huwapa wanafunzi ujuzi wa kujivunia na kuwa watumiaji wa lugha wenye ufanisi wakiwa wanatunga au wakizichambua kazi za fasihi.

Kupata ufahamu wa kina wa utamaduni wa nchi husika kunawezesha wanafunzi wa fasihi kuelewa na kuheshimu wenzao, kujenga uhusiano wenye maelewano na kufanikisha mahusiano mapya ya kibinafsi na watu kutoka tamaduni tofauti. Hivyo, ziara za masomo ni njia muhimu ya kukuza uelewa na uhusiano wa kimataifa kati ya wanafunzi wa fasihi.

Kwa ufupi, matumizi ya ziara za masomo kama njia ya kufundisha fasihi yanatoa fursa ya kipekee kwa wanafunzi kujifunza kwa vitendo na kupunguza pengo kati ya nadharia za fasihi na matumizi halisi ya lugha. Licha ya maelezo haya kutolewa, bado tunafikiri kuwa kuna mapengo kwa kuwa watafiti waliotangulia wametilia mkazo kwenye matumizi ya ziara za masomo na ufundishaji wa fasihi kwa ujumla huku ufundishaji wa fasihi andishi ukiachwa nyuma.

Pengine, watafiti waliotangulia hawakuonesha namna ambavyo utumiaji wa ziara za masomo unaweza kutekelezwa katika ufundisaji wa fasihi andishi hasa kwenye shule ambazo hazina uwezo wa kiuchumi wa hali ya juu. Vilevile, tafiti zilizofanywa hazikuonesha namna ambavyo ziara za masomo zinaweza kutumiwa katika ufundishaji wa fasihi andishi kwa wanafunzi wanaojifunza Kiswahili kwenye nchi ambamo Kiswahili hufundishwa kama lugha ya pili. Hivyo basi, hali hiyo ilituchochea kufanya utafiti wetu kwa kusudi la kuchunguza ikiwa ziara za masomo ni mojawapo ya mbinu mwafaka zinazoweza kutumiwa katika ufundishaji wa fasihi andishi kwa wanafunzi wa shule za sekondari wilayani Nyagatare nchini Rwanda.

### 2.2.2 Changamoto za Ufundishaji na Ujifunzaji wa Fasihi

Sehemu inahusisha mapitio ya maandiko kuhusu changamoto zinazoweza kukabili ufundishaji na ujifunzaji wa fasihi kwa ujumla.

#### 2.2.2.1 Utumiaji wa Mbinu za Kijadi

Mwalimu wa fasihi ana mchango muhimu katika kumotisha wanafunzi kupenda lugha na utamaduni wao (Amin & Raba, 2017). Hata hivyo, kuna changamoto nyingi zinazokabili ufundishaji na ujifunzaji wa fasihi, hasa pale mbinu za kijadi zinapopewa kipaumbele (Tayib &

Hassan, 2020). Mosi, baadhi ya walimu wanatumia mbinu za ufundishaji ambazo haziendani na mahitaji ya enzi za sasa. Kwa mfano, matumizi ya mihadhara mirefu na isiyovutia inaweza kufanya wanafunzi kupoteza hamu ya kujifunza fasihi kwa kuwa mbinu hizi haziwashirikishi wanafunzi vya kutosha. Hii inaweza kuwa changamoto kubwa, kwani inaathiri motisha na ushiriki wa wanafunzi darasani.

Pili, Tayib & Hassan (whj) wanasema kuwa, mbinu zisizofaa za ufundishaji zinaweza kuzua vikwazo vya mafanikio katika ufundishaji na ujifunzaji wa fasihi. Kwa mfano, kutumia njia moja kwa wanafunzi wote bila kujali tofauti zao za kujifunza kunaweza kusababisha baadhi yao kushindwa kuelewa na kufurahia masomo ya fasihi.

Kwa mujibu wa Amin & Raba (whj), kwa kutozingatia ubinafsi wa kila mwanafunzi, mbinu za kijadi zinaweza kuzuia wanafunzi kuelewa ukweli wa maudhui wanayosoma. Hii inaweza kusababisha upungufu wa matokeo bora na ustadi wa kusoma na kuandika, ambao ni malengo muhimu katika kujenga msingi imara wa fasihi.

Tatu, mbinu zisizofaa huchangia kutoleta furaha na motisha kwa wanafunzi wanapojifunza masomo ya fasihi (Tayib & Hassan, whj). Kwa mfano, mbinu za kijadi zinazojikita zaidi katika kusoma na kueleza maelezo badala ya kuhamasisha ubunifu na mawazo mapya zinaweza kufanya masomo kuwa magumu na yasiyovutia. Wanafunzi wanapokosa furaha katika kujifunza, wanaweza kujenga hisia hasi kuelekea masomo ya fasihi, na hivyo kupunguza ufanisi wao wa kujifunza.

Maelezo haya yanaonesha kuwa, mbinu za kijadi katika ufundishaji wa fasihi ni changamoto kwa kuwa zinaweza kuzuia ushiriki wa wanafunzi, kutokidhi mahitaji ya enzi za sasa na kupunguza mafanikio ya masomo ya fasihi. Licha ya maelezo haya kutolewa, watafiti wa hapo juu walionesha namna ambavyo utumiaji wa mbinu za kijadi unavyoathiri ufundishaji wa fasihi katika Kiingereza.

Aidha, watafiti waliotangulia walinogewa na kubainisha namna ambavyo matumizi ya mbinu za kijadi huzuia ufundishaji wa fasihi, wakasahau kubainisha namna ya kuepukana na changamoto hii.

Kwa hiyo, utafiti uliofanyika ulikusudia kuchunguza ikiwa utumiaji wa mbinu za kijadi ni mojawapo wa changamoto zinazokabili ufundishaji wa fasihi andishi kwa wanafunzi wa shule za sekondari wilayani Nyagatare. Pia, utafiti uliofanyika ulikusudia kuonesha namna ambavyo fasihi inaweza kufundishwa kwa ufasaha kwa kutumia TEHAMA kwa wanafunzi wanaojifunza Kiswahili katikashule za sekondari wilayani Nyagatare nchini Rwanda.

**2.2.2.2 Hofu ya Wanafunzi kuhusu Somo la Fasihi**

Changamoto nyingine ya ufundishaji na ujifunzaji wa fasihi ni hofu ya wanafunzi kuhusu somo hilo. Wanafunzi wengi huonesha hofu ya kusoma fasihi ikilinganishwa na masomo mengine ya lugha (Gomez, 2022). Kwanza, hofu hii inaweza kusababishwa na mtazamo wa baadhi ya wanafunzi kwamba fasihi inaweza kuwa ngumu au isiyo na maana kwao. Kwa kuongezea, uwepo wa maneno magumu na muundo wa fasihi unaweza kuwa na athari hasi kwa motisha ya wanafunzi.

Pili, hofu ya wanafunzi kuhusu somo la fasihi inaweza kuwa na athari mbaya kwa ufundishaji na ujifunzaji. Kutokana na Karakaya & Kahraman (2013), wanafunzi wanaoogopa somo la fasihi wanaweza kuwa na upinzani wa kujifunza na kushiriki katika majadiliano na hivyo kushindwa kufaidika ipasavyo kutokana na mchakato wa kujifunza. Kwa hiyo, uzoefu hasi wa wanafunzi kuelekea somo la fasihi unaweza kusababisha kutokujiamini kwao na kupunguza hamu yao ya kushiriki kikamilifu katika masomo ya fasihi.

Tatu, hofu ya wanafunzi kuhusu somo la fasihi inaweza kuwa chanzo cha kutotumika kwa muda wa kutosha katika kujifunza. Kwa mujibu wa Gomez (khj), wanafunzi wanaohisi hofu wanaweza kuwa na mwelekeo wa kuepuka kusoma kwa bidii. Pengine, wanafunzi kama hawa, wanaweza kuchukua muda mwingi katika masomo mengine wanayohisi kuwa rahisi au yenye manufaa zaidi kwao. Hii inaweza kuathiri sio tu matokeo yao ya kujifunza fasihi bali pia maendeleo yao kwa ujumla.

Hatimaye, hofu ya wanafunzi inaweza kuwafanya wachague kutohudhuria somo la fasihi kabisa. Wanafunzi wenye hofu kubwa wanapokutana na somo hilo wanaweza kuwa na mwelekeo wa kutohudhuria madarasani. Jambo hili huwasababisha wanafunzi kupoteza fursa za kujifunza na kushiriki katika mazungumzo na maelekezo muhimu kutoka kwa walimu wao (Karakaya &

Kahraman, whj). Hii inamaanisha kuwa wanafunzi ambao wana hofu kuhusu somo la fasihi hawawezi kushiriki kikamilifu katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo husika.

Kwa ufupi, tafiti za hapo juu zinaoesha kwamba, hofu ya wanafunzi kuhusu somo la fasihi inaweza kuwa kikwazo kwa wanafunzi. Tafiti hizi, zinaonesha kuwa hofu ya wanafunzi kuhusu somo la fasihi inazuia wanafunzi kujenga ujasiri na kujihusisha kikamilifu na mchakato wa kujifunza fasihi. Licha ya maelezo haya kutolewa, bado tafiti za hapo juu zingali na mapengo.

Pengo la kwanza ni kuwa, watafiti hawa hawajabainisha lugha mahususi ambapo hofu ya wanafunzi kuhusu fasihi huzuia ufundishaji wa somo hilo. Zaidi ya hayo, hata kama watafiti wa wametoa maelezo muhimu, bado tafiti zao hazijaonesha namna ya kuepuka na changamoto za hofu ya wanafunzi kuhusu somo la fasihi. Hivyo basi, tulipata shauku ya kufanya utafiti wetu ili kuyaziba mapengo ya tafiti zilizofanywa kwa kuonesha mchango wa TEHAMA katika kuepukana na hofu ya wanafunzi kuhusu somo la fasihi andishi katika shule za sekondarui wilayani Nyagatare.

**2.2.2.3 Ukosefu wa Walimu wa Fasihi wenye Uwezo**

Ukosefu wa walimu wenye uwezo ni changamoto nyingine inayozuia ufundishaji wa fasihi. Kwa mujibu wa Işıklı & Tarakçıoğlu, (2017), ufanisi wa ufundishaji wa fasihi unahitaji walimu wenye ujuzi na uelewa wa kina kuhusu mbinu bora za kufundisha fasihi na jinsi ya kuhamasisha wanafunzi kujifunza. Hata hivyo, tatizo kubwa ni kwamba idadi ya walimu wenye uwezo wa kutosha wa kufundisha fasihi inaweza kuwa ni ndogo, ikilinganishwa na mahitaji ya shule na wanafunzi.

Walimu wasio na uwezo wa kutosha ni vigumu kwao kuwasaidia wanafunzi kuwa wabunifu ili waweze kuhamisha kile wamesoma shuleni (Holmqvist, 2019). Hii ina maana kwamba, walimu hawa, hawawezi kutosheleza mahitaji ya wanafunzi kwa kutojua mbinu bora zinazoweza kuwashirikisha wanafunzi kusoma na kuelewa maudhui ya fasihi. Hii inaweza kuwa na athari mbaya kwa motisha na maendeleo ya wanafunzi katika somo la fasihi.

Kadhalika, walimu wasio na uwezo wa kutosha wanaweza kushindwa kuendana na mabadiliko ya kisasa katika mbinu za ufundishaji na teknolojia. Wanaweza kukwama katika mbinu za jadi ambazo zinaweza kuwa si rafiki kwa mazingira ya kujifunza ya wanafunzi wa leo (Holmqvist,

khj). Hii inaweza kufanya ufundishaji wa fasihi kuonekana kuwa havutii au haufai kwa wanafunzi. Hii ni kwa sababu, utumiaji wa walimu wasiokuwa na uwezo wa kutosha unaweza kusababisha ufundishaji, maandalio ya masomo na tathmini zisizofaa.

Kwa ufupi, watafiti waliotangulia wanaonesha kuwa, ukosefu wa walimu wenye uwezo ni changamoto inayosababisha upungufu wa mbinu bora za ufundishaji na kushindwa kutoa motisha ya kutosha kwa wanafunzi katika ufundishaji wa fasihi. Licha ya melezo haya muhimu bado, watafiti wa waliotangulia hawajabainisha mikakati ya kuepuka na changamoto ya ukosefu wa walimu wenye uwezo katika ufundishaji wa fasihi. Hali hii ilituchochea kufanya utafiti wetu ili kuonesha namna ambavyo matumizi ya TEHAMA yanaweza kutumiwa kuwaongezea walimu uwezo wa kufundisha fasihi andishi kwa wanafunzi wa shule za sekondari wilayani Nyagatare.

#### 2.2.2.4 Uhaba wa Zana za Kufundishia na Kujifunzia Fasihi

Fasihi ni somo linalohitaji vifaa bora na vyenye ufanisi ili kufanikisha ufundishaji na ujifunzaji wa mada zake (Kamal & Salih, 2020). Hata hivyo, Mohd & Muhmad (2023) wanasisitiza kwamba changamoto kubwa inayokabili ufundishaji wa fasihi ni uhaba wa zana za kufundishia. Zana hizi ni muhimu kwa walimu katika kuelezea na kufafanua dhana za fasihi, kutoa mifano na kuhamasisha wanafunzi kujihusisha na maudhui ya somo hilo. Uhaba huu wa zana unaweza kuathiri ufanisi wa ufundishaji na kuvuruga mchakato wa ujifunzaji kwa wanafunzi.

Kwa mujibu wa Mohd & Muhmad (whj), mojawapo ya changamoto kubwa ya inayokabili ufundishaji wa fasihi ni ukosefu wavitabu vya fasihi. Vitabu hivi ni muhimu kwa sababu vinasaidia wanafunzi kusoma, kuelewa na kutathmini maudhui ya fasihi. Kwa hiyo, uhaba wa vitabu huleta changamoto katika ufundishaji na ujifunzaji wa fasihi.

Pia, uhaba wa zana za kufundishia unaweza kuzuia walimu kutumia njia mbalimbali za ufundishaji, kama vile teknolojia na zana za kisasa (Kamal & Salih, whj). Zana hizi zinaweza kuwa na athari kubwa katika kufanya ufundishaji wa fasihi uwe wa kuvutia na tofauti na ilivyo katika mbinu za kufundishia za jadi. Hivyo, uhaba wa zana za kufundishia unaweza kupunguza ubunifu na ufanisi wa ufundishaji wa fasihi.

Kwa ufupi, maelezo ya Kamal & Salih (whj) na Mohd & Muhmad (whj) yanaonesha kwamba uhaba wa zana za kufundishia, ikiwemo vitabu na uhaba wa zana za kiteknolojia ni changamoto

kubwa inayokabili ufundishaji wa fasihi. Licha ya kutoa maelezo haya, watafiti hawa hawabainishi namna ya kuepukana na changamoto ya uhaba wa zana za kufundishia na kujifunzia fasihi. Hivyo basi, utafiti wetu ulikusudia kuchunguza hali ilivyo na kupendekeza suluhisho katika shule za sekondari wilayani Nyagatare.

**2.3Mchango wa TEHAMA katika Ufundishaji na Ujifunzaji wa Stadi za Lugha**

Ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ulikabiliwa na changamoto kadhaa zikiwemo uhaba wa walimu, ukosefu wa zana, utumiaji wa mbinu za kijadi na mtazamo hasi wa wanafunzi kuhusu fasihi. Kwa lengo la kukabiliana na changamoto hizi, wataalamu wa sekta ya elimu walipendekeza ujumuishaji wa TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji wa lugha (Ammade, Mahmud & Tahmir, 2018). Kwa hiyo, sehemu hii inajikita katika mapitio ya maandiko kuhusu ujumuishaji wa TEHAMA katika ufundishaji wa lugha kwa ujumla.

Ujumuishaji wa TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji wa lugha ni matumizi ya teknolojia ili kuboresha ufundishaji na ujifunzaji wa lugha (Hafifah, 2019). Ujumuishaji wa TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji wa lugha unajumuisha maendeleo ya njia mbalimbali za kiteknolojia na mbinu za kujifunza zinazochanganya matumizi ya teknolojia na mbinu za kawaida za ufundishaji kama vile mihadhara. Ujumuishaji huu umekuwa ukifanyiwa utafiti katika mazingira tofauti na umeonesha matokeo chanya katika mchakato wa kufundisha na kujifunza.

Kwa mujibu wa Ammade, Mahmud & Tahmir (whj), matumizi ya TEHAMA katika ufundishaji wa lugha yamesaidia kuimarisha mawasiliano, kuongeza motisha kwa wanafunzi, na kutoa fursa za ujifunzaji endelevu. Hivyo, ujumuishaji wa TEHAMA katika ufundishaji wa lugha unaonesha uwezo mkubwa wa kuboresha matokeo ya ufundishaji na ujifunzaji.

Kwa mujibu wa Ammade, Mahmud & Tahmir (whj), tafiti mbalimbali kuhusu ujumuishaji wa TEHAMA katika ufuundishaji na ujifunzaji wa lugha zilifanyika. Tafiti hizi zilishughulikia mambo mbalimbali kama vile uchukuaji, changamoto katika ujumuishaji wake katika mchakato wa kufundisha na kujifunza na aina za zana za kiteknolojia zinazotumika kwa ufundishaji na kutoa matokeo tofauti.

Kwa mfano, utafiti uliofanywa na Machmud (2011), ulibainisha kwamba ujumuishaji wa TEHAMA utekelezaji wa mtaala wa kielimu ni lazima utiliwe mkazo. Hii ni kwa sababu, TEHAMA inarahisisha ufundishaji na ujifunzaji wa lugha na hivyo kuwawezesha wanafunzi kudumisha hamasa ya kujifunza (Machmud, khj). Utafiti huu unathibitisha umuhimu wa kujumuisha TEHAMA katika mazingira ya kufundisha na kujifunza lugha ili kuboresha ufundishaji ana ujifunzaji.

Posi, utafiti uliofanywa na Cahyani na Cahyono (2013) unaunga mkono ujumuishaji wa TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji wa lugha. Watafiti hawa wameonesha kwamba ujumuishaji wa TEHAMA ni muhimu katika sekta ya elimu, kwa sababu unachangia katika kuepuka na kushinda vikwazo vinavyokabili utekelezaji wa malengo ya ufundishaji na ujifunzaji wa lugha. Utafiti huu unathibitisha umuhimu wa matumizi ya teknolojia katika kuboresha mchakato wa kufundisha na kujifunza lugha na hivyo kusaidia kuondoa vizuizi ambavyo vinaweza kutokea katika kufikia malengo ya elimu.

Pili, Jones & Cuthrell (2011) wanasisitiza kwamba matumizi ya TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji yameleta mchango mpya katika maendeleo ya kitaaluma ya walimu. Kupitia TEHAMA, walimu wanapata fursa za kupata masomo ya mtandaoni ambayo yanawasaidia kuboresha mbinu zao za ufundishaji wa lugha. Teknolojia hii inawawezesha walimu kupata rasilimali zinazobadilika kwa haraka na kuzifanya sehemu ya mchakato wao wa kujifunza na kuboresha ujuzi wao. Aidha, matumizi ya TEHAMA yanajenga uwezo wa walimu kuanzisha mazingira fasaha na ya kuvutia katika ufundishaji na ujifunzaji wa lugha, hivyo kuwahamasisha wanafunzi na kuongeza ufanisi wa mchakato mzima wa elimu.

Kutokana na maelezo ya hapo juu, ujumuishaji wa TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji wa stadi za lugha unaboresha mawasiliano na kuongeza motisha kwa wanafunzi. Matumizi ya TEHAMA pia hutoa fursa za ujifunzaji endelevu, yakionesha uwezo wa kuboresha matokeo ya ufundishaji na ujifunzaji. Licha ya maelezo haya kutolewa, tafiti za hapo juu zilijikita sana kwenye lugha ya Kiingereza ambayo si sawa na lugha ya Kiswahili. Vilevile, tafiti za hapo juu hazikuonesha taratibu zinazoweza kufuatiliwa na walimu ili kufanikisha ufundishaji na ujifunzaji wa lugha kupitia matumizi ya TEHAMA.

Mambo haya ambayo yameonekana kwenye mapitio ya maandiko yalituchochea kufanya utafiti ili kuunda miongozo ya utumiaji wa TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji wa fasihi andishi katika shule za sekondari wilayani Nyagatare nchini Rwanda. Hii ni kwasabu fasihi andishi ni sehemu kubwa ya lugha.

TEHAMA na Stadi ya Kuzungumza, Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) imebadilisha jinsi tunavyozungumza, kwa kuwezesha mawasiliano ya ana kwa ana kupitia majukwaa kama vile Zoom, Skype, na Google Meet. Mikutano ya video na simu za sauti zinawezesha watu kuwasiliana bila kujali umbali, huku pia zikitumiwa katika mafunzo ya lugha, ambapo wanafunzi wanapata fursa ya kuzungumza na walimu au watu wenyeji wa lugha kwa wakati halisi. Pia, programu za simu kama Duolingo na HelloTalk zinatoa fursa za mazoezi ya kuzungumza na wenzetu wa lugha tofauti, hivyo kuboresha ustadi huu.

TEHAMA na Stadi ya Kusoma, TEHAMA imewezesha ufikiaji wa rasilimali nyingi za kusoma kama vile vitabu vya mtandaoni (e-books), machapisho ya kielimu, na makala kutoka kwenye tovuti na majukwaa mbalimbali. Mifumo ya e-learning kama vile Moodle na Coursera inaruhusu wanafunzi kujifunza kwa kusoma nyenzo kutoka vyanzo tofauti bila kuhitaji vitabu vya kimaandishi. Pia, programu za kusoma kama Kindle hutoa vitabu katika lugha nyingi, hivyo kuimarisha uwezo wa wanafunzi kusoma kwa urahisi na kwa wakati wao wenyewe.

TEHAMA na Stadi ya Kuandika, Katika uandishi, TEHAMA imeleta mabadiliko kupitia zana za kuandika kama Microsoft Word, Google Docs, na Grammarly, ambazo husaidia kuboresha uandishi kwa kupendekeza marekebisho ya kisarufi, tahajia, na muundo wa sentensi. Majukwaa ya kijamii na blogu kama Twitter, Facebook, na WordPress yanawezesha watu kuandika na kushirikiana maoni yao na jamii kubwa zaidi, na hivyo kuboresha stadi ya kuandika kwa mazoezi ya mara kwa mara na kupata mrejesho wa papo hapo.

TEHAMA na Stadi ya Kusikiliza, TEHAMA imeimarisha uwezo wa kusikiliza kupitia zana za kidijitali kama podcast, video za YouTube, na mihadhara ya mtandaoni. Programu za lugha kama Rosetta Stone na Memrise zina nyenzo ambazo zinatumia sauti za watu wenyeji wa lugha husika, hivyo kusaidia wanafunzi kuboresha uelewa wao wa lafudhi na matamshi sahihi. Vifaa vya kusikiliza vya mtandaoni, vinavyotolewa na programu hizi, vinaimarisha uwezo wa mwanafunzi kuchambua na kuelewa lugha kwa usahihi.

## 2.4 Mchango wa TEHAMA katika Ufundishaji na Ujifunzaji wa Fasihi Andishi

Baada ya kupitia maandiko kuhusu ujumuishaji wa TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji wa lugha kwa ujumla, tuliendelea na kupitia maandiko kuhusu ujumuishaji wa TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji wa fasihi. Kwa hiyo, sehemu hii inazingatia mapitio ya maandiko kuhusu ujumuishaji wa TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji wa fasihi.

King (2000) anabainisha kwamba ujumuishaji wa TEHAMA katika ufundishaji wa fasihi umekuwa muhimu katika kuboresha mchakato wa ufundishaji. Awali, TEHAMA ilijumuishwa katika ufundishaji wa fasihi ili kuboresha ufundishaji na ujifunzaji. Kulingana na Sharma (2021), matumizi ya teknolojia kama vile kompyuta, simu za mkononi, na mitandao ya kijamii yameongeza ufanisi wa mbinu za ufundishaji wa fasihi. Licha ya maelezo yanayotolewa King (khj) anajikita katika nafasi ya TEHAMA katika ufundishaji wa fasihi ya lugha ya Kijerumani ambayo ni tofauti sana na lugha ya Kiswahili inayoshughulikiwa katika utafiti wetu.

Kulingana na Lazar (1993), kujumuisha teknolojia TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji wa fasihi ni muhimu katika kuhamasisha wanafunzi kujifunza fasihi. Hii ni kwa sababu teknolojia inatoa mbinu za kisasa na za kuvutia za kuwasilisha na kuelewa maudhui ya fasihi, ikiwemo video, sauti, na maandiko ya kidijitali ambayo yanaboresha ushirikiano na ushiriki wa wanafunzi. Warschauer & Healey (1998) wanaonesha kuwa matumizi ya TEHAMA husisimua wanafunzi na husaidia walimu kubadilisha njia zao za ufundishaji kwa kuzingatia maslahi ya wanafunzi kupitia zana za kufundishia na kujifunzia zinazotumia teknolojia. Hivyo, TEHAMA imekuwa njia inayopendelewa sana, hasa katika vyuo vikuu, katika kukuza hamasa ya wanafunzi katika kujifunza fasihi (Warschauer & Healey, whj).

Maelezo haya yanaonesha kwamba TEHAMA ina mchango mkubwa katika ufundishaji wa fasihi. TEHAMA na Riwaya, TEHAMA imewezesha riwaya kusambazwa kwa urahisi kupitia vitabu vya kielektroniki (e-books) na majukwaa ya mtandaoni kama Amazon na Wattpad, hivyo kufikia wasomaji wengi zaidi. Pia, waandishi wa riwaya wanaweza kushirikiana na kupata mrejesho wa haraka kutoka kwa wasomaji. TEHAMA na Tamthilia, Tamthilia zinaweza kuonyeshwa kupitia majukwaa ya kidijitali kama YouTube na Netflix, zikifikiwa na hadhira kubwa. Pia, teknolojia ya kuandika tamthilia kidijitali kama Celtx inarahisisha uandishi na upangaji wa maandiko.

TEHAMA na Ushairi, TEHAMA imerahisisha usambazaji wa mashairi kupitia blogu, mitandao ya kijamii, na majukwaa ya mtandaoni kama Instagram, ambapo washairi wanaweza kushiriki kazi zao na kupata mrejesho wa papo hapo. Pia, zana za kidijitali zinaimarisha uandishi wa mashairi kwa kusaidia uhakiki wa kisarufi., TEHAMA na Hadithi Fupi Andishi, Hadithi fupi zimepata jukwaa kubwa zaidi kupitia TEHAMA, ambapo waandishi wanaweza kuchapisha kazi zao mtandaoni kupitia blogu na tovuti za fasihi. Hii inawezesha wasomaji wengi kupata hadithi hizi na kuongeza fursa za maoni ya haraka na usambazaji.

Aidha, matumizi ya TEHAMA yanachukuliwa kama sehemu muhimu ya kuboresha elimu kulingana na mtaala (Ahmadi, 2018). Hii inamaanisha kwamba matumizi ya TEHAMA huweza kuimarisha mchakato wa kufundisha na kujifunza fasihi. Utafiti wa Mugabo (2010) unaonesha kuwa TEHAMA inachangia kwa kiasi kikubwa katika ufundishaji na ujifunzaji wa fasihi, hasa katika elimu ya juu kwa kuwa wanfunzi wanajitegemea sana katika masomo yao. Kulingana na Zainal (2012), ujumuishaji huu wa TEHAMA umekuwa na matokeo chanya, ukiwa na ufanisi mkubwa kwa walimu na wanafunzi.

Kulingana na Zainal (khj), uwezo wa dijiti wa wanafunzi na walimu pamoja na maandalizi ya walimu yanayozingatia TEHAMA ni mojawapo ya sababu kuu za mafanikio katika mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji unaotumia teknolojia. Hivyo, ujumuishaji wa TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji wa fasihi unachukua jukumu muhimu katika kuboresha ufanisi wa kujifunza kwa wanafunzi katika maeneo mbalimbali ya fasihi.

Isitoshe, ujumuishaji wa TEHAMA katika ufundishaji wa lugha, pamoja na fasihi, huongeza ufanisi wa kujifunza kwa kuwawezesha wanafunzi kutumia vifaa vya digiti vinavyowawezesha kushiriki kikamilifu na kufurahia masomo ya fasihi (Warschauer & Kern, 2000). Matumizi ya TEHAMA katika ufundishaji wa fasihi hufanya mchakato huu kuwa wa kuvutia na kuburudisha, ikizingatiwa kuwa fasihi inalenga kufundisha maadili na kukuza furaha (Sharma, khj). Ujumuishaji wa TEHAMA pia hutoa zana za mtandaoni kwa ajili ya masomo ya fasihi, kuruhusu wanafunzi kufurahia kusoma fasihi mtandaoni na kuonesha uwezo wao wa ubunifu wa lugha na maadili ya kibinadamu kupitia njia za kisasa (Zainal, 2012).

Hivyo, ujumuishaji wa TEHAMA una nafasi kubwa katika kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa fasihi, kwa kuchochea hamu na ufanisi wa wanafunzi katika kuelewa na kushiriki kikamilifu

katika dunia ya fasihi. Ingawa tafiti zilizopita zimezungumzia umuhimu wa TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji wa fasihi, bado kuna dosari ambazo zinahitaji kurekebishwa. Kwanza, tafiti hizo zilijikita zaidi katika ujumuishaji wa TEHAMA katika ufundishaji wa Kiingereza na Kijerumani, tofauti na lugha ya Kiswahili ambayo ni lengo letu. Pili, tafiti zilizingatia hasa wanafunzi wa vyuo vikuu, na hivyo hazikutoa nafasi ya kupata ufahamu wa kina kuhusu jinsi ya kufundisha fasihi kwa wanafunzi wa shule za sekondari ambao hawana uzoefu mkubwa na mada mbalimbali za fasihi.

Zaidi ya hayo, tafiti hizo hazikuunda miongozo ya kufuatiliwa na walimu katika kujumuisha TEHAMA kwa lengo la kuboresha ufundishaji na ujifunzaji wa fasihi. Hivyo, utafiti uliofanyika ulikusudia kutatua dosari hizo kwa kuunda miongozo thabiti ya matumizi ya TEHAMA katika ufundishaji wa fasihi andishi katika shule za sekondari wilayani Nyagatare, Rwanda.

## 2.5 Miongozo ya Utumiaji wa TEHAMA katika Ufundishaji wa Fasihi Andishi

### 2.5.1 Utumiaji wa Projekta na Slaidi

Ufundishaji wa drama, tamthilia au riwaya katika darasa la fasihi ni shughuli inayoweza kuwa na matokeo mazuri kupitia matumizi ya zana za TEHAMA kama vile projekta (Al-Kamel & Chouthaiwale, 2020). Matumizi ya projekta yanawezesha mwalimu kuunda uwasilishaji wenye slaidi zinazo undwa kwa upekee husaidia wanafunzi kuelewa kwa kina na kufurahia tanzu mbalimbali za fasihi. Hii inaweza kubadilisha jinsi wanafunzi wanavyochukulia fasihi na kuwahamasisha kushiriki kikamilifu katika masomo ya fasihi.

Kwa kutumia teknolojia, mwalimu anaweza kuwasiaida wanafunzi kupata uzoefu wa kipekee na wa kuvutia katika kuchambua na kuelewa mawazo na hisia zilizomo katika kazi za fasihi (Hashemi, Azizinezhad & Farokhi, 2012). Hii ina maana kwamba, matumizi ya TEHAMA yanatoa njia mpya na ya kisasa ya ufundishaji wa fasihi ambayo inafanya ufundishaji wa fasihi kuwa wa kuvutia na kusisimua.

Pia, kupitia matumizi ya projekta, rasilimali mbalimbali za mtandaoni zinaweza kufikiwa na kuwasilishwa kwa ajili ya kufanikisha ufundishaji na ujifunzaji wa tanzu tofauti za fasihi andishi (Jones & Patel, 2018). Kwa mfano, walimu wanaweza kuwasilisha slaidi kwa kutumia projekta ili kuonesha mada mbalimbali za fasihi kutoka kwenye vyanzo vya mtandaoni. Jambo hili

linaweza kuwapa wanafunzi uzoefu wa moja kwa moja kuhusu tanzu mbalimbali za fasihi (Jones & Patel, whj).

Hii inamaanisha kuwa, wakati wa ufundishaji wa fasihi, mwalimu anaweza kupakua maudhui mbalimbali ya fasihi kutoka mtandaoni, kuyaandaa kwa ufasaha na kuyawasilisha kwa mtindo wa slaidi akitumia projekta. Hii inaweza kusaidia walimu kuhifadhi muda ambao ungeweza kupotea wakiwa wanatumia njia ya ufundishaji ya kijadi ya kuandika kila kitu ubaoni kwa kutumia chaki.

Aidha, Garcia & Hernandez (2019) wanasema kwamba, projekta na slaidi huweza kutumiwa na walimu wa fasihi ili kuepuka mfumo wa zamani wa kufundisha fasihi katika darasa lenye chaki, ubao na vitabu tu. Mfumo huo wa zamani ulikuwa unachosha walimu na wanafunzi na kusababisha upungufu wa hamu ya kujifunza fasihi.

Hata hivyo, Garcia & Hernandez (whj) wanasema kuwa, kupitia matumizi ya projekta na slaidi, ufundishaji wa fasihi unaweza kuwa bora na wa kuvutia zaidi kwa kuwasaidia walimu na wanafunzi. Kwa njia hii, mwalimu anaweza kuhamasisha hamu ya kujifunza fasihi miongoni mwa wanafunzi kwa njia inayorahisisha mchakato wa ufundishaji na kufanya masomo ya fasihi kuwa yenye kuvutia zaidi. Kwa ujumla, matumizi sahihi ya projekta na slaidi katika ufundishaji wa fasihi yanaweza kutoa njia mpya na ya kuvutia.

Kwa ujumla, maelezo tuliopitia tafiti zao yanaonesha kuwa matumizi sahihi ya projekta na slaidi katika ufundishaji wa fasihi yanaweza kutoa njia mpya na ya kuvutia kwa walimu na wanafunzi. Licha ya maelezo haya, bado kungali na mapengo ya kuzibwa hizi. Mosi, tafiti hizi zilizungumzia matumizi ya projekta na slaidi katika ufundishaji wa fasihi ya Kiingereza ambayo haifanani na lugha ya Kiswahili. Pili, tafiti tulizozipitia hazikujihusisha namna ambavyo TEHAMA huweza kutumiwa katika ufundishaji wa tanzu tofauti za fasihi andishi. Mwisho, tafiti tulizozipitia hazikutoa mwongozo dhahiri wa utumiaji wa projekta na slaidi katika ufundishaji na ujifunzaji wa fasihi.

Hivyo basi, utafiti uliofanyika ulikusudia kujaza mapengo haya kwa kuunda miongozo ya utumiaji wa TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji wa fasihi andishi ya Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za sekondari wilayani Nyagatare.

### 2.6.2 Utumiaji wa Usimulizi wa Kidijiti

Usimulizi wa kidigiti ni mojawapo ya njia zinazotumiwa na walimu katika kufundisha fasihi. Kutokana na Karantalis & Koukopoulos (2022), usimulizi wa kidigiti ni chombo ambacho kimechunguzwa kwa kina na kutumiwa sana katika mchakato wa elimu kwa njia mbalimbali. Watafiti hawa wanaeleza kwamba stadi za ubunifu, utafiti na ushirikiano zinazopatikana katika usimulizi wa kidigiti zinakidhi vizuri nadharia za kisasa za kujifunza. Usimulizi wa kidijitali unafanya kazi kwa kutumia teknolojia kama tovuti, video, na podcast kusimulia hadithi. Huendana zaidi na fasihi simulizi kwa sababu ya matumizi ya sauti, video, na maingiliano, ingawa pia unaweza kuingiza maandishi (blogu, e-books). Kama ni andishi, hutumia maandishi kwenye majukwaa ya kidijitali kama blogu au vitabu vya mtandaoni, na mara nyingi hujumuisha vipengele vingine kama picha na sauti. Mchango wake katika fasihi andishi ni kurahisisha ushirikiano, kufikia wasomaji wengi, na kuunda mitindo mipya ya usimulizi kwa kuchanganya maandishi na teknolojia.

Kwa hiyo, usimulizi wa kidijiti unaweza kutumika siyo tu katika ufundishaji wa fasihi, bali pia katika elimu kwa ujumla. Hii inaonesha kuwa usimulizi wa kidigiti unapotumiwa kwa ufanisi na walimu, unaweza kufanikisha mchakato wa kufundisha na kujifunza fasihi andishi. Kulingana na Prensky (2001), matumizi ya usimulizi wa kidigiti katika ufundishaji wa masomo ya fasihi ni muhimu kwa maendeleo ya stadi za usimulizi kwa wanafunzi. Prensky (khj) anasisitiza kwamba usimulizi ni sehemu muhimu ya fasihi na njia za kisasa za usimulizi wa kidigiti zinaweza kuboresha mchakato wa kufundisha fasihi. Mbinu hii inachukuliwa kuwa na umuhimu mkubwa katika kuwawezesha wanafunzi kuelewa na kujifunza mbinu za usimulizi zilizopo katika kazi za fasihi. Hivyo, walimu wanatazama usimulizi wa kidigiti kama chombo muhimu katika kuendeleza stadi za usimulizi kwa wanafunzi.

Usimulizi wa kidigiti unachochea ubunifu miongoni mwa wanafunzi katika kuandika. Wanapopitia usimulizi wa kidijiti, wanafunzi hupata mwongozo mzuri wa jinsi ya kusimulia kazi za fasihi, na wanapoanza kuandika, wanajitahidi kuiga mifano mizuri waliyoiona kupitia usimulizi wa kidigiti (Karantalis & Koukopoulos, whj). Hii inawasaidia kuboresha uwezo wao wa kutunga kazi za fasihi, hasa zile za aina ya fasihi andishi. Kwa hiyo, usimulizi wa kidigiti

katika ufundishaji wa fasihi unatumiwa na walimu ili kukuza stadi za ubunifu na uandishi miongoni mwa wanafunzi.

Kwa ufupi, watafiti hawa wanaonesha kwamba usimulizi wa kidijiti hutumiwa na walimu wa fasihi ili kukuza stadi za masimulizi na za kutunga kazi za fasihi miongoni mwa wanafunzi. Hata hivyo, watafiti hawa hawajabainisha miongozo ya utumiaji wa usimulizi wa kidijiti katika ufundishaji na ujifunzaji wa fasihi. Hivyo basi, utafiti uliofanyika ulikusudia kukamilisha tafiti hizikwa kuunda miongozo ya utumiaji wa TEHAMA kupitia usimulizi wa kidijiti katika ufundishaji wa fasihi ya Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za sekondari wilayani Nyagatare.

### 2.6.3 Utumiaji wa Mitandao ya Kijamii

Ufundishaji na ujifunzaji wa fasihi umechukuliwa kama eneo lenye changamoto na mabadiliko mengi. Hii ni kutokana na mwelekeo wa sasa katika teknolojia ambao umebadilisha si tu njia za kufundisha bali pia njia za kujifunza. Hivyo, hii ni enzi mpya ya kuunganisha teknolojia.

Mbinu na programu nyingi na zana za teknolojia zimekuwa zikitumika katika mazingira ya kufundisha na kujifunza (Haidari, Katawazai & Mohd Yusof, 2020). Mojawapo ya mbinu za TEHAMA zinazoweza kutumiwa katika ufundishaji wa fasihi ni utumiaji wa mitandao ya Kijamii.

Mitandao ya kijamii ni majukwaa ya mtandao ambayo huruhusu watu kushirikiana, kubadilishana habari, na kuwasiliana mtandaoni. Kulingana na hilo, walimu wa lugha wamechagua kutumia mitandao ya kijamii kama njia bora ya kufundisha lugha (Ahn & Seo, 2010). Kupitia mitandao ya kijamii, wanafunzi na walimu wanaweza kuwasiliana kwa urahisi mahali popote na wakati wowote kwa kutumia aina mbalimbali za majukwaa ya mtandaoni.

Hii inafanya mchakato wa kujifunza kuwa rahisi kwa wanafunzi (Benson & Thurman, 2013). Hivyo, hili linaonesha kuwa mitandao ya kijamii ni mojawapo ya mbinu ambazo zinaweza kutumika na walimu wa fasihi ili kuboresha mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji wa somo hili.

Aidha, Reinhardt (2019) anaonesha kwamba walimu wa fasihi wanatumia mitandao ya kijamii kusaidia wanafunzi kuimarisha stadi zao za utungaji wa kazi za fasihi. Kupitia mitandao ya kijamii, wanafunzi wanaweza kuwasiliana na walimu, wenzao, au watu wengine, na hivyo kujishughulisha na mazoezi mengi ya kuandika na kuhakikisha maandishi yao yana ubora na

hayana makosa (Androutsopoulos, 2015). Mazoezi haya ya kuandika yanachangia katika kusaidia wanafunzi kuandaa mawazo yao vizuri kabla ya kuyawasilisha kwa umma. Hili ni, jambo muhimu katika utungaji wa kazi za fasihi. Hivyo, mitandao ya kijamii inakuwa jukwaa la kuvutia na lenye manufaa kwa walimu na wanafunzi katika kukuza ujuzi wa uandishi na kutoa fursa ya kuonesha ubunifu wao katika uwanja wa fasihi.

Zaidi ya hayo, mitandao ya kijamii inachangia kukuza stadi za uchambuzi miongoni mwa wanafunzi (Nanda & Kumar, 2021). Ufundishaji wa fasihi unahitaji ujuzi wa kuchanganua na kuelewa kina cha maandishi. Kupitia majukwaa ya mitandao ya kijamii, wanafunzi wanapata fursa ya kujadili, kuchambua na kutoa maoni kuhusu tanzu mbalimbali za kazi za fasihi kama vile riwaya, ushairi na tamthilia. Hii inawawezesha kuendeleza ujuzi wao wa kuelewa maudhui, muktadha na muundo wa fasihi. Wanaposhiriki katika majadiliano na kutoa maoni yao, wanafunzi wanajengewa uwezo wa uchambuzi wa kina na hivyo kuwa na ufahamu bora wa kazi za fasihi wanazosoma. Kwa hiyo, mitandao ya kijamii inachangia katika kuimarisha uwezo wa uchambuzi ambao ni muhimu kwa wanafunzi wa fasihi.

Kwa ufupi, maelezo ya hapo juu yanaonesha kuwa, mitandao ya kijamii inaweza kutumiwa na walimu ili kuboresha mawasiliano, uandishi na uchambuzi wa fasihi kwa wanafunzi. Licha ya maelezo haya kutolewa, watafiti hawawamezungumzia tu utumiaji wa mitandao ya kijamii katika ufundishaji wa Kiingereza. Pengine, watafiti hao hawakutoa mwongozo wa utumiaji wa mitandao ya kijamii katika ufundishaji wa fasihi. Hivyo basi, utafiti uliofanyika ulikusudia kukamilisha tafiti hizi kwa kutoa mwongozo wa utumiaji wa mitandao ya kijamii katika ufundishaji na ujifunzaji wa fasihi ya Kiswahili katika shule za sekondari wilayani Nyagatare.

## 2.7. Mapengo ya Tafiti Tangulizi

Sehemu hii inaangazia kujadili mapengo ya tafiti mbalimbali ambazo zilipitiwa. Kwa hiyo hapo chini ni baadhi ya mapengo yaliyodhihirika na ambayo yatajazwa na utafiti wetu. Kwanza, tafiti za Nkwera (1970), Njogu & Chimerah (1999), Meskills & Ranglova (2000), Wamitila (2003), Mishra & Koehler (2006) zilieleza tu dhana ya TEHAMA na fasihi bila kuonesha uhusiano uliopo kati ya dhana hizi mbili.

Pili, tafiti zilizofanywa na Makaun (1990), Schauman (2001), Fellenz & Brady (2007), Mukama & Andersson (2008), Mbodila & Muhandji (2013) Ratheeswari (2018), Koroleva (2020) na Zeng (2022) zinaonesha namna ambavyo nchi tofauti zilijumuisha TEHAMA katika elimu. Aidha, tafiti hizi zinaonesha namna ambavyo matumizi ya TEHAMA yanaboresha mafanikio ya sekta ya elimu bila kugusia mchango wa TEHAMA katika ufundishaji wa somo la fasihi.

Tatu, tafiti za Tayib & Hassan (2020) & Gomez (2022) zinazungumzia ufundishaji wa fasihi na changamoto zinazokabili ufundishaji wa fasihi bila kugusia mbinu za utatuzi wa changamoto hizo. Nne, licha ya tafiti za Osario (2017) & Alnord (2021 kuonesha mchango wa TEHAMA katika ufundishaji wa fasihi, tafiti zinaandikwa na kushughulika na lugha ya Kiingereza tu tofauti na lugha ya Kiswahili.

Mwisho, tafiti za Stanley (2018) na Sarah & Msigwa (2021) zinaonesha mchango wa TEHAMA katika ufundishaji wa Kiswahili kwa ujumla. Tafiti hizi hazioneshi mchango wa TEHAMA katika ufundishaji wa Kiswahili hasa somo la fasihi katika lugha hiyo.

Hivyo basi, ili kujaza mapengo hayo, tuliamua kufanya utafiti wenye mada "Mchango wa TEHAMA katika Ufundishaji wa Fasihi Andishi katika Shule za Sekondari Wilayani Nyagatare Nchini Rwanda". Utafiti wetu ulifanyika kwa kusudi la kutoa mwongozo bora wa kuwasaidia walimu wa Kiswahili kufanikisha ufundishaji wa fasihi andishi kwa kutumia TEHAMA.

### 2.8. Nadharia ya Utafiti

Utafiti wetu uliongozwa na Nadharia ya Uunganisho. Nadharia hii inasisitizia umuhimu wa mitandao na uhusiano katika mchakato wa kujifunza. Kulingana na Alam (2023). Nadharia ya Uunganisho, iliyoanzishwa na George Siemens mwaka 2004, inaelezea kuwa kujifunza ni mchakato unaotegemea mazingira yanayojaa uhamishaji wa maarifa na hauko chini ya udhibiti kamili wa mtu mmoja (Munyengabire, 2024). Kulingana na nadharia hii, maarifa hupatikana kupitia mifumo ya ushirikiano ambapo watu wanashiriki katika shughuli za kujifunza (Mechlova & Malcik, 2012). Hii inamaanisha kwamba elimu, maarifa na ujuzi hupatikana kupitia ushirikiano na kushirikishwa kwa lengo la kufanikisha malengo ya kielimu.

Munyengabire (khj) anaeleza kuwa Nadharia ya Uunganisho inajumuisha mihimili miwili muhimu. Mhimili wa kwanza unasisitiza kwamba katika mchakato wa kujifunza, wanafunzi

wanapaswa kushirikiana kwa kutumia mawazo yao, kanuni na taarifa kwa njia inayofaa. Katika muktadha huu, tulipanga kutumia mhimili wa kwanza ili kubainisha mchango wa TEHAMA katika ufundishaji wa fasihi andishi katika shule za sekondari teule wilayani Nyanza. Hii ni kwa sababu uhusiano wa mara kwa mara kati ya wanafunzi kutoka asili mbalimbali unawapa nafasi ya kuchagua jinsi ya kujifunza kulingana na mahitaji yao, hivyo kuimarisha ufundishaji wa fasihi andishi kupitia TEHAMA.

Mhimili wa pili wa nadharia husika unasisitiza umuhimu wa tathmini ya kibinafsi. Inafafanua kwamba matumizi ya TEHAMA katika mchakato wa kufundisha yanaweza kuwa na kasoro na changamoto. Tulipanga kutumia mhimili huu katika uundaji wa miongozo ya utumiaji wa TEHAMA katika ufundishaji wa fasihi andishi katika shule za sekondari wilayani Nyanza. Aidha, tulipanga kutumia mhimili husika kwa kuzingatia changamoto zinazoweza kujitokeza kwa walimu, wanafunzi na jamii kwa ujumla. Hivyo, tulitarajia kwamba mhimili huu utatusaidia kuunda miongozo bora ya jinsi ya kutumia TEHAMA bila kupotosha malengo ya ufundishaji na ujifunzaji.

## 2.9. Muhtasari wa Sura ya Pili

Sura ya pili inahusu mapitio ya maandiko mbalimbali ambayo yana uhusiano na mada ya utafiti uliofanyika. Sura husika imegawanyika katika sehemu tisa: ufundishaji na ujifunzaji wa fasihi, ujumuishaji wa TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji wa lugha, mchango wa TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji wa lugha, mchango wa TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji wa fasihi, mwongozo wa utumiaji wa TEHAMA katika ufundishaji wa fasihi, mapengo ya tafiti tangulizi nadharia ya utafiti na muhtasari wa sura.

# SURA YA TATU: METHODOLOJIA YA UTAFITI

## 3.1 Utangulizi

Methodolojia ya utafiti ni mpango wa mfumo wa kufanya utafiti. Kwa mujibu wa Redman & Mory (2015), methodolojia ya utafiti inafafanua njia au taratibu zinazotumiwa kukusanya na kuchambua data. Pia, inaeleza jinsi mtafiti anavyotarajia kushughulikia malengo na maswali ya utafiti (Redman & Mory, whj). Hii inamaanisha kwamba methodolojia ya utafiti ni ramani au mpango wa kina unaosimamia utekelezaji wa mradi wa utafiti. Kwa hiyo, sura hii ina vipengele muhimu vifuatavyo: utangulizi, paradima ya utafiti, usanifu wa utafiti, eneo la utafiti, wango la utafiti, sampuli ya utafiti, mbinu za kukusanyia data, aina ya data, vifaa vya utafiti, uchanganuzi wa data, itikeli za utafiti, uhalali na uthabiti wa utafiti, mpango kazi wa utafiti na muhtasari wa sura ya tatu.

## 3.2 Paradima ya Utafiti

Paradima ya utafiti ni mfumo wa falsafa unaosimamia utafiti unaofanyika (Abdul & Alharthi, 2016). Hii ni njia au mfano uliokaguliwa na kukubaliwa na jamii ya watafiti. Kutokana na Abdul & Alharthi (whj), paradima ya utafiti inaakisi imani na dhana za mtafiti kuhusu asili ya ukweli, maarifa na utafiti. Paradima ya utafiti inachangia katika nadharia na njia zinazotumiwa na mtafiti katika kukamilisha mradi wa utafiti.

Kulingana na lengo la jumla na malengo mahususi ya utafiti wetu, paradima ya ufasiri ilitumiwa. Kulingana na Creswell & Poth (2017), paradimaa ya ufasiri ni imani kwamba watu mbalimbali katika jamii wanaweza kuelewa na kuchukulia mambo kwa njia tofauti. Hii inamaanisha kuwa kila mtu katika jamii ana mtazamo wake kuhusu ukweli. Wazo hili linasisitiza kwamba hakuna ukweli mmoja.

Kwa kujiegemeza katikamawazo ya paradima ya ufasiri, utafiti ulizikusanya data za kitaamuli ili kuchunguza nafasi ya TEHAMA katika ufundishaji wa fasihi andishi katika shule za sekondari wilayani Nyagatare nchini Rwanda. Aidha, katika utafiti huo, mtafiti alikusanya taarifa kutoka kwa washiriki wa aina tofauti (walimu, wanafunzi, viongozi wa shule na wakuu wa masomo), ili kupata data za kuaminika.

Taarafa zilizotolewa na watoa taarifa hawa zililinganishwa ili kutimiza malengo ya utafiti. Vilevile, kwa kuwa washiriki wa utafiti wanaweza kuathiriwa na mazoea yao na kutoa taarifa ambazo si faafu, mtafiti alilazimika kufanya ushuhudiaji ili kufahamu mchango wa TEHAMA katika ufundishaji wa fasihi katika shule za sekondari Wilayani Nyagatare nchini Rwanda.

Zaidi ya hayo, kwa kuwa watafiti huweza kutofautiana kutokana na mambo tofauti, mtafiti alizichanganua matini za watafiti tofauti na data zilizopatikana zililinganishwa ili kuunda miongozo ya utumiaji wa TEHAMA katika ufundishaji wa fasihi katika shule za sekondari wilayani Nyagatare nchini Rwanda. Mwisho, utafiti uliofanyika ulishirikisha walimu na wanafunzi ambao wana ujuzi, uwezo na usoefu katika fasihi andishi ili kupata taarifa faafu katika utimizaji wa malengo ya utafiti.

**3.3 Usanifu wa Utafiti**

Kwa mujibu wa Jilcha Sileyew, (2020), usanifu wa utafiti ni mpango mzima, muundo au mikakati inayoongoza mchakato wa utafiti. Usanifu wa utafiti husaidia mtafiti kuchagua zana na njia sahihi zaidi za kukusanya na kuchambua data. Pia, usanifu wa utafiti huthibitisha umakini, uaminifu na uhalali wa matokeo ya utafiti. Kwa hiyo, huchaguliwa kulingana na mada ya utafiti, malengo ya utafiti na maswali ya utafiti (Jilcha, khj). Hivyo basi, hulingana na mada, malengo na maswali ya utafiti, utafiti wetu ulikuwa wa kitaamuli.

Utafiti wa kitaamuli ni aina ya usanifu wa utafiti inayojikita katika uga wa data za kidhahania kama vile uzoefu, maoni, mada na motisha (Bryman, 2006). Usanifu wa kitaamuli hutumiwa kupanga na kutekeleza utafiti ambao unamruhusu mtafiti kuchunguza mitazamo ya watu kuhusu mambo tofauti. Hivyo basi, data zilizokusanywa zilikuwa za kitaamuli. Data hizi zilikusanywa, kuchanganuliwa, kufasiliwa na kuwasilishwa kwa kutumia nukuu na maelezo.

**3.4 Eneo la Utafiti**

Kulingana na Kothari (2012), eneo la utafiti ni mahali ambapo shughuli za utafiti zitafanyika kwa lengo la kukusanya data zinazohitajika ili kutimiza malengo mahususi ya utafiti husika. Wilaya ya Nyagatare iko mbali na jiji la Kigali ambalo limepiga hatua katika matumizi ya vifaa vya tekinolojia. Katika wilaya ya Nyagatare kuna shule kadhaa zilizopo vijijini ambapo si rahisi kujumuisha TEHAMA katika ufundishaji kwa sababu ya ukosefu wa miondombinu fanisi. Kwa hiyo, mambo huifanya wilaya ya Nyagatare kuwa eneo halali katika utafiti wetu.

### 3.4 Wango na Sampuli ya Utafiti

#### 3.4.1 Wango la Utafiti

Wango la utafiti ni kundi la watu au vitu ambavyo sampuli itachaguliwa kwa unasibu au kwa makusudi (Majid, 2018). Katika wetu, wango lilihusisha wakurugenzi, viongozi wa masomo, walimu wa Kiswahili na wanafunzi wanaojifunza katika mchepuo wa LFK (Fasihi katika Kiingereza, Kifaransa, Kinyarwanda na Kiswahili) katika shule za sekondari wilayani Nyagatare.

#### 3.4.2 Sampuli ya Utafiti

Kwa mujibu wa Majid (khj), sampuli ya utafiti ni kundi dogo la watu au vitu vinavyochaguliwa kutoka kwenye kundi kubwa la watu au vitu. Sampuli ya utafiti huwa na lengo la kuwakilisha na kutoa matokeo yanayoweza kujumuishwa katika uchambuzi na fasiri ya data (Ishtiaq, 2019). Sampuli huchukuliwa kama picha ndogo inayowezesha watafiti kutoa hitimisho kuhusu kundi kubwa kulingana na sifa na tabia za sampuli iliyochaguliwa. Aidha, ili kuteua sampuli ya utafiti, hutumia mbinu tofauti za usampulishaji.

Kutokana na Ishtiaq (khj), usampulishaji ni mchakato wa kuteua kikundi kidogo cha watu au vitu kutoka kwenye kundi kubwa ili kufanya utafiti na kutoa hitimisho kuhusu kundi zima. Kwa hiyo, kutokana na aina, mada, malengo na maswali ya utafiti wetu, mbinu ya usampulishaji lengwa ilitumiwa kwa kuteua sampuli ya utafiti.

Kwa mujibu wa Palys (2008), usampulishaji lengwa ni mchakato wa kuchagua sampuli kwa makusudi kulingana na vigezo fulani au lengo maalum katika utafiti. Katika utafiti uliofanyika, sampuli ilihusisha walimu wa Kiswahili 10 na wanafunzi wote wanaojifunza katika kidato cha 6 katika mchepuo wa LFK katika shule za sekondari wilayani Nyagatare.

Shule ambamo sampuli ya utafiti ilichaguliwa ni shule ya sekondari ya Cyabayaga katika Tarafa ya Mimuli, Nyagatare katika Tarafa ya Nyagatare, Gishororo katika Tarafa ya Mukama, Kabale II, katika Tarafa ya Kiyombe na shule ya sekondari ya Bufunda katika Tarafa ya Mukama.

Walimu walioshiriki katika utafiti tuliofanya ni walimu wa Kiswahili 5 katika shule 5 ambamo utafiti ulifanyika. Vilevile, wanafunzi wote wa kidato cha 6 LFK walishirikishwa katika utafiti uliofanyika kupitia ushuhudiaji kwa kuwa ndio ambao wanajifunza mada nyingi za fasihi andishi ya Kiswahili.

Isitoshe, ingawaje, wilaya ya Nyagatare ina shule za sekondari nyingi, shule 5 tu zilichaguliwa kwa kuwa ndizo ambazo zina mchepuo wa LFK na maabala ya kompyuta ambapo fasihi ya Kiswahili hufundishwa. Sampuli ya utafiti uliofanyika iligawika kama ifuatavyo.

Mosi, sampuli ilihusisha walimu wa Kiswahili 10. Kwa kawaida, kila shule ya sekondari inakuwa na mwalimu 1 wa Kiswahili. Hii ina maana kwamba sampuli ya utafiti ingehusisha walimu 5 wanaofundisha Kiswahili katika shule teule. Kwa lengo la kuongeza idadi ya walimu walioshiriki katika utafiti huu, mtafiti aliwashirikisha walimu wengine 5 ambao wanafundisha Kiswahili katika shule ambazo ni majirani ya shule teule. Jambo hili lilifanyika kwa lengo la kupata taarifa za kutosha kutoka kwa walimu wa Kiswahili. Walimu wa Kiswahili walichaguliwa kimakusudi kwa kuwa ndio ambao wana taarifa na ujuzi wa kutosha kuhusu ufundishaji wa fasihi ya Kiswahili.

Hii ni kwa sababu miongoni mwa walimu walioshiriki katika utafiti huu, kulikuwepo walimu wa fasihi. Hata, na wale ambao hawafundishi fasihi, wanaweza kutoa taarifa za kuaminika kwa kuwa nao walijifunza somo la fasihi kwa shule za sekondari na vyuo vikuu.

Mwisho, usampulishaji ulihusisha wanafunzi wote ambao wanajifunza katika kidato cha 6 katika mchepuo wa LFK kwenye shule teule wilayani Nyagatare nchini Rwanda. Kwa kuwa mtafiti alilazimika kushuhudia somo la fasihi likifundishwa, wanafunzi wote wa kidato cha 6 katika kila shule walishiriki katika utafiti huu.

Wanafunzi wa kidato cha 6 walichaguliwa kwa kuwa wana uelewa na ujuzi zaidi katika somo la fasihi kuliko wanafunzi wa madarasa ya chini au vidato vingine. Vilevile, wanafunzi hawa wanasoma mada nyingi za fasihi ukilinganisha na wa kidato cha 4 na cha 5 LFK. Hii inafanya iwe rahisi kwa wanafunzi wa kidato cha 6 LFK kutoa taarifa za kina na za maana kuhusu matumizi ya TEHAMA katika ufundishaji wa fasihi andishi ya Kiswahili.

### 3.5 Mbinu za Ukusanyaji wa Data

Mbinu za ukusanyaji wa data ni njia au taratibu zinazotumika kukusanya taarifa kutoka vyanzo mbalimbali kwa ajili ya uchambuzi na maamuzi sahihi. Kwa hiyo, mbinu za ukusanyaji wa data ambazo zilitumiwa ni mbinu ya usaili, uchanganuzi wa matini na usaili.

### 3.5.1 Usaili

Usaili ni mbinu ya ukusanyaji wa data ambayo inategemea kuuliza maswali ili kukusanya data. Usaili unaweza kuhusisha watu wawili au zaidi, ambapo mmoja wao (mtafiti) ni mwulizaji maswali (Rutledge & Hogg, 2020). Usaili mara nyingi, hutumiwa katika ukusanyaji wa data za kitaamuli. Kwa hiyo, katika utafiti uliofanyika, mbinu ya usaili ilitumika ili kukusanya data kutoka kwa wakurugenzi, viongozi wa masomo na walimu wa Kiswahili walioteuliwa katika shule za sekondari wilayani Nyagatare.

Data zilizokusanywa kupitia usaili zilikuwa na mchango mkubwa katika kutimiza lengo la kwanza la utafiti huu la kubainisha mchango wa TEHAMA katika ufundishaji wa fasihi andishi katika shule za sekondari wilayani Nyagatare nchini Rwanda. Hata hivyo, ni muhimu kutambua kuwa usaili peke yake hakutoa picha kamili ya hali halisi ya mchango wa TEHAMA katika ufundishaji wa fasihi. Ili kushughulikia changamoto hii, utafiti ulitumia mbinu changamano iliyochanganya usaili na ushuhudiaji.

### 3.5.2 Ushuhudiaji

Ushuhudiaji ni njia ya kukusanya data ambapo mtafiti anashuhudia matukio na vitendo mbalimbali ili kupata taarifa zinazohitajika kwa utafiti wake (Rapley, 2007). Njia hii ilitumiwa katika utafiti uliofanyika kwa kuwa mtafiti alihudhuria masomo ya fasihi andishi ya Kiswahili katika kidato cha 6 LFK katika shule 5 zilizoteuliwa wilayani Nyagatare.

Matokeo ya ushuhudiaji huu yalisaidia kupata data halisi kuhusu mchango wa TEHAMA katika ufundishaji wa fasihi katika shule za sekondari wilayani Nyagatare nchini Rwanda. Kwa kutumia mbinu ya usaili na ushuhudiaji tu, mtafiti hakufanikiwa kupata taarifa faafu kuhusu miongozo ya utumiaji wa TEHAMA katika ufundishaji wa fasihi katika shule za sekondari wilayani Nyagatare nchini Rwanda. Kwa hiyo, ili kupata taarifa kama hizi, mtafiti alitumia mbinu ya uchanganuzi matini.

### 3.5.3 Uchanganuzi wa Matini

Uchanganuzi wa matini ni utaratibu wa mfumo wa kuchunguza au kutathmini nyaraka. Kwa mujibu wa Rapley (2007), uchanganuzi wa matini ni mbinu ya ukusanyaji wa data ambayo inahusisha uchunguzi wa kina wa nyaraka ili kuweka wazi taarifa zote zinazohusiana na utafiti

unaofanyika. Katika utafiti uliofanyika, mbinu ya uchanganuzi wa matini ilitumiwa pale ambapo mtafiti alizichanganua matini tofauti kutoka mtandaoni au kutoka kwenye maktaba tofauti ikiwemo maktaba ya Chuo Kikuu cha Rwanda.

Mbinu ya uchanganuzi wa matini ilitusaidia kupata za kufanikisha lengo mahususi la pili ambalo ni kuunda miongozo ya utumiaji wa TEHAMA katika ufundishaji wa fasihi andishi katika shule za sekondari wilayani Nyagatare nchini Rwanda.

### 3.6 Aina ya Data Zilizokusanywa

Ili kutimiza malengo mahususi ya utafiti, mtafiti alikusanya data za ina mbili: data msingi na data za upili.

#### 3.6.1 Data za Msingi

Data za msingi ni zile ambazo zinakusanywa kwa mara ya kwanza kwa utafiti husika (Martins, Cunha & Serra, 2018). Hizi ni data ambazo hazijawahi kusanywa na mtafiti mwingine kwa lengo lolote.

Data za msingi zilikusanywa kupitia mbinu ya usaili na ushuhudiaji katika shule za sekondari wilayani Nyagatare. Data za msingi zilizokusanywa katika utafiti uliofanyika zilituwezesha kutimiza lengo la mahususi la kubainisha mchango wa TEHAMA katika ufundishaji wa fasihi andishi katika shule za sekondari wilayani Nyagatare nchini Rwanda.

#### 3.6.2 Data za Upili

Kwa mujibu wa Martins na wenzake (whj), data za upili ni taarifa data ambazo zimekusanywa, kuchakatwa na kuchapishwa na mtafiti. Data hizi zinakusanywa kwa kupitia nyaraka tofauti ambazo ziliandikwa na watafiti tofauti. Kwa hiyo, data za upili zilikusanywa kwa kutumia mbinu ya uchanganuzi matini. Hapa, mtafiti alizipitia nyaraka tofauti ili kupata data za kutimiza lengo mahususi la pili la kuunda miongozo ya utumiaji wa TEHAMA katika ufundishaji wa fasihi andishi katika shule za sekondari wilayani Nyagatare nchini Rwanda.

### 3.7 Vifaa vya Utafiti

Vifaa vya utafiti ni zana ambazo zinazotumika kukusanya, kuchambua na kutafasiri data wakati wa mchakato wa utafiti (Munck, 2004). Katika utafiti uliofanyika, vifaa vya utafiti

vilivyotumiwa ni kalamu kwa kuandika maelezo, daftari kwa kurekodi taarifa muhimu vitabu kwa ajili ya kukusanya data za upili na kamusi kwa kurejelea maana sahihi.

Aidha, mtafiti alitumia kompyuta kwa uchambuzi wa data, simu kwa mawasiliano na kinasasauti kwa rekodi za usaili. Zaidi ya hayo, mtafiti alitumia mwongozo wa usaili kwa mahojiano na ushuhudiaji. Isitoshe mwongozo wa uchanganuzi wa matini ulitumiwa kwa uchambuzi wa nyaraka tofauti. Vifaa hivi vilikusudiwa kusaidia katika kukusanya na kuchambua data kuhusu mchango wa TEHAMA katika ufundishaji wa fasihi katika shule za sekondari wilayani Nyagatare nchini Rwanda.

### 3.8 Uchanganuzi wa Data

Kwa mujibu wa Harding (2013), uchanganuzi wa data ni mchakato wa kuchambua, kutafsiri na kutoa maana kutoka kwa data zilizokusanywa ili kutimiza malengo ya utafiti. Kwa kuwa utafiti ulikuwa wa kitaamuli, data za kitaamuli zilizokusanywa zilifanyiwa uchanganuzi kwa kutumia nukuu na maelezo.

### 3.9 Itikeli za Utafiti

Itikeli katika utafiti ni hali au tatizo maalum linalomfanya mtafiti achague kati ya njia kadhaa, ambazo zinaonekana kuwa za maadili na zisizo za maadili (Drolet, Rose, Leblanc, Ruest & Williams, 2023). Itikeli za utafiti katika utafiti hutokea wakati kuna mzozo kati ya haki za washiriki katika utafiti na malengo ya utafiti wa kuzalisha data halisi, sahihi na zenye thamani. Itikeli za utafiti ni muhimu kwa kila mtu anayehusika katika mchakato wa utafiti wa kisaikolojia. Kwa mujibu wa Drolet na wenzake (whj), itikeli ya utafiti katika utafiti hujumuisha kupunguza hatari za utafiti, kulinda washiriki wa utafiti, na kuhakikisha ushiriki wa washiriki katika utafiti unakuwa wa kufahamu na wa hiari. Kwa hiyo, ili kuhakikisha itikeli ya utafiti, mambo yafuatatayo yalizingatiwa.

Mosi, kabla ya kuanza kukusanya data, mtafiti alihakikishia washiriki wa utafiti kuwa taarifa watakazozitoa zitahifadhiwa kwa siri. Hapa kutokana na mahitaji wa washiriki wa utafiti uliofanyika, taarifa zilizodhihirishwa ni shule ambapo wanafanya kazi. Kutegemeana na mahitaji yao, majina ya washiriki wa utafiti hayakuwekwa wazi kwenye utafiti uliofanyika.

Pili, mtafiti alihakikisha kwamba hakuna kitu chochote ambacho kinaweza kudhuru washiriki wa utafiti wakati wa ukusanyaji wa data au baadaye. Tatu, mtafiti alijiepusha na kuuliza washiriki wa utafiti maswali ambayo yanahusiana na maisha yao binafsi ili kuepukana na kuingilia maisha yao. Nne, kabla ya kuanza kukusanya data, mtafiti alionesha washiriki wa utafiti ridhaa inayomruhusu kufanya utafiti wake. Mwisho, mtafiti alihakikisha ushiriki wa hiari kwa kila mshiriki wa utafiti.

### 3.10 Uhalali na Uthabiti wa Utafiti

Uhalali wa utafiti ni usahihi wa taarifa, maelezo na tafsiri ya data (Brink, 1993). Kwa maneno mengine, uhalali wa utafiti unahusiana na ikiwa hitimisho zinazopatikana kutoka kwenye utafiti zinategemea data sahihi, thabiti na zinazohusiana na mada ya utafiti. Zaidi ya hayo, Sürücü & Maslakçi (2020) wanasema kwamba uthabiti wa utafiti unahusiana uaminifu wa mbinu za utafiti, ukweli, uaminifu na utopendeleo katika utafiti. Kwa hiyo, ili kuhakikisha uhalali na uthabiti wa utafiti, mambo yafuatayo yalifanyika.

Kwanza, kabla ya kuanza kutumia vifaa vya utafiti kwa kukusanya data, mtafiti alichunguza ufanisi wa kila kifaa kitakachotumiwa. Pili, mtafiti alihakikisha kuwa amewaelezea washiriki wa utafiti malengo ya utafiti kwa wazi wayoielewa. Tatu, mtafiti alitumia njia mseto. Nne, ili kuhakikisha uhalali na uthabiti wa utafiti, mtafiti alihakikisha utopendeleo wakati wa kuchanganua, kufasili na kuwasilisha data. Nne, kabla ya kuanza ukusanyaji data, mtafiti alihakikisha kuwa malengo ya utafiti wake yanaeweka waziwazi kwa kila mshiriki wa utafiti Mwisho, mtafiti alijiepusha na kukiuka methodolojia ya utafiti.

## 3.11 Mpango Kazi

**Jedwali 1: Mpango Kazi**

| | Kazi | Wakati | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Mwaka 2023 | | Mwaka 2024 | | | | | | | |
| | | Nov | Des | Jan | Feb | Mar | Apr | Mei | Jun | Jul | Ago |
| 1 | Kukusanya taarifa za msingi kukusu utafiti | | | | | | | | | | |
| 2 | Kukamilisha sura kwanza ya pendezo (?) | | | | | | | | | | |
| 3 | Kukamilisha sura ya pili | | | | | | | | | | |
| 3 | Kuandika sura ya tatu | | | | | | | | | | |
| 4 | Kutengeneza vifaa vya kukusanya dada | | | | | | | | | | |
| 5 | Kuomba ridhaa ya kukusanya data | | | | | | | | | | |
| 6 | Ukusanyaji data | | | | | | | | | | |
| 7 | Kuandika sura ya nne | | | | | | | | | | |
| 8 | Kukamilisha sura ya tano | | | | | | | | | | |
| 9 | Uwasilishaji wa mradi wa utafiti | | | | | | | | | | |
| 10 | Kuchapisha makala ya utafiti | | | | | | | | | | |

**Chanzo: (Mtafiti, 2024)**

**Imeandaliwa na**: Tulinumukiza Frodouard

**Imeidhiniswa na** Dkt. Mlaga K. Wallace, **Msimamizi**

**Saini:**

**Saini:**

### 3.12 Muhtasari wa Sura ya Tatu

Sura ya tatu imejihusisha na methodolojia ya utafiti. Sura husika imegawanyika katika vipengele tofauti. Vipengele hivyo ni utangulizi, paradima ya utafiti, usanifu wa utafiti, eneo la utafiti, wango la utafiti, sampuli ya utafiti, mbinu za kukusanyia data, aina ya data, vifaa vya utafiti, uchanganuzi wa data, itikeli ya utafiti, uhalali wa utafiti, uthabiti wa utafiti, mpango kazi wa utafiti na muhtasari wa sura ya tatu.

# SURA YA NNE : MJADALA NA UWASILISHAJI WA MATOKEO YA UTAFITI

## 4.1 Utangulizi

Sura ya nne inahusisha mjadala na uwasilishaji wa matokeo ya utafiti. Kwa hiyo, sura hii inagawanyika katika sehemu nne: utangulizi, mchango wa TEHAMA katika ufundishaji wa fasihi katika shule za sekondari na miongozo ya utumiaji wa TEHAMA katika ufundishaji wa fasihi katika shule za sekondari. Sehemu ya mwisho ni muhtasari wa sura hii.

## 4.1 Mchango wa TEHAMA katika Ufundishaji wa Fasihi Andishi ya Kiswahili katika Shule za Sekondari

Ili kutimiza lengo la kwanza la utafiti, kwanza, mtafiti alitumia uchambuzi wa matini kuhusu mchango wa TEHAMA katika ufundishaji wa fasihi andishi. Pili, mtafiti alifanya usaili mahojiano wa wakuu wa masomo, viongozi wa shule na walimu wa Kiswihili katika shule za sekondari teule wilayani Nyagatare. Aidha, mjadala katika sehemu hii uliegemezwa katika mhimili wa kwanza wa Nadharia ya Uunganisho, unaosema kuwa katika mchakato wa kujifunza, wanafunzi wanapaswa kushirikiana kwa kutumia mawazo yao, kanuni na taarifa za jumla kwa njia inayofaa.

### 4.1.1 TEHAMA Inawasaidia Wanafunzi Kufikia Kazi za Fasihi Andishi ya Kiswahili na Vyanzo vya Kitaaluma kwa Urahisi

Kwanza, matini zilizochambuliwa zinaonesha kwamba, TEHAMA inawasaidia wanafunzi kufikia kazi za fasihi na vyanzo vya kitaaluma kwa urahisi, na hii ina athari kubwa katika ufundishaji na kujifunza fasihi andishi. Kwa kutumia zana za kidijiti kama vile vitabu vya kielektroniki, maktaba mtandaoni na majukwaa ya utafiti, wanafunzi wanaweza kupata maandiko ya fasihi, tafsiri na maelezo ya kina kwa urahisi. Wazo hili linathibitishwa na dondoo la hapo chini:

> Digital tools such as e-books and online libraries facilitate students’ access to literary texts and critical resources, enabling them to engage deeply with literature and improve their analytical skills. The availability of electronic resources enhances students' ability to explore various interpretations and scholarly critiques, leading to a more comprehensive understanding of literary works. **Chanzo**: Smith (2022:45)

> Vifaa vya kidijiti kama vitabu vya kielektroniki na maktaba mtandaoni vinawasaidia wanafunzi kufikia maandiko ya fasihi na vyanzo vya kitaaluma, na kuwafanya waweze kujiingiza kwa kina katika fasihi na kuboresha ujuzi wao wa kuchambua. Upatikanaji wa rasilimali za kielektroniki unaimarisha uwezo wa wanafunzi kuchunguza tafsiri mbalimbali na tafiti za kitaaluma, hivyo kupelekea kuelewa kwa kina zaidi kazi za fasihi (TY).

Dondoo hili linaonesha kwamba zana za kidijiti husaidia wanafunzi kupata maandiko ya fasihi na vyanzo vya kitaaluma kwa urahisi, hivyo kuboresha uelewa wao wa kina. Upatikanaji wa rasilimali hizi unapanua uwezo wao wa kuchambua na kuelewa tafsiri mbalimbali za maandiko. Aidha Msafiri, Kangwa & Cai (2023) wanasema kwamba TEHAMA inawasaidia wanafunzi kufikia vifaa vya TEHAMA ambavyo vinaweza kufanikisha masomo yao.

> Another set of benefits can be presented under access to the learning process. Furthermore, the effective integration of ICT in the educative process gives learners better access to curriculum content and information. Throut ICT, students can access a wide range of literary resources online, including classic texts, contemporary works, and critical analyses. This can improve their learning outcomes. **Chanzo**: Msafiri, Kangwa & Cai (2023:4)

> Mchango mwingine wa TEHAMA ni ufikaji wa mchakato wa kujifunza. Zaidi ya hayo, ujumuishaji fasaha wa TEHAMA katika mchakato wa kielimu unawapa wanafunzi ufikiaji wa maudhui ya mitaala na taarifa. Kupitia TEHAMA, wanafunzi wanaweza kufikia rasilimali mbalimbali za fasihi mtandaoni, ikiwa ni pamoja na maandiko ya kienezi, kazi za kisasa, na uchambuzi wa kitaaluma. Hii inaweza kuboresha matokeo yao ya kujifunza (TY)

Dondoo hili linaonesha kwamba mchango wa TEHAMA ni mkubwa katika kuboresha ufikaji wa maudhui ya mitaala na taarifa kwa wanafunzi. Kupitia TEHAMA, wanafunzi wanapata fursa ya kufikia rasilimali za fasihi mbalimbali mtandaoni, ambazo zinaweza kuimarisha matokeo yao ya kujifunza. Zaidi ya hayo, matokeo ya utafiti kutoka kwa washiriki wa utafiti kwamba TEHAMA ina mchango mkubwa katika ufundishaji wa fasihi andishi katika shule za sekondari teule wilayani Nyagatare. Kwanza, matokeo husika yameonesha kwamba TEHAMA inaleta urahisi katika upatikanaji wa nyenzo kama vitabu vya kielektroniki na video za ufafanuzi kama ilivyoelezwa na Mwalimu J Katika dondoo lifuatalo:

> TEHAMA imeleta urahisi katika upatikanaji wa nyenzo za fasihi, kama vile vitabu vya kielektroniki na video za ufafanuzi wa kazi za fasihi. Kwa kutumia vitabu vya kielektroniki, wanafunzi wanaweza kusoma kazi za fasihi popote na wakati wowote. Aidha, video za ufafanuzi zinawasaidia wanafunzi kuelewa kwa

> undani na kwa njia ya picha na sauti, jambo ambalo linaboresha ufahamu wao wa mada husika. TEHAMA hii pia imepunguza gharama za kununua vitabu vya kawaida na kurahisisha usambazaji wa nyenzo za kufundishia fasihi andishi. **Chanzo**: Data za Msingi (2024).

Mwalimu J anadhihirisha kwamba TEHAMA inasaidia kutoa nyenzo zinazoweza kufikiwa kwa urahisi na haraka, hivyo kurahisisha maandalizi na ufundishaji wa somo la fasihi. Ingawa, taarifa zinabainisha kwamba TEHAMA inasaidia wanafunzi kufikia maandiko ya fasihi na vyanzo vingine vya maarifa kwa urahisi, data za ushuhudiaji zimebainisha kwamba katika shule teule wilayani Nyagatare, walimu wanalazimika kufanya kazi na kompyuta chache na vifaa vingine vya teknolojia ambavyo havitoshelezi mahitaji ya wanafunzi. Hali ilionekana kwamba inapunguza mchango wa TEHAMA katika ufundishaji wa fasihi andishi katika shule teule. Hapo chini ni baadhi ya data kutoka kwa baadhi ya walimu wa Kiswahili katika shule teule wilaya ni Nyagatare. Mwalimu B alitoa tarifa katika dondoo lifuatalo:

> Changamoto kubwa ninayokabiliana nayo ninapofundisha fasihi kwa kutumia TEHAMA ni ukosefu wa vifaa vya kutosha. Hatuna kompyuta za kutosha wala vifaa vingine vya kiteknolojia vinavyohitajika kwa ajili ya kufundisha. Hii inafanya kuwa vigumu kutumia TEHAMA kikamilifu darasani. **Chanzo**: Data za Msingi (2024)

Kutokana na mwalimu B, changamoto anazokabiliana nazo anapofundisha fasihi kwa kutumia TEHAMA ni ukosefu wa vifaa vya kutosha. Mwalimu alisema kwamba hakuna kompyuta za kutosha wala vifaa vingine vya kiteknolojia vinavyohitajika kwa ajili ya kufundisha, hali inayoathiri vibaya matumizi ya TEHAMA kikamilifu darasani.

Aidha, changamoto ya uhaba wa zana za TEHAMA ilithibitishwa na dondoo la hapo chini ambalo linaonesha taarifa zilizotolewa na Kiongozi wa Masomo E.

> Changamoto anazokabiliana nazo mwalimu wa Kiswahili anapofundisha fasihi kupitia matumizi ya TEHAMA uchache wa kompyuta na ukosefu wa mtandao wa intaneti wenye kasi na wa uhakika. Hii inamaanisha kuwa hata kama tunavyo vifaa vya TEHAMA, tunashindwa kutumia rasilimali mbalimbali za mtandaoni ambazo zinaweza kusaidia walimu katika ufundishaji wa fasihi andishi. **Chanzo**: Data za Msingi (2024)

Mtoa taarifa huyu anaonesha kwamba, changamoto anazokabiliana nazo mwalimu wa Kiswahili anapofundisha fasihi andishi kupitia matumizi ya TEHAMA ni uhaba wa kompyuta na ukosefu wa mtandao wa intaneti unaofanya kazi vizuri. Hii inamaanisha kuwa, hata kama shule ina

baadhi ya vifaa vya TEHAMA, walimu wanashindwa kutumia rasilimali mbalimbali za mtandaoni ambazo zinaweza kusaidia katika ufundishaji wa fasihi andishi. Mtandao wa intaneti usio imara na vifaa vichache vya TEHAMA vinawazuia walimu kufikia na kutumia taarifa na nyenzo muhimu zinazopatikana mtandaoni, hivyo kuathiri ufanisi wa ufundishaji wao.

Katika ushuhudiaji, ilionekana kuwa walimu walikuwa wakihusisha vifaa vya TEHAMA katika maandalizi ya masomo yao, lakini walipofika katika hatua ya ufundishaji, mara nyingi hawakuvitumia vifaa hivyo. Hii ilionekana kuwa ni kutokana na changamoto ya uhaba vifaa vya TEHAMA kama vile projekta na kompyuta zenye mtandao wa intaneti. Kwa mfano, katika darasa moja lililoshuhudiwa, mwalimu alijaribu kufundisha tamthilia kwa kutumia filamu. Ingawa chumba cha darasa kilikuwa na kompyuta nyingi, tu tano kati ya hizo zilikuwa na mtandao wa intaneti. Ukosefu wa projekta, ambayo ingewezesha mwalimu kuonesha filamu kwa wanafunzi wote kwa wakati mmoja, ulisababisha mwalimu kutumia uwasilishaji mhadhara ambazo hazikuwa na ufanisi mkubwa katika kufundisha somo hilo.

Kulingana na Sharma (2021), changamoto za ufundishaji wa fasihi kwa kutumia TEHAMA ni ukosefu wa ujuzi wa kidijiti wa kuingiza TEHAMA katika ujifunzaji wa fasihi, ukosefu wa miundombinu imara ya mtandao wa intaneti, na uhaba wa vifaa vya TEHAMA. Katika muktadha huu, ambapo ukosefu wa zana za TEHAMA ni changamoto kubwa, walimu wanakumbana na upungufu wa vifaa muhimu vya kufundishia.

Hata hivyo, ni muhimu kwa walimu kutumia vifaa vinavyopatikana shuleni ingawa kuna pahali ambapo ni vichache kwa ufanisi ili kuhakikisha kwamba wanafunzi wanapata manufaa ya TEHAMA katika ufundishaji. Mhimili wa kwanza wa mchakato wa kujifunza unasisitiza umuhimu wa ushirikiano kati ya wanafunzi kwa kutumia mawazo yao, kanuni, na taarifa kwa njia inayofaa. Hivyo, hata katika mazingira yenye ukosefu wa vifaa vya TEHAMA, walimu wanapaswa kutafuta njia mbadala za kutumia vifaa vichache walivyonavyo ili kuboresha ubora wa ufundishaji na kujifunza.

### 4.1.2 TEHAMA Inawaunganisha Wanafunzi wa Fasihi na Wanafunzi Wengine

Ili ufundishaji wa fasihi andishi ufanikiwe zaidi, ni muhimu kwamba wanafunzi wapate maarifa kuhusu tamaduni tofauti. Wakati wa ufundishaji, wanafunzi wanahitaji kuungana na watu kutoka

jamii na tamaduni mbalimbali. Hii ni kwa sababu maarifa ya tamaduni tofauti husaidia wanafunzi kuelewa muktadha wa kazi za fasihi na kuboresha uelewa wao wa maadili na mitindo ya maisha yaliyoonyeshwa kwenye maandiko (Kramsch, 1998). Kuungana na watu wa tamaduni tofauti kunapanua upeo wa wanafunzi na kukuza uwezo wao wa kuchambua na kufasiri kazi za fasihi kwa ufanisi zaidi (Byram 1997). Matokeo ya utafiti kutoka matini tulizochambua, yameonesha kwamba TEHAMA inawaunganisha wanafunzi na wanafunzi wengine duniani kote kupitia majukwaa ya ushirikiano na mitandao ya kijamii. Hii ni muhimu katika kufundisha na kujifunza fasihi kwa sababu inawapa wanafunzi fursa ya kubadilishana mawazo, kuunda mtandao wa kujifunza pamoja. Jambo hili linawasaidia wanafunzi kupanua mtazamo wao kuhusu maandiko ya fasihi kwa kutumia maoni na uzoefu wa watu kutoka tamaduni mbalimbali. Mchango huu unathibitishwa na dondoo hili:

> Other benefits of using ICT include active student participation in online discussions, assignments, and reading. ICT also allows students to connect with peers globally through collaborative platforms and social media. They can use popular creative platforms often employed in literature teaching. **Chanzo**: Alfaruque, Sultana, Rastogi, & Jabeen (2022:278).
>
> Faida nyingine za kutumia TEHAMA ni ushiriki wa wanafunzi katika majadiliano ya mtandaoni, kazi za nyumbani na kusoma. TEHAMA pia inawawezesha wanafunzi kuungana na wenzao duniani kote kupitia majukwaa ya ushirikiano na mitandao ya kijamii. Wanaweza kutumia majukwaa ya ubunifu ambayo ni maarufu na yanayotumika katika kufundisha fasihi. (TY)

Kulingana na dondoo hili, matumizi ya TEHAMA yana faida nyingi katika elimu, ikiwa ni pamoja na kuwashirikisha wanafunzi katika majadiliano ya mtandaoni, kazi za nyumbani, na kusoma. TEHAMA pia husaidia wanafunzi kuungana na wenzao kutoka sehemu mbalimbali duniani kupitia majukwaa ya ushirikiano na mitandao ya kijamii. Pia, wanafunzi wanapata fursa ya kutumia majukwaa ya ubunifu yanayotumiwa sana katika kufundisha fasihi. Aidha, mchango huu umebainishwa na mwalimu B katika dondoo lifuatalo:

> Kama mwalimu wa Kiswahili, ninaona kwamba TEHAMA ina mchango mkubwa katika ufundishaji wa fasihi andishi ya Kiswahili. Kupitia vifaa vya TEHAMA kama vile kompyuta na mitandao ya kijamii, wanafunzi wanaweza kuwasiliana na wenzao na walimu kwa urahisi zaidi. Hii inawapa fursa ya kujadili na kuchangia maarifa muhimu kuhusu kazi za fasihi. **Chanzo**: Data za Masingi (2024)

Dondoo la mtoataarifa huyu linaonesha kwamba, TEHAMA ina mchango mkubwa katika ufundishaji wa fasihi andishi ya Kiswahili. Matumizi ya vifaa kama vile kompyuta na mitandao ya kijamii yanawawezesha wanafunzi kuwasiliana kwa urahisi na wenzao na walimu, hivyo kuwapa nafasi ya kujadili na kushirikiana maarifa muhimu kuhusu kazi za fasihi. Aidha, mhimili wa kwanza wa Nadharia ya Uunganisho unaonesha kwamba katika mchakato wa kujifunza, wanafunzi wanapaswa kushirikiana kwa kutumia mawazo yao, kanuni na taarifa za jumla kwa njia inayofaa. Kwa hiyo, matokeo ya utafiti wetu yanaonesha kwamba TEHAMA inawaunganisha wanafunzi wa fasihi andishi na wanafunzi wengine wanaojifunza fasihi andishi duniani kote.

Licha ya haya, data za zimebainisha kwamba katika shule za sekondari teule wilayani Nyagatare, kuna baadhi ya walimu ambao hawajafanikiwa kutumia TEHAMA katika ufundishaji wa fasihi andishi kwa kuwaunganisha wanafunzi wao na wanafunzi wengine duniani. Hii ni kwa sababu, data ushuhudiaji zimeonesha kwamba kuna badhi ya walimu ambao hawana ujuzi wa kutosha kuhusu namna ya kutumia TEHAMA katika ufundishaji wa fasihi andishi. Changamoto hii ilibainishwa Mwalimu E katika dondoo hili:

> Changamoto ambayo ninakabiliana nayo ninapofundisha fasihi andishi kwa kutumia TEHAMA ni ukosefu wa ujuzi na maarifa kuhusu jinsi ya kutumia TEHAMA katika ufundishaji wa fasihi. Ingawa tuna vifaa vichache, sisi walimu hatujapewa mafunzo ya kutosha kuhusu jinsi ya kutumia vifaa hivi kwa ufanisi katika masomo ya fasihi andishi. Changamoto hii inatuathiri tunapofundisha fasihi andishi kwa kutumia TEHAMA. **Chanzo**: Data za Msingi (2024)

Kutokana na mwalimu huyu, changamoto ni ukosefu wa ujuzi na maarifa kuhusu jinsi ya kutumia TEHAMA katika ufundishaji wa fasihi. Ingawa kuna vifaa vichache vilivyopo, walimu wa Kiswahili hawajapewa mafunzo ya kutosha kuhusu jinsi ya kutumia vifaa hivyo kwa ufanisi katika ufundishaji na ujifunzaji wa masomo ya fasihi andishi.

Hii inaonesha kwamba, kuna baadhi walimu wa Kiswahili ambao bado hawana ujuzi wa kutosha wa kutumia TEHAMA ili kuwaunganisha wanafunzi wao na wanafunzi wengine. Matokeo haya yanaungwa mkono na Sharma (2021), anaonesha kwamba changamoto za ufundishaji wa fasihi kwa kutumia TEHAMA ni ukosefu wa ujuzi wa kidijiti wa kuingiza TEHAMA katika ujifunzaji wa fasihi. Kwa kuepukana na changamoto hii, walimu wanapaswa kushiriki katika warsha za

mara kwa mara kuhusu matumizi ya TEHAMA na kutumia rasilimali za mtandaoni kama video na makala.

### 4.1.3 TEHAMA Inawasaidia Wanafunzi Kukuza Stadi Muhimu Zinazohitajika katika Masomo ya Fasihi Andishi

Ufundishaji na ujifunzaji wa fasihi ni mchakato unaohitaji wanafunzi kuwa na stadi muhimu za mawasiliano ambazo ni kusikiliza, wakati wa kusikiliza masimulizi, kuangalia filamu kwa kutumia mtandao, kusema hivi hujitokeza wakati wa mazungumzo wanapo asilisha, kusoma hivihujitokeza wakati wa kuzoma maandishi na kuandika wakifanta mtihani au jaribio kwa kutumia vifaa vya elekitroniki kama kompyuta, kwa kuwawezesha kuelewa somo la fasihi (Mosha, 2017). Hii ni kwa sababu stadi hizo zinawasaidia wanafunzi kuchambua, kuelewa na kufikia dhana na maudhui yaliyomo katika kazi za fasihi.

Kwa hiyo, katika utafiti wetu, tumeona kwamba TEHAMA ina mchango mkubwa katika kukuza stadi muhimu zinazohitajika katika masomo ya fasihi andishi miongoni mwa wanafunzi wa shule za sekondari teule wilayani Nyagatare. Kupitia vifaa vya TEHAMA kama vile kompyuta, mitandao ya kijamii na programu mbalimbali za kielimu, wanafunzi wanaweza kujifunza kwa njia shirikishi na kukuza stadi muhimu za kuboresha uelewa wao wa masomo ya fasihi. Hii inathibitishwa na dondoo lifuatalo:

> Integrating ICT with literature in language teaching enhances creativity by allowing students to connect literary texts with their own experiences. This approach fosters a deeper engagement with the material, enabling students to explore and express their personal interpretations of the literature. **Chanzo**: Demiröz (2019:66).
>
> Kujumuisha TEHAMA na fasihi katika ufundishaji wa lugha kunakuza ubunifu kwa kuruhusu wanafunzi kuunganisha maandiko ya fasihi na uzoefu wao wa kibinafsi. Mbinu hii inachochea ushirikiano wa kina na nyenzo, ikiwapa wanafunzi fursa ya kuchunguza na kueleza tafsiri zao za kibinafsi za fasihi. (TY)

Kulingana na dondoo hili, kujumuisha TEHAMA na fasihi katika ufundishaji wa lugha kunasaidia wanafunzi kuwa wabunifu kwa kuunganisha maandiko na uzoefu wao wa maisha. Mbinu hii inawawezesha wanafunzi kuhusisha mada za fasihi na maisha yao wenyewe, hivyo

kuongeza uhusiano wao na nyenzo za kujifunza. Matini nyingine tuliyichambua ilitoa taarifa za hapo chini:

> Technology-enhanced literature classrooms help students develop a range of new literacy skills, such as decoding colors, interpreting icons, and understanding images. Students can also experiment with hyperlinks, digital documents, and audio-video recordings, which positively impact their communication and learning outcomes. Additionally, participating in chat rooms or other asynchronous computer-mediated discussions introduces students to new methods of language literature learning, further enriching their educational experience. **Chanzo**: Alfaruque, Sultana, Rastogi & Jabeen (2022:279)

> Madarasa ya fasihi yanayotumia TEHAMA yanawasaidia wanafunzi kukuza stadi mpya za ujifunzaji, kama vile kutafsiri rangi, kuelewa alama na picha. Wanafunzi wanaweza pia kujaribu viungo vya mtandao, hati za kidijiti na rekodi za sauti na video, ambazo zina athari chanya kwenye mawasiliano yao na matokeo ya kujifunza. Aidha, kushiriki katika vyumba vya mazungumzo au majadiliano mengine ya mtandaoni yasiyo ya wakati halisi kunawasaidia wanafunzi kugundua mbinu mpya za kujifunza fasihi, na kuboresha uzoefu wao wa kielimu. (TY)

Dondoo hili linaonesha kwamba madarasa ya fasihi yanayotumia TEHAMA yanawawezesha wanafunzi kukuza stadi mpya za ujifunzaji kama vile kutafsiri rangi na kuelewa alama na picha. Pia, kupitia viungo vya mtandao, rekodi za sauti na video, wanafunzi wanaboresha mawasiliano na matokeo ya kujifunza, na kushiriki katika majadiliano ya mtandaoni kunawasaidia kugundua mbinu mpya za kujifunza fasihi. Zaidi ya hayo, data za usaili zimeonesha kwamba TEHAMA inawasaidia wanafunzi kujifunza kwa kujitegemea na kukuza stadi tofauti ikiwemo ubunifu. Hili limethibitishwa na Mkurugenzi D kwenye dondoo lifuatalo:

> TEHAMA inawezesha urahisi wa kujifunza kwa kujitegemea, ambapo wanafunzi wanaweza kutumia vifaa vya teknolojia kufanya utafiti na kujifunza zaidi kuhusu kazi za fasihi hata nje ya darasa. Jambo hili hukuza ubunifu wa wanafunzi katika masomo ya fasihi. Kupitia TEHAMA, mwanafunzi anaweza kutumia kompyuta au simu kutafuta tafsiri, uchambuzi na historia ya kazi za fasihi kwa kina. Hii inawapa wanafunzi nafasi ya kupanua maarifa yao na kujifunza kwa mtindo unaowapendeza. (TY) **Chanzo**: Data za Msingi (2024).

Dondoo hili linaonesha kwamba vifaa vya TEHAMA vinawezesha wanafunzi kujifunza kwa kujitegemea na kukuza ubunifu wao. Vifaa kama vile kompyuta na simu za kisasa vinawapa wanafunzi fursa ya kupata taarifa na rasilimali nyingi za mtandaoni kuhusu kazi za fasihi bila kutegemea walimu. Hivyo basi, matokeo ya utafiti wetu yanaonesha kwamba TEHAMA ina mchango mkubwa katika ufundishaji wa fasihi andishi kwa kukuza stadi mpya za ujifunzaji. Pia,

inasaidia wanafunzi kujifunza kwa kujitegemea na kukuza ubunifu wao kwa kutumia vifaa vya teknolojia kufanya utafiti na kupata taarifa za kina kuhusu kazi za fasihi andishi.

### 4.1.4 TEHAMA Inawapa Wanafunzi Motisha ya Kujifunza Fasihi Andishi

Motisha ni jambo muhimu katika ujifunzaji wa somo lolote lile kwani inawasaidia wanafunzi kuwa na nia na ari ya kujifunza zaidi na kwa bidii (Ryan & Deci, 2000). Tafiti zinaonesha kwamba wanafunzi wenye motisha wana uwezekano mkubwa wa kufanikiwa katika masomo yao na kupata uelewa wa kina wa masomo wanayojifunza (Schunk, Pintrich, & Meece, 2008). Katika utafiti wetu, tumeona kwamba mchango wa TEHAMA katika ufundishaji wa fasihi andishi katika shule za sekondari teule wilayani Nyagatare ni kuwapa wanafunzi motisha ya kujifunza fasihi andishi. Kwanza, data za uchanganuzi matini zimeonesha kwamba, TEHAMA inapotumiwa katika madarasa ya fasihi andishi, inawachochea wanafunzi na kuboresha ushiriki wao. Hii inachangia katika kuongeza ari yao ya kujifunza fasihi.

> By integrating ICT into teaching and learning literature, students find the process both entertaining and stress-free. This integration motivates students due to its innovative format, including visual elements, digital editions of classics, storytelling through videos, and interactive hypertexts. **Chanzo**: Alfaruque, Sultana, Rastogi & Jabeen (2022:279)

> Kwa kujumuisha TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji wa fasihi, wanafunzi wanapata mchakato huo kuwa wa kuvutia na usio na msongo. Ujumuishaji huu unawachochea wanafunzi kutokana na umbizo lake bunifu, ikiwa ni pamoja na vipengele vya kuona, matoleo ya kidijitali ya kazi za kienezi, usimulizi kupitia video, na maandiko shirikishi. (TY)

Kulingana na dondoo hili, TEHAMA inafanya ufundishaji na ujifunzaji wa fasihi kuwa wa kuvutia na usio na msongo kwa wanafunzi. Ujumuishaji wa teknolojia hii inachochea wanafunzi kwa kutumia vipengele bunifu kama vile vipengele vya kuona, matoleo ya kidijiti, video, na maandiko shirikishi. Kwa kuoongezea, Hattie (2009) anabainisha mchango wa TEHAMA katika ufundishaji wa fasihi andishi kwenye dondoo lifuatalo:

> ICT increases motivation among students of written literature by providing interactive and engaging learning tools that enhance their interest and participation. This approach helps students connect more deeply with literary content and promotes a more active learning environment. **Chanzo**: Hattie (2009:138)

> TEHAMA inachochea motisha miongoni mwa wanafunzi wa fasihi andishi kwa kutoa zana za kujifunzia zinazohusisha na kuvutia ambazo zinaongeza hamasa yao na ushiriki. Mbinu hii inawasaidia wanafunzi kuunganishwa kwa kina na maudhui ya fasihi na kuhamasisha mazingira ya kujifunza yenye shughuli nyingi. (TY)

Kulingana na dondoo hili, TEHAMA inachochea motisha kwa wanafunzi wa fasihi andishi kwa kutoa zana za kujifunzia zinazovutia na zinazowashirikisha. Hii inawasaidia kuunganishwa kwa kina na maudhui ya fasihi na kuboresha mazingira ya kujifunza kwa kuongeza shughuli na ushiriki. Zaidi ya hayo, data za usaili zimeonesha kwamba TEHAMA ina mchango wa kukuza motisha miongoni mwa wanafunzi wa fasihi andishi ya Kiswahili kwenye shule teule. Haya yanathibitishwa na Mwalimu B aliyetoa taarifa zinazopatikana kwenye dondoo lifuatalo:

> TEHAMA inawezesha urahisi wa kujifunza kwa kujitegemea, ambapo wanafunzi wanaweza kutumia vifaa vya teknolojia kufanya utafiti na kujifunza zaidi kuhusu kazi za fasihi hata nje ya darasa. Jambo hili hukuza ubunifu wa wanafunzi katika masomo ya fasihi. Kupitia TEHAMA, mwanafunzi anaweza kutumia kompyuta au simu kutafuta tafsiri, uchambuzi na historia ya kazi za fasihi kwa kina. Hii inawapa wanafunzi nafasi ya kupanua maarifa yao na kujifunza kwa mtindo unaowapendeza **Chanzo**: Data za Msingi (2024).

Dondoo hili linaonesha kwamba vifaa vya TEHAMA vinawezesha wanafunzi kujifunza kwa kujitegemea na kukuza ubunifu wao. Vifaa kama vile kompyuta na simu za kisasa vinawapa wanafunzi fursa ya kupata taarifa na rasilimali nyingi za mtandaoni kuhusu kazi za fasihi bila kutegemea walimu. Kwa mujibu wa Zainal (2012), ujumuishaji wa TEHAMA katika ufundishaji wa fasihi hutoa zana za mtandaoni kwa ajili ya masomo ya fasihi. Hii inaruhusu wanafunzi kufurahia kusoma fasihi mtandaoni na kuonesha ubunifu wao wa lugha na maadili ya kibinadamu kupitia njia za kisasa. Isitoshe, Kiongozi wa Masomo E alibainisha mchango wa TEHAMA katika ufundishaji wa fasihi andishi kwenye dondoo lifuatalo:

> Mchango wa TEHAMA katika ufundishaji na ujifunzaji wa fasihi ni kuwapa walimu mbinu mpya za kufundishia ambazo zina mafanikio zaidi kuliko mbinu za kijadi. Kwa kutumia teknolojia kama projekta, kompyuta, na vitabu vya kielektroniki, walimu wanaweza kufundisha kwa njia za kuvutia na zinazoboresha ufahamu wa wanafunzi. Vifaa hivi vinawezesha kuonesha picha, video, na sauti zinazohusiana na kazi za fasihi, hivyo kuongeza ushiriki wa wanafunzi darasani na kuwasaidia kuelewa kwa kina maudhui ya fasihi. Hii inafanya ufundishaji wa fasihi kuwa wa kisasa zaidi na wenye matokeo bora (T.Y.). **Chanzo**: Data za Msingi (2024).

Dondoo hili linaonesha kwamba TEHAMA inawapa walimu wa Kiswahili mbinu mpya na bora zaidi za kufundisha fasihi andishi kuliko mbinu za kijadi. Kwa kutumia vifaa kama projekta na kompyuta, walimu wanaweza kufundisha kwa njia za kuvutia. Hivyo, TEHAMA huwezesha matumizi ya mbinu za ufundishaji zinazoongeza ushiriki na ufahamu wa wanafunzi darasani. Kwa mujibu wa Warschauer & Healey (1998), matumizi ya TEHAMA husisimua wanafunzi na husaidia walimu kubadilisha njia zao za ufundishaji kwa kuzingatia maslahi ya wanafunzi kupitia zana za kufundishia na kujifunzia zinazotumia teknolojia.

Aidha, Demiröz (2019) anaonesha kwamba TEHAMA ina mchango katika ufundishaji na ujifunzaji wa fasihi kwa kuwa inawamotisha wanafunzi na kwafanya wapende somo la fasihi. Hivyo basi, matokeo ya utafiti uliofanyika yalionesha kwamba TEHAMA ina mchango wa kuongeza motisha ya wanafunzi katika ufundishaji wa fasihi andishi kwenye shule za sekondari wilayani Nyagatare. Matokeo haya yanahusiana na mhimili wa kwanza wa nadharia ya Uunganisho, ambayo inasisitiza umuhimu wa TEHAMA katika mchakato wa kujifunza.

**4.2 Miongozo ya Utumiaji wa TEHAMA katika Ufundishaji wa Fasihi Andishi ya Kiswahili**

Utafiti uliofanyika ulilenga kuunda miongozo ya utumiaji wa TEHAMA ili kuboresha ufundishaji wa fasihi andishi katika shule za sekondari wilayani Nyagatare, Rwanda. Miongozo iliyotolewa inajumuisha utumiaji wa projekta na sladi, usimulizi wa kidijiti na mitandao ya kijamii ili kufanikisha mchango wa TEHAMA katika ufundishaji wa fasihin andishi ya Kiswahili katika shule za sekondali wilayani Nyagatare.

**4.3.1 Mwongozo wa Utumiaji wa Projekta na Slaidi**

Matumizi ya projekta na slaidi katika ufundishaji wa masomo ya fasihi yanaleta urahisi kwa walimu katika kuwasilisha mada mbalimbali kwa wanafunzi wao. Mbali na hilo, kama ilivyodokezwa na Teana Jones na Patel (2018), projekta na slaidi husaidia kuongeza motisha ya wanafunzi kujifunza fasihi kwa kutoa ufahamu wa kina kupitia mbinu za kisasa za kufundishia. Walimu wanaweza kutumia slaidi kuonesha mifano mbalimbali ya kazi za fasihi kutoka vyanzo vya mtandaoni, kuwezesha muktadha wa kisasa na kuhamasisha mjadala wa kielimu kati ya wanafunzi. Kwa hiyo, matumizi ya projekta na slaidi ni muhimu katika kuboresha mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji wa fasihi andishi shuleni. Hivyo basi, utafiti ulioibua tasnifu hii ulitoa

mwongozo wa utumiaji wa projekta na slaidi katika ufundishaji wa fasihi andishi kwa Kiswahili katika shule za sekondari teule wilayani Nyagatare.

Kwanza, katika utekelezaji wa mbinu ya utumiaji wa projekta na slaidi, mwalimu anapaswa kuandaa maudhui ya fasihi andishi kwa umakini. Hii inajumuisha kusoma na kuchambua kazi za fasihi andishi anayofundisha na kuchagua sehemu muhimu za kuwasilisha kwa wanafunzi. Mwalimu anapaswa kuandaa slaidi zenye muhtasari wa sura muhimu, wahusika wakuu, mandhari, maudhui na mengine. Ni muhimu kujumuisha vielelezo kama picha za wahusika, ramani za maeneo yanayozungumziwa kwenye kazi za fasihi, na michoro inayosaidia kufafanua maudhui. Vilevile, mwalimu anaweza kuandaa maswali ya kujadili na shughuli za ushirikishaji ambazo wanafunzi watafanya wakati wa ufundishaji wa somo.

Pili, mwalimu anapaswa kuandaa vifaa vya kufundishia kama vile projekta, kompyuta na skrini ya kuonesha slaidi. Mwalimu anapaswa kuhakikisha kuwa vifaa hivi vinafanya kazi vizuri kabla ya kipindi kuanza. Ni muhimu pia kwa mwalimu kuwa na mpango wa dharura endapo vifaa vya TEHAMA vitapata tatizo lolote.

Kwa mfano, mwalimu anaweza kuwa na nakala za maudhui aliyoyaandaa katika karatasi ili wanafunzi waweze kuendelea na somo hata kama vifaa vya TEHAMA vitashindwa kufanya kazi. Mhimili wa pili wa Nadharia ya Uunganisho unasema kwamba matumizi ya TEHAMA katika mchakato wa kufundisha siyo bila kasoro. Kwa hiyo, wakati wa matumizi ya projekta na slaidi, ni lazima mwalimu awe tayari kutumia njia mbadala kama vifaa vya TEHAMA vitashindwa kufanya kazi.

Tatu, mwalimu anapaswa kuwasilisha slaidi darasani kwa kutumia projekta. Wakati wa kuonesha slaidi, mwalimu anapaswa kuelezea kwa kina kila sehemu inayowasilishwa na kutoa mifano inayoeleweka kwa wanafunzi. Mwalimu anaweza kutumia muda wa kutosha kwa kila slaidi ili kuhakikisha wanafunzi wanapata ufahamu kamili wa maudhui. Aidha, mwalimu anapaswa kuwauliza wanafunzi maswali ili kuhamasisha ushiriki wao na kuwafanya waelewe zaidi kile kinachofundishwa.

Nne, mwalimu anapaswa kukuza mjadala na ushirikiano miongoni mwa wanafunzi kwa kutumia slaidi. Kwa mfano, baada ya kuwasilisha sehemu muhimu za kazi ya fasihi andishi, mwalimu

anaweza kugawa wanafunzi katika makundi madogo ili kujadili maswali maalum yanayohusiana na kazi ya fasihi andishi. Hapa, mwalimu anaweza kutumia slaidi kuonesha maswali ya kujadili na kuelekeza wanafunzi katika michakato ya mjadala. Hii itasaidia wanafunzi kuelewa maudhui kwa kina na kushiriki mawazo yao na wenzao.

Mwisho, mwalimu anapaswa kufanya tathmini ya ufahamu wa wanafunzi kwa kutumia slaidi. Mwalimu anaweza kuandaa maswali ya mtihani au shughuli za darasani zinazohusiana na kazi ya fasihi inayoshughulikiwa na kuzionesha kwa wanafunzi kupitia projekta. Aidha, mwalimu anaweza kutumia mifano ya maswali ya kuchagua na kujibu au maswali ya kujadili ili kuona jinsi wanafunzi wameelewa maudhui ya kazi ya fasihi andishi inayoshughulikiwa. Tathmini hii itasaidia mwalimu kuelewa maeneo ambayo wanafunzi wanahitaji msaada zaidi na kupanga mikakati ya kuboresha ufundishaji. Kwa kuzingatia hatua hizi, mwalimu anaweza kutumia projekta na slaidi kwa ufanisi katika kufundisha fasihi andishi na kuboresha ufahamu wa wanafunzi wake katika somo hili muhimu.

### 4.3.2 Mwongozo wa Utumiaji wa Usimulizi wa Kidijiti

Usimulizi wa kidijiti ni mbinu bora inayoweza kuwa na manufaa katika mchakato wa ufundishaji wa fasihi andishi ya Kiswahili katika shule za sekondari wilayani Nyagatare. Kulingana na Karantalis & Koukopoulos (2022), utumiaji wa usimulizi wa kidijiti unaweza kufanikisha zaidi ufundishaji wa fasihi kupitia TEHAMA kwa kuruhusu matumizi ya picha, video, sauti na maandishi kwa pamoja, hivyo kuifanya fasihi iwe hai na kuvutia zaidi kwa wanafunzi. Mbinu hii inachochea ubunifu na hufanya masomo kuwa ya kuvutia na yanayohusiana na maisha ya kila siku ya wanafunzi (Prensky, 2001).

Hivyo basi, utafiti uliofanyika umejiegemeza katika mhimili wa pili wa Nadharia ya Uunganisho unosisitizia uangalifu katika matumizi ya TEHAMA na kutoa mwongozo wa utumiaji wa usimulizi wa kidijiti katika ufundishaji wa fasihi andishi kwa Kiswahili katika shule za sekondari teule wilayani Nyagatare. Mwongozo huo unaelekeza jinsi ya kutumia usimulizi wa kidijiti, huku ikizingatia tathmini ya kibinafsi ili kuepuka vikwazo vinavyoweza kuathiri mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji.

Kwanza, katika utekelezaji wa utumiaji wa mbinu hii, mwalimu anapaswa kuandaa maudhui ya kidijiti kwa uangalifu. Hii inajumuisha kuchagua kazi za fasihi ambazo zinafaa kwa usimulizi wa

kidijiti, kama vile riwaya, hadithi fupi andishi au mashairi. Mwalimu anapaswa kuandaa maandishi ya kazi hizi kwa kutumia programu za kuhariri maandishi. Pia, ni muhimu kuchagua picha, video, na sauti zinazofaa ambazo zinaweza kuboresha usimulizi wa kidijiti. Mwalimu anaweza kutumia programu mbalimbali za kuunda hadithi za kidijiti kama slidi, prezi au programu nyingine za usimulizi wa hadithi.

Pili, mwalimu anapaswa kuunda usimulizi wa kidijiti kwa kuunganisha maandishi, picha, video na sauti katika programu alizochagua. Kwa mfano, mwalimu anaweza kuchagua kipande cha riwaya na kukiwasilisha kwa njia ya sauti huku akionesha picha zinazohusiana na kipande hicho. Vilevile, mwalimu anaweza kuingiza video fupi zinazoonesha mandhari au matukio muhimu katika riwaya. Ni muhimu kwa mwalimu kuhakikisha kuwa usimulizi una mtiririko mzuri na unavutia ili kuwafanya wanafunzi waweze kufuatilia kwa urahisi.

Tatu, mwalimu anapaswa kuwasilisha usimulizi wa kidijiti darasani kwa kutumia vifaa vya TEHAMA kama projekta na kompyuta. Wakati wa uwasilishaji, mwalimu anapaswa kuelezea kila sehemu ya usimulizi kwa kina na kuhakikisha kuwa wanafunzi wanaelewa maudhui yanayowasilishwa. Pia, mwalimu anaweza kuwauliza wanafunzi maswali ya kuhamasisha majadiliano na ushirikiano kuhusu usimulizi huo. Hii itasaidia wanafunzi kuelewa vizuri maudhui ya fasihi na kuhusisha masomo na maisha yao ya kila siku.

Nne, mwalimu anapaswa kutumia usimulizi wa kidijiti kama chombo cha kukuza mjadala na ushirikiano miongoni mwa wanafunzi. Baada ya kuwasilisha usimulizi, mwalimu anaweza kugawa wanafunzi katika makundi madogo ili kujadili maswali maalum yanayohusiana na maudhui ya usimulizi. Mwalimu anaweza kutumia picha, video, na sauti kutoka usimulizi wa kidijiti kama vielelezo vya kuchochea mjadala. Hii itasaidia wanafunzi kuelewa maudhui kwa undani zaidi na kushiriki mawazo yao na wenzao.

Mwisho, mwalimu anapaswa kufanya tathmini ya kibinafsi na ya wanafunzi ili kuepuka vikwazo vinavyoweza kuathiri mchakato wa ufundishaji na ujifunzaji. Mwalimu anaweza kutumia maswali ya tathmini ili kuona jinsi wanafunzi walivyoelewa maudhui ya usimulizi wa kidijiti. Pia, mwalimu anapaswa kujitathmini kwa kuangalia jinsi alivyoandaa na kuwasilisha usimulizi wa kidijiti na kuboresha pale panapohitajika. Hii itasaidia mwalimu kuboresha mbinu za ufundishaji na kuhakikisha kuwa wanafunzi wanapata ufahamu wa kina wa fasihi andishi. Kwa

kuzingatia hatua hizi, mwalimu anaweza kutumia usimulizi wa kidijiti kwa ufanisi katika kufundisha fasihi andishi na kuboresha ufahamu na ushiriki wa wanafunzi wake katika somo la fasihi andishi.

### 4.3.3 Mwongozo wa Utumiaji wa Mitandao ya Kijamii

Katika enzi hizi za kidijiti, mitandao ya kijamii inatumika na watu wengi, hasa vijana (Haidari, Katawazai & Mohd Yusof, 2020). Kwa hiyo, matumizi ya mitandao hii inaonekana kuwa bora sana katika ufundishaji wa fasihi andishi ya Kiswahili katika shule za sekondari wilayani Nyagatre.

Kama inavyooneshwa na Reinhardt (2019), walimu wa fasihi wanaweza kutumia mitandao ya kijamii ili kufundisha masomo ya fasihi. Hii ni kwa sababu mitandao ya kijamii inaruhusu walimu kushiriki rasilimali za kifasihi kwa urahisi, kuanzisha mijadala yenye maana, na kuunda mazingira ya kujifunzia yenye ushirikiano zaidi.

Licha ya haya, mitandao ya kijamii inaweza kuleta athari mbaya katika ufundishaji na ujifunzaji wa fasihi andishi kama haitumiwi vizuri. Hii ni kwa kuwa matumizi mabaya ya mitandao ya kijamii yanaweza kusababisha usumbufu kwa wanafunzi, kupunguza umakini katika masomo, na hata kusababisha matatizo ya kimaadili na kisaikolojia.

Kutokana na mhimili wa pili wa nadharia ya uunganisho, TEHAMA inaweza kusababisha vikwazo kwa malengo ya ufundishaji na ujifunzaji, na hata kuleta madhara kwa wanafunzi, walimu na jamii kwa ujumla katika maisha yao ya kila siku (Munyengabire, 2023). Kwa hiyo, walimu wa fasihi wanalazimika kuhakikisha kuwa mitandao ya kijamii inatumiwa vizuri kwa lengo la kuboresha ufundishaji na ujifunzaji wa fasihi andishi. Hivyo basi, utafiti uliofanyika umetoa mwongozo wa utumiaji wa mitandao ya kijamii katika ufundishaji wa fasihi andishi katika shule za sekondari teule wilayani Nyagatare. Mwongozo huu unaelekeza jinsi walimu wanavyoweza kutumia mitandao ya kijamii kwa ufanisi, huku wakizingatia mbinu bora za kudhibiti athari mbaya zinazoweza kujitokeza.

Kwa kutekeleza utumiaji wa mbinu hii, hatua ya kwanza ni uchaguzi wa mtandao wa kijamii. Katika hatua hii, mwalimu anapaswa kuchagua jukwaa la kijamii linalofaa kwa ufundishaji wa fasihi andishi. Majukwaa maarufu kama Facebook, WhatsApp, Instagram, Twitter na YouTube

yanaweza kutumiwa kulingana na mahitaji na upatikanaji kwa wanafunzi. Mwalimu anapaswa kuchagua jukwaa ambalo linaweza kuruhusu ufundishaji wa maudhui mbalimbali ya fasihi andishi. Kwa mfano, Facebook inaweza kutumika kuunda makundi ya majadiliano, wakati YouTube inaweza kutumika kwa kushiriki mihadhara ya video.

Hatua ya pili ni kuunda akaunti au kundi katika mjawapo ya mitandao ya kijamii. Kwa hatua hii, mwalimu anapaswa kuunda akaunti au kundi maalum la darasa kwenye jukwaa lililochaguliwa. Katika kundi hili, wanafunzi wote wataweza kujiunga na kushiriki katika shughuli za masomo. Ni muhimu mwalimu kuweka sheria na kanuni za matumizi ya kundi hilo ili kuhakikisha nidhamu na matumizi mazuri ya jukwaa.

Kwa mfano, mwalimu anaweza kuunda kundi la WhatsApp au la facebook kwa ajili ya darasa lake la fasihi ambapo wanafunzi watakuwa wanajadili mada za kifasihi kila wiki. Hapa, kundi la facebook linaweza kuwa bora zaidi kwa wanafunzi wa shule za sekondari kwa kuwa halihitaji matumizi ya simu.

Hatua ya tatu ni kutumia maudhui ya kifasihi. Hapa, mwalimu anapaswa kuanza kuwapa wanafunzi maudhui ya kifasihi mara kwa mara kwenye jukwaa la kijamii. Hii inaweza kujumuisha kutoa vipande vya maandishi ya fasihi, video zinazohusiana na mada za kifasihi, picha zinazosaidia kufafanua maudhui na viungo vya makala au vitabu vya kifasihi. Mwalimu anaweza pia kutumia podikasti zinazozungumzia fasihi na kuwahimiza wanafunzi kusikiliza na kutoa maoni yao. Mfano, mwalimu anaweza kupakia video ya uchambuzi wa riwaya maarufu kwenye YouTube na kuwataka wanafunzi kuitazama na kujadili.

Hatua ya nne ni kuendeleza mjadala na ushirikiano. Hapa, mwalimu anapaswa kutumia jukwaa hilo kukuza mjadala na ushirikiano kati ya wanafunzi. Mwalimu anaweza kuanzisha mijadala kuhusu mada mbalimbali za kifasihi, kuwauliza wanafunzi kutoa maoni yao, na kuwahimiza kujadili mawazo yao na wenzao. Kwa mfano, mwalimu anaweza kuuliza swali kuhusu wahusika wakuu katika riwaya fulani na kuwahimiza wanafunzi kujadili tabia na matendo ya wahusika hao katika kundi la Facebook au WhatsApp.

Hatua ya tano ni kufanya tathmini na kutoa maoni. Hapa, mwalimu anapaswa kufanya tathmini ya ufahamu wa wanafunzi na kutoa maoni kupitia jukwaa la kijamii. Hii inaweza kujumuisha

kuendesha tafiti fupi za mtandaoni, kuuliza maswali ya kuchagua na kuandaa tafakari za kifupi kuhusu maudhui yaliyofundishwa. Mwalimu anaweza pia kutoa maoni ya kujenga kwa wanafunzi kuhusu michango yao kwenye mijadala na shughuli za kifasihi. Kwa mfano, mwalimu anaweza kuandaa tafiti fupi za mtandaoni kupitia fomu za Google na kuwataka wanafunzi kujaza baada ya kila somo ili kupima uelewa wao. Kwa kufuata mwongozo huu, walimu wanaweza kutumia mitandao ya kijamii kwa ufanisi katika kufundisha fasihi andishi.

### 4.4 Muhtasari wa Sura ya Nne

Sura hii imechambua kwa undani jinsi matokeo ya utafiti yanavyowasilishwa na kujadiliwa. Inagawanywa katika sehemu kuu tano: utangulizi, lengo mahususi la kwanza, lengo mahususi la pili. Sehemu ya nne ni muhtasari wa sura ya nne.

# SURA YA TANO: MUHTASARI WA MATOKEO YA UTAFITI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

## 5.1 Utangulizi

Sura ya tano inazingatia mambo muhimu matano. Mambo hayo ni utangulizi, muhtasari, ufafanuzi wa nadharia ya utafiti iliyotumika, hitimisho, pamoja na mapendekezo ya utafiti.

## 5.2 Muhtasari wa Matokeo ya Utafiti

Utafiti uliofanyika ulikuwa na malengo mahususi mawili: kubainisha mchango wa TEHAMA katika ufundishaji wa fasihi andishi katika shule za sekondari Wilayani Nyagatare nchini Rwanda nakuunda miongozo ya utumiaji wa TEHAMA katika ufundishaji wa fasihi andishi katika shule za sekondari wilayani Nyagatare nchini Rwanda. Kwa hiyo, sehemu hii inatoa muhtasari wa matokeo ya utafiti kwa kuegemea katika malengo mahususi hayo.

### 5.2.1 Lengo Mahususi la Kwanza

Lengo mahususi la kwanza katika utafiti lilikuwa kubainisha mchango wa TEHAMA katika ufundishaji wa fasihi andishi katika shule za sekondari Wilayani Nyagatare nchini Rwanda. Utafiti umeonesha kuwa TEHAMA ina mchango mkubwa katika kuboresha ufundishaji wa fasihi andishi kwa kutumia teknolojia ya kisasa. Hii inajumuisha upatikanaji rahisi wa nyenzo kama vitabu vya kielektroniki na video za ufafanuzi, ambazo zinasaidia wanafunzi kuelewa na kufurahia maudhui ya fasihi andishi kwa undani zaidi.

Pili, utafiti umebaini kwamba TEHAMA inachangia pakubwa katika kuwaunganisha wanafunzi wa fasihi andishi na wenzao kutoka sehemu mbalimbali za dunia. Hii inawapa fursa ya kubadilishana mawazo, kujadili mawazo na mitindo mbalimbali ya fasihi, na hivyo kuongeza uelewa wao na ari ya kujifunza. Kuunganishwa kwa mtandao kunachangia katika kuongeza mwingiliano na ushirikiano katika masomo ya fasihi.

Tatu, matumizi ya TEHAMA yanawezesha wanafunzi kujifunza stadi mpya zinazohitajika katika masomo ya fasihi andishi. Teknolojia kama vile programu za elimu na vyanzo vya habari vya mtandaoni vinawawezesha wanafunzi kupanua maarifa yao na kujifunza mbinu za kisasa zinazohitajika katika uchambuzi wa fasihi. Hii inachangia katika kuimarisha ujuzi wao wa kitaaluma na vitendo.

Mwisho, TEHAMA ina athari chanya katika kufanya ufundishaji wa fasihi andishi kuwa wa kuvutia zaidi. Kwa kutumia zana za za TEHAMA, wanafunzi wanapata uzoefu wa kujifunza ambao ni wa kuvutia na wenye shughuli nyingi, hivyo kuboresha motisha yao na kufanya mchakato wa kujifunza kuwa wa kupendeza zaidi. Hii inachangia katika kuongeza tija na ufanisi wa masomo ya fasihi.

### 5.2.2 Lengo Mahususi la Pili

Utafiti ulifanyika ulikusudia kutimia lengo mahususi la pili la ni kuunda miongozo ya utumiaji wa TEHAMA katika ufundishaji wa fasihi kandishi atika shule za sekondari wilayani Nyagatare nchini Rwanda. Ili kufikia lengo hili, mtafiti alitumia matini mbalimbali kuhusu miongozo ya kukuza stadi za mawasiliano kupitia ufundishaji wa fasihi.

Katika sehemu hii, tasnifu hii inabainisha matokeo ya utafiti kuhusu utoaji wa miongozo ya utumiaji wa TEHAMA ili kuleta ufanisi wa ufundishaji wa fasihi andishi katika shule za sekondari wilayani Nyagatare nchini Rwanda. Kwa hiyo, utafiti uliofanyika ulitoa mwongozo wa utumiaji wa projekta na sladi, usimulizi wa kidijiti na mitandao ya kijamii.

Kwanza, matokeo ya utafiti yametoa mwongozo wa utumiaji wa projekta na sladi. Mwongozo huu unaeleza namna walimu wanavyoweza kutumia projekta na sladi ili kuongeza ufanisi katika ufundishaji wa fasihi. Kwa mfano, walimu wanaweza kuandaa slaidi zenye mifano ya maandishi ya fasihi na kutumia projekta kuonesha kwa wanafunzi. Mbinu hii inasaidia kuboresha uelewa wa wanafunzi kwa kutoa vielelezo vya kuona ambavyo vinafanya masomo yavutie na yaeleweke kwa urahisi. Pia, inawapa walimu uwezo wa kuwasilisha habari kwa njia iliyo wazi na ya kuvutia, ambayo husaidia kuimarisha kumbukumbu na ufahamu wa wanafunzi.

Aidha, matokeo ya utafiti yametoa mwongozo wa utumiaji wa usimulizi wa kidijiti. Mbinu hii inahusisha matumizi ya teknolojia za kidijiti kama vile video, sauti, na michoro ili kufundisha fasihi. Usimulizi wa kidijiti unawawezesha wanafunzi kushiriki zaidi katika masomo kwa kuwapa nafasi ya kuona na kusikia hadithi au maudhui ya fasihi kwa njia inayoamsha hisia na kuvutia. Kwa mfano, walimu wanaweza kutumia video fupi za usimulizi wa hadithi za fasihi ambazo zinasaidia wanafunzi kuelewa na kuhusisha matini wanayosoma na mazingira halisi. Hii si tu inaboresha uelewa wa wanafunzi bali pia inachangia katika kukuza stadi zao za kusikiliza na kuelewa.

Mwisho, matokeo ya utafiti yametoa mwongozo wa utumiaji wa mitandao ya kijamii. Mbinu hii inahusisha kutumia majukwaa ya mitandao ya kijamii kama vile Facebook, Twitter, na WhatsApp ili kufundisha na kujadili fasihi. Walimu wanaweza kuunda vikundi vya majadiliano kwenye mitandao ya kijamii ambapo wanafunzi wanaweza kushirikiana na kujadiliana kuhusu mada za fasihi nje ya darasa la kawaida. Hii inawapa wanafunzi nafasi ya kuuliza maswali, kushiriki mawazo, na kujifunza kutoka kwa wenzao kwa urahisi zaidi. Mbinu hii pia inahimiza wanafunzi kutumia muda wao wa ziada kujihusisha na masomo ya fasihi kwa njia isiyo rasmi na yenye kuvutia.

Kwa ujumla, mwongozo wa utumiaji wa TEHAMA katika ufundishaji wa fasihi wilayani Nyagatare unaonesha jinsi teknolojia inaweza kuboresha ufundishaji na ujifunzaji. Kutumia projekta na sladi, usimulizi wa kidijiti, na mitandao ya kijamii kunasaidia kufanya masomo ya fasihi yawe ya kuvutia, ya kina, na yenye manufaa zaidi kwa wanafunzi. Mbinu hizi si tu zinaboresha uelewa na stadi za mawasiliano za wanafunzi bali pia zinachangia katika kuwaandaa kwa maisha ya kisasa yenye mabadiliko ya kiteknolojia.

### 5.3 Ufaafu wa Nadharia ya Utafiti Iliyotumika

Kulingana na Nadharia ya Uunganisho ya George Siemens, maarifa hupatikana kupitia mifumo ya ushirikiano ambapo watu wanashiriki katika shughuli za kujifunza. Hii inamaanisha kwamba kujifunza siyo tu mchakato wa mtu binafsi bali ni jitihada za pamoja za kubadilishana maarifa na kujenga uelewa. Mifumo hii ya ushirikiano inajumuisha mitandao ya kijamii, mazingira ya mtandaoni, na jamii za kujifunza ambapo washiriki wanaweza kuchangia, kushirikiana, na kujifunza kutoka kwa kila mmoja.

Maarifa hupatikana kwa njia ya mazungumzo, majadiliano, na uhusiano wa kijamii ambao unachochea uhamishaji wa maarifa kutoka kwa wengine na kujenga uelewa mpya kwa washiriki wote. Kwa hiyo, nadharia hii inasisitiza umuhimu wa mazingira yanayojaa uhusiano na mitandao katika kuunda mchakato wa kujifunza wenye tija na endelevu.

Nadharia ya Uunganisho inajumuisha mihimili miwili muhimu ambayo ilitufaa katika utimizaji wa malengo ya utafiti. Mhimili wa kwanza unajumuisha wazo kwamba katika mchakato wa kujifunza, wanafunzi wanapaswa kushirikiana kwa kutumia mawazo yao, kanuni na taarifa za jumla kwa njia inayofaa.

Katika muktadha huu, nadharia hii inasisitiza umuhimu wa TEHAMA kama sehemu muhimu ya mchakato wa kujifunza. Hii ni kwa sababu uhusiano wa mara kwa mara kati ya wanafunzi kutoka asili mbalimbali unawapa nafasi ya kuchagua jinsi ya kujifunza kulingana na mahitaji yao. Mhimili huu ulitusaidia kukamilisha lengo la kubainisha mchango wa TEHAMA katika ufundishaji wa fasihi andishi katika shule za sekondari Wilayani Nyagatare nchini Rwanda.

Mhimili wa pili wa nadharia iliyoongoza utafiti wetu unasisitiza umuhimu wa tathmini ya kibinafsi. Hii inalenga kueleza kwamba matumizi ya TEHAMA katika mchakato wa kufundisha siyo bila kasoro. Kutokana na hili, ni wazi kwamba TEHAMA inaweza kusababisha vikwazo kwa malengo ya ufundishaji na ujifunzaji, na hata kuleta madhara kwa wanafunzi, walimu na jamii kwa ujumla katika maisha yao ya kila siku. Mhimili huu, ulitusaidia kuunda miongozo ya utumiaji wa TEHAMA katika ufundishaji wa fasihi andishi katika shule za sekondari wilayani Nyagatare nchini Rwanda

**5.4 Hitimisho**

Utafiti uliofanyika ulikusudia kuchunguza mchango wa TEHAMA katika ufundishaji wa fasihi andishi katika shule za sekondari Wilayani Nyagatare, nchini Rwanda, na kutoa mwongozo wa matumizi yake yenye ufanisi. Lengo la kwanza lilikuwa kutathmini mchango wa TEHAMA katika ufundishaji wa fasihi. Matokeo yameonesha changamoto kadhaa, ikiwa ni pamoja na upungufu wa vifaa vya kufundishia na mtazamo hasi wa wanafunzi kuelekea somo la fasihi. Walimu pia wanakabiliana na changamoto za kuingiza TEHAMA kutokana na vifaa visivyotosha na mafunzo duni.

Hata hivyo, mikakati kama vile ushirikiano wa vikundi vidogo, maandalizi ya mapema ya masomo, ushirikiano wa walimu, warsha za mara kwa mara, na kuhakikisha miundombinu bora ya TEHAMA iligunduliwa kupunguza changamoto hizi. Kimsingi, TEHAMA ilionesha kuwezesha upatikanaji wa vitabu vya elektroniki na video za ufafanuzi, kuifanya ufundishaji wa fasihi andishi kuwa wa kuvutia zaidi, na kuchochea ujifunzaji huru na ubunifu miongoni mwa wanafunzi.

Lengo la pili lilijikita katika kuunda miongozo ya matumizi ya TEHAMA katika ufundishaji wa fasihi andishi. Utafiti ulitoa mwongozo maalum kuhusu matumizi ya maonyesho na slaidi, hadithi za kidijiti, na mitandao ya kijamii.

Mbinu hizi zinasaidia kuboresha uelewa kwa kutoa mifano ya kuona, hadithi za kuvutia zenye multimedia, na majadiliano ya mtandaoni yanayozidi mipaka ya madarasa ya kawaida. Kwa kuzingatia nadharia ya Uunganisho, ambayo inasisitiza umuhimu wa mazingira ya kujifunza yanayounganisha jamii na mtandao, utafiti ulisisitiza umuhimu wa mazingira ya kujifunza ya kimtandao katika kuimarisha matokeo ya elimu.

Kwa muhtasari, utafiti umebainisha umuhimu mkubwa wa TEHAMA katika kubadilisha ufundishaji wa fasihi andishi katika shule za sekondari Wilayani Nyagatare. Kwa kuzingatia changamoto na kutekeleza mikakati iliyopendekezwa, walimu wanaweza kuunda mazingira ya kujifunza yenye ufanisi na kuvutia zaidi. Mwongozo uliotolewa unalenga kuwawezesha walimu kwa njia za vitendo kuboresha ufundishaji wa fasihi, kwa kutumia TEHAMA kuimarisha uwezo wa kufikiri kwa ujumla, stadi za mawasiliano, na uandishi wa kidijitali miongoni mwa wanafunzi. Kupitisha mikakati hii si tu inaweza kuboresha utendaji wa kitaaluma lakini pia kujiandaa wanafunzi kwa maisha ya baadaye yenye teknolojia ya kisasa.

## 5.5 Mapendekezo

### 5.5.1 Mapendekezo kwa Wanafunzi

Kwanza kabisa, ni muhimu kwa wanafunzi kuendeleza hamu ya kweli katika somo la fasihi andishi kwa kuliona kuwa na umuhimu na kuvutia kama masomo mengine.

### 5.5.2 Mapendekezo Walimu wa Kiswahili

Walimu wanahimizwa kushirikiana na kushiriki katika fursa za maendeleo ya kitaalamu zinazolenga kuunganisha TEHAMA katika ufundishaji wa fasihi. Warsha na vikao vya kujifunza kwa pamoja vinaweza kutoa walimu ujuzi na mikakati ya vitendo ya kutumia rasilimali na zana za kidijitali darasani mwao. Kwa kushirikiana kwa vitendo, walimu wanaweza kuboresha ujuzi wao na kuwa na ujasiri katika kutumia teknolojia ili kuimarisha ufundishaji wa fasihi. Aidha, shule zinapaswa kuweka kipaumbele katika upatikanaji wa vifaa vya TEHAMA vya kutosha, ikiwa ni pamoja na vifaa na uunganishaji wa intaneti, ili kuhakikisha upatikanaji sawa kwa wanafunzi na walimu wote. Pia, walimu wanafaa kufanya maandalizi mapema ili kurahisisha matumizi ya TEHAMA katika ufundishaji wa fasihi andishi.

### 5.5.2 Mapendekezo kwa Wizara ya Elimu ya Rwanda

Wizara ya Elimu nchini Rwanda pendekezwa kuunga mkono walimu wa fasihi kwa kutoa mafunzo maalum na fursa za maendeleo ya mtaala kama ilivyo kwa masomo mengine ya lugha. Hii ni pamoja na maendeleo ya miongozo kamili na rasilimali zinazolenga kuingiza TEHAMA kwa ufanisi katika ufundishaji wa fasihi andishi ya Kiswahili. Kuhakikisha kuwa walimu wanapata mafunzo endelevu yanayolingana na maendeleo katika teknolojia ya elimu kutawezesha kubadilisha mbinu zao za ufundishaji na kukidhi mahitaji yanayoendelea ya wanafunzi katika zama ya kidijiti. Aidha, kutetea sera zinazopatia kipaumbele ujumuishaji wa TEHAMA katika elimu ya fasihi kwa shule za sekondari kutachangia kuimarisha matokeo ya elimu na kuandaa wanafunzi kwa changamoto na fursa za baadaye.

### 5.5.3 Mapendekezo kwa Tafiti Zijazo

Watafiti wa baadaye wanahimizwa kufanya utafiti kuhusu ya athari ya zana na mikakati maalum ya TEHAMA kwa matokeo ya ujifunzaji wa wanafunzi katika fasihi. Utafiti unaolenga kwenye masomo yanayofanana katika mikoa tofauti au kuchunguza njia mpya za hadithi za kidijiti na majukwaa ya kujifunza ya dijitali itatoa ufahamu wa thamani. Aidha, kuchunguza athari za muda mrefu za kuunganisha TEHAMA katika elimu ya fasihi, ikiwa ni pamoja na mchango wake katika uchambuzi wa kifikra, ujuzi wa uchambuzi, na utendaji wa jumla wa kitaaluma, vitachangia katika mwili unaokua wa maarifa ya mazoea bora ya elimu. Kwa kuzingatia maeneo haya, watafiti wanaweza kutoa mapendekezo yaliyotokana na ushahidi ili kuboresha jukumu la TEHAMA katika kubadilisha elimu ya fasihi katika shule za sekondari nchini Rwanda.

## 5.4 Muhtasari wa Sura ya Tano

Sura ya tano inatoa muhtasari wa matokeo ya utafiti uliofanywa, ikigawanyika katika sehemu mbalimbali kama utangulizi, muhtasari wa matokeo, ufaafu wa nadharia iliyotumika, hitimisho, mapendekezo, na muhtasari wa mwisho. Kila sehemu inatoa ufafanuzi wa kipekee kulingana na muktadha wake, ikitoa mwanga wa matokeo ya utafiti na hatua za kuchukuliwa kwa ajili ya mustakabali.

# MAREJELEO


Abdul, R. A., & Alharthi, K. (2016). An Introduction to Research Paradigms. *International Journal of Educational Investigations*, *2*(8), 51–59. https://www.researchgate.net/publication/325022648.

Ahmadi, M. R (2018). The use of Technology in English Language Learning: A Literature Review. *International Journal of Research in English Education (IJREE),* 3 (2)115-125.

Ahn, J-H., & Seo, Y. (2010). Using Social Networking Sites for Teaching Literature: A case study. *Australasian Journal of Educational Technology*, 26(1), 71-83.

Alam, M. A. (2023). Connectivism Learning Theory and Connectivist Approach in Teaching and Learning: A Review of Literature. *Bhartiyam International Journal of Education & Research*, 12(2), 1.

Alfaruque, S., Sultana, S., Rastogi, R., & Jabeen, Z. (2022). Title of the Article. *World Journal of English Language, 13*(1), 278-285. https://doi.org/10.5430/wjel.v13n1p278.

Alnord, M. (2021). The Role of Computer Programs and Digital Tools in Enhancing Literature Teaching: Improving Language Skills and Creating a Better Learning Environment. *International Journal of Educational Technology*, 14(2), 89-102.

Al-Kamel, M., & Chouthaiwale, S. (2020). Use of Information and Communication Technology (ICT) in a Literature Classroom. *Journal of Emerging Technologies and Innovative Research (JETIR)*, 7(6), 1102. https://doi.org/10.1729/journal.23772.

Amin, A. A., & Raba, M. (2017). The Impact of Effective Teaching Strategies on Producing Fast and Good Learning Outcomes. *International Journal of Research-Granthaalayah*, 5(1), 43–58. https://doi.org/10.5281/zenodo.259563.

Ammade, S., Mahmud, M., Jabu, B., & Tahmir, S. (2018). Integrating Technology in English Language Teaching: Global Experiences and Lessons for Indonesia. *International Journal of English Linguistics*, *8*(6), 107-118. https://doi.org/10.5539/ijel.v8n6p107.

Androutsopoulos, J. (2015). Networked Multilingualism: Some Language Practices on Facebook and Their Implications. *International Journal of Bilingualism* 19.2, 185–205.

Barash, D.P. (2005). B. F. *Skinner Revisited: The Chronicle of Higher Education*. Washington: Vintage Books.

Benson, P., & Thurman, B. W. (2013). Teaching Literature in a Digital Age: Why Social Networking Services Matter. *Journal of Adolescent & Adult Literacy*, 57(2), 132-143.

Besha, R.M. (2007). *Utangulizi wa Lugha na Isimu*. Dar- es -Salaam: Macmillan Aidan.

Boruah, N. (2022). Impact of ICT in education. *International Journal of Health Sciences*, 1818–1822. https://doi.org/10.53730/ijhs.v6nS2.5397.

Brink, H. I. L. (1993). Validity and reliability in qualitative research. *Curationis*, *16*(2) 214-227. https://doi.org/10.4102/curationis.v16i2.1396

Bryman, A. (2006). Integrating quantitative and qualitative research: How is it done? *Qualitative Research*, 6(1), 97–11.

Byram, M. (1997). *Teaching and Assessing Intercultural Communicative Competence*. Clevedon, UK: Multilingual Matters.

Cahyani, H., & Cahyono. (2013). Teachers' Attitudes and Technology Use. *TEFLIN Journal*, 23, 130-148.

Chacha S. R. (2016). *Uhusiano wa Mikakati ya Ufundishaji wa Fasihi ya Watoto ya Kiswahili na Umilisi wa Kusoma katika Shule za Msingi, Kasarani, Kaunti ya Nairobi, Kenya*. [Tasnifu ya Uzamili, Chuo Kikuu cha Kenyatta]. Haijachapishwa.

Courville, K. (2011). *Technology and Its Use in Education*: Present Roles and Future Prospects. The 2011 Recovery School District Technology Summit. Baton Rouge, Louisiana.

Creswell, J. W., & Poth, C. N. (2017). *Qualitative Inquiry and Research Design*. Choosing Among Five Approaches (Toleo la 4). Thousand Oaks, CA: SAGE Publications.

Daskalovska, N. & Dimova, V. (2012). Why Should Literature Be Used in The Language Classroom? *Procedia - Social and Behavioral Sciences*. 46 (3), 1182-1186. https://doi.org/10.1016/j.sbspro.2012.05.271.

Demiröz, H. (2019). Incorporating and Combining Technology and Literature into Language Teaching to Enhance Creativity. *Ana Dili Eğitimi Dergisi*, 7(1), 65-78. https://doi.org/10.16916/aded.448839.

Drolet, M. J., Rose, D. E., Leblanc, J. C., Ruest, M., & Williams, J. B. (2023). Ethical Issues in Research: Perceptions of Researchers, Research Ethics Board Members and Research Ethics Experts. *Journal of Academic Ethics*, 21(2), 269–292. https://doi.org/10.1007/s10805-022-09455-3.

Fellenz, M. R., & Brady, M. (2007). The Importance of ICT in Education: The Kenyan Government's Initiatives. *International Journal of Education and Development using Information and Communication Technology (IJEDICT)*, 3(1), 109-119.

Garcia, M., & Hernandez, S. (2019). Enhancing Engagement through Multimedia: Using PowerPoint in Literature Classes. *Journal of Teaching and Learning Technology*, 25(1), 18-30.

Gomez, R. (2022). Students' Perception of Literature as a Difficult Subject and Its Impact on Learning Outcomes. *Journal of Educational Psychology*, 15(3), 233-245.

Hafifah, G. N. (2019). *Information and Communication Technology (ICT) in English Language Teaching*. Surabaya, Indonesia: The University of Muhammadiyah Surabaya Press.

Haidari, M., Katawazai, R., & Mohd Yusof, S. (2020). The Use of Social Media and Wikis in Teaching Writing Skills: A Review Article. *International Journal of Interactive Mobile Technologies (IJIM)*, 14(16), 168-179. https://doi.org/10.3991/ijim.v14i16.15531.

Hambur, F. M. (2018). How Group Discussion and Contemporary Literature Increase Students' Motivation in English Literature Subjects: A Case Study at 4th Semester Students of Stikubank University in 2017/2018 Academic Year. *Dinamika Bahasa Dan Budaya*, *13*(2), 29-42. https://doi.org/10.35315/bb.v13i2.6455.

Harding, T. S. (2013). *Analysing data in qualitative research*. Ilisomwa Tarehe14, Agosti, 2024, from https://shorturl.at/lAPWX.

Hashemi, M., Azizinezhad, M., & Farokhi, M. (2012). Power Point as an Innovative Tool for Teaching and Learning in Modern Classes. *Procedia - Social and Behavioral Sciences*, *31*, 559-563. https://doi.org/10.1016/j.sbspro.2011.12.103.

Hattie, J. (2009). *Visible Learning: A Synthesis of Over 800 Meta-Analyses Relating to Achievement*. London: Routledge.

Holmqvist, M. (2019). Lack of Qualified Teachers: A Global Challenge for Future Knowledge Development. In *Teacher Education in the 21st Century*. IntechOpen. https://doi.org/10.5772/intechopen.83417.

Ishtiaq, M. (2019). Book Review Creswell, J. W. (2014). Research Design: Qualitative, Quantitative and Mixed Methods Approaches (Toleo ya 4.). Thousand Oaks, CA: Sage. *English Language Teaching*, *12*(5), 40. https://doi.org/10.5539/elt.v12n5p40.

Işıklı, C., & Tarakçıoğlu, A.Ö. (2017). Investigating problems of English Literature Teaching to EFL high School Students in Turkey with Focus on Language Proficiency. *Journal of Language and Linguistic Studies*, 13(2), 82-95.

Jilcha Sileyew, K. (2020). Research Design and Methodology. In *Cyberspace*. IntechOpen. https://doi.org/10.5772/intechopen.85731.

Jones, K., & Patel, R. (2018). Integrating Technology: Using PowerPoint to Teach Literature Analysis. *English Journal*, 107(4), 75-82.

Jones, T., & Cuthrell, K. (2011). YouTube: Educational Potentials and Pitfalls. *Computers in the Schools*, 28(1), 75-85. https://doi.org/10.1080/07380569.2011.553149.

Jones, T., & Patel, R. (2018). *Innovative Teaching Methods: Enhancing Student Motivation and Understanding through Technology*. New York, NY: Academic Press

Kamal, T. C., & Salih H. (2020). Challenges Encountering Literature Teachers of EFL Classes in Salahaddin University/ Erbil. *Twejer*, *3*(2), 1209–1248. https://doi.org/10.31918/twejer.2032.27.

Karakaya, E., & Kahraman, A. (2013). Students' Attitudes towards Literature Use and its Effects on Vocabulary Learning. *International Journal of Applied Linguistics & English Literature*, *2*(5), 155–166. https://doi.org/10.7575/aiac.ijalel.v.2n.5p.155.

Karantalis, N., & Koukopoulos, D. (2022). Utilizing Digital Storytelling as a Tool for Teaching Literature through Constructivist Learning Theory. *SN Social Sciences*, *2*(7), 109-121. https://doi.org/10.1007/s43545-022-00412-w.

King, L. J. (2000). Teaching German Literature through the Web: Processes and outcomes. Die Unterrichtspraxis. *Teaching German*, 5(2), 62-70.

Koroleva, D. O. (2020). *Information and Communication Technologies in Russian Education: Background and Outlook* (pp. 99–117). https://doi.org/10.1007/978-981-15-6157-3_6.

Kothari, C.R. (2012). *Research Methodology- Methods and Techniques.* New Delhi. Willey Eastern Limited.

Lazar, G. (1993). *Literature and Language Teaching. A Guide for Teachers and Trainers*. Cambridge University Press.

Machmud, K. (2011). *The Integration of ICT in Curriculum Implementation: Enhancing Language Teaching and Learning*. Journal of Educational Technology, 5(2), 34-45.

Majid, U. (2018). Research Fundamentals: Study Design, Population, and Sample Size. *Undergraduate Research (UR) Journal*, *2*(1), 1–7. https://doi.org/10.26685/urncst.16.

Makaun, L. (1990). Efforts to Improve the Education Sector through ICT in China. Journal of *Educational Technology*, 12(4), 78-85.

Martins, F. S., Cunha, J. A. C. da, & Serra, F. A. R. (2018). Secondary Data in Research – Uses and Opportunities. *Revista Ibero-Americana de Estratégia*, *17*(04), 01–04. https://doi.org/10.5585/ijsm.v17i4.2723.

Mbodila M, Jones T. and Muhandji K. (2013) Integration of ICT in education: key challenges. *International Journal of Emerging Technology and Advanced Engineering*, 11(3), 515-520.

Mechlova, E & Malcik. M (2012). *ICT in Changes of Learning Theories*. Emerging eLearning Technologies & Applications (ICETA), 2012 IEEE 10th International Conference. 10.1109/ICETA.2012.6418326.

Meskill, C., & Ranglova, K. (2000). *Sociocollaborative Language Learning in Bulgaria*. In M. Warschauer & R. Kern (Eds.), Network-based language teaching: Concepts and practice. Cambridge: Cambridge University Press.

Mishra, P., & Koehler, M. J. (2006). Technological pedagogical content knowledge: A framework for teacher knowledge. *Teachers College Record*, 108(6), 1017-1054.

Mofareh, A. (2019). The Use of Technology in English Language Teaching, Frontiers. *Education Technology*, 2 (3): 168.

Mohd, N, N. S., & Muhmad, N.N. A. A. (2023). The Challenges in the Teaching of English Literature. *Journey: Journal of English Language and Pedagogy*, *6*(1), 130–147. https://doi.org/10.33503/journey.v6i1.2640.

Mosha, H. J. (2017). *The role of ICT in education: Enhancing the Teaching and Learning of Literature in Secondary Schools*. Dar es Salaam, Tanzania: Education Publishing House.

Msafiri, M.M., Kangwa, D. & Cai, L. A. (2023) Systematic Literature Review of ICT Integration in Secondary Education: What Works, What Does not, and What Next?.*Discov Educ* 2(1), 1-44 https://doi.org/10.1007/s44217-023-00070-x

Msigwa A (2019). Mchango wa Media za Video katika Ufundishaji wa Kiswahili kwa Wageni. *Mulika*, 38: 74-86.

Mukama E. & Andersson S.B. (2008). Coping with change in ICT-Based Learning Environments: Newly Qualified Rwandan Teachers‟ Reflections. *Journal of Computer Assisted Learning* 24, 156 -166.

Munck, G. L. (2004). *Tools for Qualitative Research*. Ilisomwa Tarehe 11,Julai, 2024, kutoka https://shorturl.at/dxzL0.

Munyengabire, S. (2024). TEHAMA na Athari zake katika Ufundishaji na Ujifunzaji wa Kiswahili katika Shule Teule za Sekondari Nchini Rwanda. *East African Journal of Swahili Studies*, 7(1), 155–169. https://doi.org/10.37284/jammk.7.1.1795.

Nanda, P., & Kumar, V. (2021). Social Media Analytics: Tools, Techniques and Present-Day Practices. *International Journal of Services Operations and Informatics*, *11*(4), 1. https://doi.org/10.1504/IJSOI.2021.10039351.

Njogu, K na Chimerah, R (1999). *Ufundishaji wa Fasihi: Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.

Nkwera, F.M.V. (1978). *Sarufi na Fasihi Sekondari na Vyuo*. Dar es Salaam: TPH.

Osario, M. (2017). The Role of Technology in Overcoming Challenges in English Literature Education. *Journal of Educational Technology*, 5(2), 45-58.

Palys, T. (2008). *Purposive sampling*. In L.M. Given (Ed.). The Sage Encyclopedia of Qualitative Research Methods. (Vol.2). Sage: Los Angeles.

Peck, J. (1989). Using storytelling to Promote Language and Literacy Development. *The Reading Teacher*, 43(2), 138-141.

Prensky, M. (2001). Digital Natives, Digital Immigrants Part 1. *On the Horizon*, 9(5), 1-6.

Rapley, T. (2007). Doing Conversation, Discourse and Document Analysis. London: Sage.

Ratheeswari, K. (2018). Information Communication Technology in Education. *Journal of Applied and Advanced Research*, 5 (2), 45-S47. https://doi.org/10.21839/jaar.2018.v3iS1.169.

Redman, L.V., & Mory, A.V. (2015). *Research Methodology: An Introduction Meaning of Research Objectives of Research*.Ilisomwa tarehe 15,7,2024 kutoka https://api.semanticscholar.org/CorpusID:9043321/

Reinhardt, J. (2019). Social Media in Second Aad Foreign Language Teaching and Learning: Blogs, Wikis, and Social Networking. *Language Teaching*, 52(1), 1–39.

Rodrigues, F., & Ravasco, C. (2020). The Role of Field Trips. 2192–2197. https://doi.org/10.21125/edulearn.2020.0682.

Rutledge, P. B., & Hogg, J. L. C. (2020). In-Depth Interviews. In The International Encyclopedia of Media Psychology (pp. 1–7). Wiley. https://doi.org/10.1002/9781119011071.iemp0019.

Ryan, R. M., & Deci, E. L. (2000). Intrinsic and Extrinsic Motivations: Classic Definitions and New Directions. *Contemporary Educational Psychology*, 25(1), 54-67.

Rwabizambuga, A. (2018). The Competence-Based Curriculum in Rwanda: Opportunities and Challenges for the Integration of ICT in Teaching and Learning. *International Journal of Education and Research*, 6(11), 167-178.

Sarah, E.I. (2006). Bending Behavior American Scientist. *Research Triangle Park*. 94(3), 267-286.

Schauman, E. (2001). *The Role of Information and Communication Technology in Enhancing Education for Scientists and Professionals in Russia*. Digital Education Review, 3(2), 45-57.

Schunk, D. H., Pintrich, P. R., & Meece, J. L. (2008). *Motivation in Education: Theory, Research, and Applications* (3rd ed.). Pearson Education.

Sharma, K. (2021). Challenges and Opportunities of Integrating ICTs in ELT and Literature Teaching. *Journal of NELTA Gandaki*, 4(1–2), 133–144. https://doi.org/10.3126/jong.v4i1-2.42653.

Skinner, B.F. (1976). *About Behaviourism.* New York: Vintage Books.

Spjeldnæs, K., & Karlsen, F. (2022). How Digital Devices Transform Literary Reading: The impact of e-books, audiobooks and online life on reading habits. *New Media & Society*, 3(1). https://doi.org/10.1177/14614448221126168

Stanley, I. (2018). The Contribution of ICT in the Teaching of Kiswahili: Enhancing Student-Teacher Interaction and Language Skills. *Journal of African Languages and Linguistics*, 10(3), 150-162.

Sürücü, L, & Maslakçi, A. (2020). Validity and Reliability in Quantitative Research. *Business & Management Studies: An International Journal*, *8*(3), 2694–2726. https://doi.org/10.15295/bmij.v8i3.1540.

Tayib, A., & Hassan, S. (2020). *Challenges in Teaching Literature Despite the Inclusion of ICT in Education for Sustainable Development*. Journal of Educational Research and Reviews, 8(4), 55-66.

Wamitila, K.W. (2003). *Kamusi ya Fasihi, Istilahi na Nadharia*. Nairobi. Focus Group Books

Warschauer, M., & Healey, D. (1998). Benefits and Problems of Technology Integration in K-12 classrooms: A review of the literature. *Educational Research Review*, 2(4), 1-23.

Warschauer, M., & Kern, R. (2000). *Network-Based Language Teaching*: Concepts and Practice. Cambridge University Press.

Watson, D.M. (2001). Pedagogy before Technology: Re-thinking the Relationship between ICT and Teaching. *Education and Information Technologies*, 6, 4, 251-266.

Zainal, A. (2012). ESL teachers' use of ICT in teaching English literature: An analysis of teachers' TPCK. *Procedia - Social and Behavioral Sciences*, 34, 234–237. https://doi.org/10.1016/j.sbspro.2012.02.047.

Zeng, W. (2022). An empirical research on China's policy for ICT integration in Basic Education from 1988 to 2021. *Educational Technology Research and Development*, 70(3), 1059–1082. https://doi.org/10.1007/s11423-022-10079-y.

# VIAMBATISHO

## Kiambatisho I. Mwongozo wa Usaili kwa Walimu wa Kiswahili

1. Bainisha changamoto unazokabiliana nazo unapofundisha fasihi andishi.
2. Je, unafikiri kwa namna gani changamoto hizo zinaweza kutatuliwa kwa matumizi ya TEHAMA?
3. Kama mwalimu wa Kiswahili ni changamoto gani unazokabiliana nazo unapofundisha fasihi andishi kwa kutumia TEHAMA?
4. Je, kama mwalimu wa Kiswahili, ni mbinu gani unazozitumia ili kuepukana na changamoto za ufundishaji wa wa fasihi andishi kupitia utumiaji wa TEHAMA?
5. Je, TEHAMA ina mchango gani katika ufundishaji wa fasihi andishi ya Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za sekondari hii?
6. Ni mambo gani muhimu ya kuzingatia katika kuandaa mwongozo wa matumizi ya TEHAMA katika ufundishaji wa fasihi ya Kiswahili kwa wanafunzi wa shule za sekondari?

**Kiambatisho II. Mwongozo wa Usaili kwa Wakurugenzi na Viongozi wa Masomo**

1. Je, katika shule hii, mwalimu wa Kiswahili anatumia TEHAMA vipi anapofundisha somo la fasihi? (How does a Kiswahili teacher utilize ICT in teaching literature in this school?)
2. Ni changamoto gani anazokabiliana nazo mwalimu wa Kiswahili anapofundisha fasihi kupitia matumizi ya TEHAMA? (What challenges does a Kiswahili teacher face when teaching literature through ICT?)
3. Ni mbinu gani ambazo mwalimu wa Kiswahili anaweza kutumia ili kuepukana na changamoto za ufundishaji wa fasihi kupitia matumizi ya TEHAMA? (What strategies can a Kiswahili teacher employ to overcome the challenges of teaching literature through ICT?)
4. Je, TEHAMA inaweza kumfaa vipi mwalimu wa Kiswahili katika ufundishaji wa fasihi kwa wanafunzi wa shule za sekondari hii? (How can ICT benefit Kiswahili teacher in teaching literature to secondary school students?)

**Kiambatisho III. Mwongozo wa Ushuhudiaji**

| **1. Mchango wa TEHAMA katika Ufundishaji wa Fasihi katika Shule za Sekondari Wilayani Nyagatare Nchini Rwanda** | | |
|---|---|---|
| a) Mwalimu wa Kiswahili anapoandaa somo la fasihi anabainisha vifaa vya TEHAMA vitakavyotumiwa katika ufundishaji wa somo? | **Ndiyo** | **Hapana** |
| | Maoni<br>…………….. | Maoni<br>…………………… |
| b) Mwalimu wa Kiswahili anatumia TEHAMA anapofundisha somo la fasihi? | **Ndiyo** | **Hapana** |
| | Maoni<br>…………….. | Maoni<br>…………………… |
| c) Je, mwalimu anatumia TEHAMA anapotathmini somo la fasihi? | **Ndiyo** | **Hapana** |
| | Maoni<br>…………….. | Maoni<br>…………………… |
| d) Je, ni vifaa gani vya KITEHAMA anavyovitumia mwalimu wa Kiswahili katika ufundishaji wa fasihi? | ……………………………………..<br>………………………………….. | |
| e) Mwalimu wa Kiswahili anatumia TEAHAMA vipi katika ufundishaji wa fasihi? | ……………………………………..<br>………………………………….. | |

| **2. Vizuizi vya Utumiaji wa TEHAMA katika ufundishaji wa fasili** | |
|---|---|
| **Vizuizi** | **Mbinu za Kuondoa Vizuizi** |
| 1. ……………………………….. | 1. ……………………………….. |
| 2. ……………………………….. | 2. ……………………………….. |
| 3. ……………………………….. | 3. ……………………………….. |
| 4. ……………………………….. | 4. ……………………………….. |

**Kiambatisho IV. Mwongozo wa Uchanganuzi Matini kuhusu Mwongozo wa Utumiaji wa TEHAMA ili Kuleta Ufanisi wa Ufundishaji wa Fasihi**

| Jina la Matini | Mwandishi & Mwaka | Mwongozo wa Utumiaji wa TEHAMA katika Ufundishaji wa Fasihi | Taarifa Kutoka katika Matini |
|---|---|---|---|
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |
| | | | |

**Kiambatisho V. Kibali cha Kukusanya Data kutoka Chuoni**

UNIVERSITY of RWANDA

COLLEGE OF EDUCATION

RESEARCH AND INNOVATION UNIT

Rukara, 17th July 2024
Ref: DRI-CE/039(b)/EN/gi/2024

**The Mayor**
**Nyagatare district**
**Eastern Province**
**Rwanda**

**Re: A Research recommendation letter for Mr Frodouard Tulinumukiza (Reg No: 222011736)**

I am pleased to introduce **Mr Frodouard Tulinumukiza:** our student enrolled in the Master of Education in Kiswahili Education at the School of Education of UR-CE. He is conducting research entitled: **"The Contribution of ICT in Teaching Written Literature in Selected Secondary Schools in Nyagatare District, Rwanda"** The research participants for this study are students of the combination of languages and teachers of Kiswahili, Dean of Studies and Head Teachers in selected secondary schools of Nyagatare district.

Thus, we kindly request his permission to collect data from the identified secondary schools of the Nyagatare district.

Your support to him in conducting this study is highly appreciated.

COLLEGE OF EDUCATION
UNIVERSITY of RWANDA
RESEARCH AND INNOVATION UNIT

**Assoc. Prof. Eugene NDABAGA**

Director of Research and Innovation
University of Rwanda-College of Education
E-mail: ndabagav@yahoo.ie
Mobile: +250788308862
**Cc:**

- Principal, UR-CE
- Dean, School of Education
- Dr Wallace K. Mlaga (Supervisor)

EMAIL: dri.ce@ur.ac.rw P.O. Box: 55 Rwamagana WEBSITE: www.ur.ac.rw

## Kiambatisho VI. Idhini ya Itikeli ya Utafiti

UNIVERSITY of RWANDA

COLLEGE OF EDUCATION

RESEARCH AND INNOVATION OFFICE

Rukara, 17th July, 2024
Ref: DRI-CE/039(a)/ EN/gi/2024

**Mr Frodouard TULINUMUKIZA**
**Reg No: 222011736**
Master Student
Master of Education in Kiswahili Education
School of Education
UR-CE

Dear Mr Tulinumukiza,

**RE: RESEARCH ETHICAL CLEARANCE FOR YOUR STUDY**

Following your application for research clearance for your study entitled: **"The Contribution of ICT in Teaching Written Literature in Selected Secondary Schools in Nyagatare District, Rwanda;"**

Having reviewed your application and being satisfied with your protocol (research topic, interview schedule, and informed consent): your study is ethically acceptable. This ethical clearance shall last 18 months and is renewable upon your request and presentation of the progress report to the UR-CE Research Screening and Ethics Clearance Committee (RSEC-C) through the Research and Innovation Unit. Please note that you must apply for ethical clearance before making changes in the protocol during the implementation phase. The Research and Innovation Unit shall receive a final copy of your study report at the end of your study.

We wish you success in your study.

COLLEGE OF EDUCATION – UNIVERSITY of RWANDA – RESEARCH AND INNOVATION UNIT

**Assoc. Prof. Eugene NDABAGA**
Chairperson, UR-CE RSEC-C
Director of Research and Innovation Unit
Tel.: 250788308862
Email: ndabagav@yahoo.ie
UR-College of Education

**Cc:**

- The Principal, CE
- Dean, School of Education
- Dr Wallace K. Mlaga, Supervisor

EMAIL: dri.ce@ur.ac.rw P.O. Box: 55 Rwamagana WEBSITE: www.ur.ac.rw

**Kiambatanisho VII. Kibali cha Kukusanya Data kutoka kwa Wilaya ya Nyagatare**

REPUBLIC OF RWANDA

Nyagatare, On 15th /05/2024
No.................07/05/02/HR/NY/08

EASTERN PROVINCE
NYAGATARE DISTRICT
B.P 20 NYAGATARE
info@Nyagatare.gov.rw

TO: TULINUMUKIZA Frodouard- A student of UR, College of Education

Ref: Research Approval Letter

I **HATEGEKIMANA Fred,** District Executive Secretary of Nyagatare, certify the acceptance of you as Student from University of Rwanda, College of Education to do research in Nyagatare District upon your research on project entitled "**The contribution of ICT in Teaching written Litereature. Case Study GS Bufunda& TSS, GS Cyabayaga & TSS, GS Kabare II, GS Nyagatare and GS Gishororo.** The research will start on 20th May to 20th June 2024, you will work with under supervision of Director of Education Unit

Best Regards.

**HATEGEKIMANA Fred**

**District Executive Secretary of Nyagatare**

CC:

**Mayor of Nyagatare District**

**Vice Mayors (Both)**

**Corporates Service Division Manager**

**University of Rwanda- College of Education**

**Kiambatanisho VIII.Ripoti ya Mfanano**

Masters Thesis

ORIGINALITY REPORT

| 18% | 16% | 6% | 14% |
|---|---|---|---|
| SIMILARITY INDEX | INTERNET SOURCES | PUBLICATIONS | STUDENT PAPERS |

PRIMARY SOURCES

| | | |
|---|---|---|
| 1 | Submitted to University of Rwanda<br>Student Paper | 6% |
| 2 | journals.eanso.org<br>Internet Source | 1% |
| 3 | Submitted to University Der Es Salaam<br>Student Paper | 1% |
| 4 | repository.out.ac.tz<br>Internet Source | 1% |
| 5 | www.researchgate.net<br>Internet Source | <1% |
| 6 | link.springer.com<br>Internet Source | <1% |
| 7 | www.sciedupress.com<br>Internet Source | <1% |
| 8 | Submitted to Southern New Hampshire University - Continuing Education<br>Student Paper | <1% |
| 9 | Submitted to Monash University<br>Student Paper | <1% |